# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

# Verbatim Report Of

# DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MALAVA CONSTITUENCY HELD AT MATETE SALVATION ARMY CHURCH

ON

15TH OCTOBER, 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MALAVA CONSTITUENCY HELD AT MATETE SALVATION ARMY CHURCH ON 15.10.02.**

**Present**

1. Com. Kavetsa Adagala

**Secretariet in Attendance**

1. Vincent Watako - Asst. Programme Officer
2. Patricia Mwangi - Verbatim Recorder

Amaswache - District Co-ordinator

**Member of the 3C's**

1. Mr. Makokha Wanjia - Chairman
2. Jotham Rapondo - Secretary
3. Mr. Jonstone Chibeu - member
4. Mrs. Esther Wehayai - “
5. Mrs. Sarah Mukolwe - “
6. Mr. Tindi Makanya - “
7. Mrs. Gladys Webuye - “
8. Mr. Joram Mukaisi - “
9. Cllr. Muchiti Tadayi - “
10. Cllr. Luka Nalyanya - “
11. Mr. Cephar Rumbosta - “

The meeting started at 10.45AM

**Prayers**: Hamjambo? Katika jina la Yesu Kristo, tuamini sote na tuombe.

Baba katika jina la Yesu Kristo ni asante wakati huu siku ya leo Baba, siku ile ambayo wewe mwenyewe ulichagua ukatuandalia, sisi sote tukutane hapa kwa jinsi au kwa ajili ya kutengeneza mambo yanayo tuhusu kulingana na Kenya yetu.

Baba ni asante kwa wale wote ambao wamefika, ni asante kwa wale ambao wako bado njiani, ni asante kwa wale ambao wangali nyumbani, na Baba hao wote ninawaweka mikononi mwako, upate kuwaongoza, uwape fikira nzuri Baba wote wafike hapa, na sisi sote tuambatane kwa kutengeneza au kwa kuungana kwa yale ambayo yanatakikana tufanye hapa.
Baba wale ambao wamekalia mkutano huu ninawaweka mikononi mwako. Baba uwajaalie na ongeo lote Baba, lisiwe lao wenyewe bali litoke kwa roho wako mtakatifu. Baba ni asante kwa wale ambao hawajafika, tunatarajia watafika, ni asante yote ambayo tunaenda kuongea, Baba isiwe yetu, itoke kwa roho wako mtakatifu, tumalize salama kwa usalama wako. Ni asante Baba, ni katika jina la Yesu Kristo naomba na kuamini. AMEN.

**Amaswache:** Wakaazi wa Malava Constituency, Commissioner, Chairman wa Malava CCC Mr. Makokha Wanjia, Honourable Werengai na wengine walio hapa hamjambo nyote?

**Audience**: Hatujambo.

**Amaswache:** Yangu hayatakuwa mengi bali machache. Kitu cha kwanza nitawajulisha hapa Commissioner Kavetsa naye atawajulisha wengine ambao wametoka kwenye Commission na kabla hajafanya hivyo, nitawasimamisha Malava CCC wasimame kidogo watu wawaone na wawajue, please. Hao wenye watasimama, wengine bado wako kule nje ndio wanachama wa Malava CCC, na katikati pale ni Chairman Mr. Makokha Wanjia, huyu ni mwanachama Mrs. Esther Werengai, na yule ni katibu Mr. Rapando. Nimeona mwingine ndiYo yule pale bado anakuja Mr. Johnson Chebeu na wengine watakuja mkutano ukiendelea, please sit.

Kwa ufupi, tulichagua center ya Matete, nilichagua mwenyewe kuwarudishia watu wa Matete asante kwamba tulipokuwa na hearings, Matete recorded the highest number in Lugari District, sasa nikaona kwa Constituency ya Malava watu wamenipigia simu wakifanya complaints, mbona hatukupeleka mkutano Malava kwa center huko, nikawaambia nitarudisha mkutano kwa wale wenye walipeana maoni mengi, na Matete registered the highest, mji-congratulate wenyewe mjipigie makofi.

Commissioner, sina mengi I will hand over the programme to you, thank you.

**Com. Adagala:** Mrembe mwosi?
**Audience:** mrembe

**Com. Adagala:** Mrembe gandi?
**Audience:** mrembe.

**Com. Adagala**: *Kuyanzi guduka hano*, tumefurahi sana kufika hapa na nimefurahi hasa kwa sababu tumefanya na District Co-ordinator kazi, sikufika hapa wakati ule, lakini yeye tunahusiana sana, anapanga mipango na hata akifika ofisi, tuna office headquaters tunaonana, na ameniambia mambo yenu na pia nafikiri kwa Western Province, Lugari District ndiyo ilikuwa na the highest written memoranda. Yaani mumesoma eh sivyo, Wa Kabras wamesoma, isipokuwa Mheshimiwa Shitanda aliniambia wanawake wa Kabras hawajasoma, hiyo ni kweli?

**Audience**: ……….. wamesoma sana.

**Com. Adagala:** Tulipambana naye, akasema kamati ni ngumu kwa sababu wanawake wa Kabras hawajasoma. Haya sasa nitaona kama wako leo, na ni jukumu la wanawake ambao wako kwa kamati kuleta wanawake, ku-mobilize wanawake. Sasa nimeona huyu Committee member ameingia peke yake, mwingine alikuwa hapa peke yake na kweli ni jambo la kushangaza kwa sababu watu wa Malava hawazaliwi na wanawake, situweke kwa historia hiyo na kwa science, hawazaliwi na wanawake. Kama hamzaliwi na wanawake, na mnazaliwa na wanawake na hawako hapa, inaonyesha mumewakalia sana.

Si ni moja, hamzaliwi na wanawake au mumewakalia sana, wako lakini mumewakalia sana. Kila mwanaume ana wanawake wawili kwa maisha yake, mama yake na mke wake, halafu wasichane wake, binti wake wapo. Hata hamtaki binti wenu wajue mambo ya karne mpya. Haya, nani alimualika nyinyi? Hallo Chairman wa Committee, who invited people?

**Interjections:**

**Com. Adagala**: Excuse me, ninazungumza na Chairman, sitaki vitu vya kuropoka ropoka hapa.

**Chairman:** Alikuwa Co-ordinator ndiye aliandika notice kwa watu wote.

**Com. Adagala**: Ya watu wote,

**Chairman:** Ya watu wote.

**Com. Adagala**: Sio mtu alialikwa?

**Chairman**: Hapana.

**Com. Adagala**: Mtu hakuandikiwa barua anaalikwa. I am telling you, mnafanya makosa makubwa sana, hata dhambi mbele ya Mungu. Kuna Christian Organization in Geneva ya dunia nzima na inasema, wanataka iwekwe kwa orodha ya dhambi, kudhulumu wanawake na kuwakalia, iwe dhambi. Kwa sababu yale mnafanya ni dhambi, I want to know where the women are na vijana, vijana wako wapi? Yaani wazee ndio wako Malava? I am serious.

**Esther Werengai**: Asante sana Ms. Kavetsa Commissioner, mimi kama mkaaji wa Matete, … Okay, my name is Esther Werengai, Committee member. Mimi kama mkaaji wa Matete na kama ninajua watu wa Matete…..,

**Com. Adagala**: One of the reasons?

**Esther Werangai:** Sababu moja ambayo wamama hawahudhurii mikutano, wamama kama unasema wanakaliwa. Tumewaambia lakini wamama wenyewe wengi wao hawapendi kuenda kwa mikutano na wengine wanakaliwa na waume wao, ma -bwana zao. No, Rhoda hiyo ni haki, wamama wengi wao hawapendi kwenda kwa mikutano wenyewe na wengine wanakaliwa sana. Those are two main important reasons.

**Com. Adagala**: Therefore I don't see why I should talk to you about the Constitution because it is about freedom and equality. So I don't see why I should talk to people ambao wako slave drivers, ambao wanakalia wengine, about freedom and equality.

**Amaswache**: Hallo nisikizeni kidogo, Commissioner, kama Co-ordinator nataka nikuambie kitu kimoja. Wamama wa kwetu hapa wameanza kuingia pole pole, give us one hour, women will be more than men here, they are going to come. You know they have got their home ……

**Com. Adagala**: Hii kazi tumechelewa, sasa mnasema watu watakuja, sasa, tutamaliza saa ngapi? Hamna sitima hapa, tutamaliza saa ngapi? Haya funuweni hiyo Constitution yenu. Please open to the table of contents, I don't want to hear anything about people who are oppressed. Hapo kwa Constitution yenu… No, no, have you given out? So where are they? Mtapata copies za Katiba, wangapi wana copies za Katiba? Ndiyo hiyo iko peke yake, hebu nione copies, weka juu nione? Mzee wacha nikuambie pengine hiyo ndiyo Prof. Ghai amekutumia, utamwamini zaidi, hiyo ndiyo iko, hiyo ndiyo Prof. Ghai akonayo pia okay?

That is what there is, what would you like? Could you put, weka hiyo juu nione, wangapi wanayo. Watu wangapi? Is this thing working, tafadhali keti chini, keti chini mtapata. Please sit, Chairman I want to see an active committee. Patricia please, ketini chini, madam come and distribute these things stop seating there, come and distribute.

Vincent, how many are in a bundle? Okay you should double they are a hundred not two, is it one bundle? Yeah, you know people will come afterwards, you have to have some for them. Haya chukuweni Katiba yenu, tufunue ukurasa wa kwanza, okay, kila mtu ana nakala? Haya. Hapa na mimi, mimi ni Commissioner Kavetsa Adagala, kwetu ni Mudete, yaani Matete kwetu ni Mudete mlogori, tuko Commissioners watatu. Tafadhali ambia huyo mtu… Tuko Commissioners watatu kwa Commission Western, Nancy Baraza, Mutakha Kangu na mimi.

Leo mimi nitakuwa hapa, kesho Lumakanda itakuwa Mutakha Kangu. Nancy Baraza alikuwa upande ule wa Bungoma na kadhalika. Tulikuwa na afisa mwingine Nyegenye, alikuwa upande wa Busia na sisi tumefanya Vihiga district tumemaliza, sasa tumekuja Lugari na tutaendelea halafu tutakuwa Kakamega, Lurambi na tutaenda. Mutakha Kangu sasa ako Shinyalu. Kila

mahali Kenya, kuna kikao kama hichi cha Tume ya Kurekebisha Katika, kuzungumzia kuhusu mambo ya Katiba, kukagua na kuona kama kuna mahali pa kurekebisha zaidi. Kweli wale wazee na hata vijana sasa munaweza kukubali, Tume nyingine yeyote haijawahi kutoa ripoti yao sivyo?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Adagala:** Sheria yetu ya Bunge ilitengeneza ilisema, we shall read the report and the draft bill to the public. Ndio hiyo, nyinyi mlipata kwanza kabla mtu yeyote hajapata, hata Chairman wa Committee yetu, Hon. Raila na kamati yake walipata baadaye. Haikuwa iende kwa mtu, halafu ipitie kwa deski ingine, halafu itawekwa chini ya desk, ilikuja direct. Wangapi walinunua gazeti ya Constitution. Sasa kuna watu wamesoma mbeleni hapa, mtatusaidia sana kwa sababu ni kitu kigumu, si kigumu kwa lugha lakini kwa fikira kwa sababu ni fikira ya nchi ya Kenya na pia ni fikira ya kitu ambacho tunaita kitu cha vizazi na vizazi.

Siku ya leo haitakuwa tena, ndiyo mnaona nimekasirika, mpaka miaka hamsini au pengine mia moja. Itakuwa na vitu vingine pengine referendum na nini lakini kurekebisha Katiba nzima, haitakuweko tena, kwa muda mrefu sana. Na ninafikiri hakuna mtu ataishi kuwa a hundred and fifty hapa, hata akiwa mtoto amezaliwa sasa, pengine hataona siku kama hii. Nataka mjue ile wanaita historic day, ile ambayo haitakuwa tena au ile ambayo watoto watakumbushwa na pia tutaikumbuka kwa kumbu kumbu, tafadhali muelewe hivyo.

Sasa tutakaa na tujue tuko kwa kitu serious, kitu kamili, ndio mkinipa excuses ya juu juu kuhusu hii na ile, hata haina maana kwa sababu ni kitu ambacho hauwezi kusema okay, next Sunday, we shall be here again, we cannot be. With me is Vincent hapa nataka aji-introduce, Programme Officer.

**Vincent Watako**: Mrembe mwesi?
**Audience**: Mrembe.

**Vincent Watako**: Vananga Vincent Watako.

**Com. Adagala**: Nyai Muhonga, na kuna hapa Patricia Mwangi.

**Patricia Mwangi**: Habari zenu, mimi ninaitwa Patricia Mwangi, mirembe vosi?
**Audience**: Mrembe.

**Patricia Mwangi**: Mrembe gandi?

**Audience:** Mrembe.

**Com. Adagala**: Yeye alikuwa anakuja hata zamani in the 60s na rafiki yake hapa kwa Kevei hapa kwa Sabwa. Sasa huyu ndiye ako in-charge of Verbatim Recording. Kila kitu tunasema hapa, anaandika word for word, okay. Yeye pia ndiye anasimamia idara hiyo, that department in our Commission, na alikuwa anafanya kwa Hansard huko Parliament. Vincent ni muyai Muwanga, kwao ni hapa tu, na yeye ni wakili chipukizi. Tutaendelea, kazi iko hapa nyingi, ndio sasa hata ni vibaya tumeanza ikichelewa hivi na kuna vitu vingine nitaeleza tukifika kati, watu wakiweko wengi.

Nataka tuanze na contents, halafu it will be like a break, we shall talk about process okay. Tukianza mapema ndio tunaanza na hiyo lakini nataka tuingie kwa Katiba yenyewe, District Co-ordinator ni sawa? Okay, hatutapoteza kitu lakini kama….okay, hiyo kwa table of contents, hawa wakina mama kuna mtu yeyote hapa anajua Kiingereza au Kiswahili? Chairman, you know what we are going to do, if these people are seating here and they all don't know what they are doing, wachanganyike kwa wengine ili wajue ile inafanywa.

Table of contents, I want us to first of all just look at the table of contents, hapo mwanzilisho, kifunuzi. Changanyika kwa wengine kwa sababu hautajua kile kinaendelea. Nakala ya Kiswahili bado hawajamaliza translation, okay? Committee members seat among these people, Werengai seat here, why do you keep him separate, not all of them. They need to seat to be helped, na kama una mtoto nyumbani amesoma mama, utampelekea akusomee unasikia?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Adagala:** Nitauliza, I will beg, I will plead with you to be quite because we are recording this. Msizungumze vile kama ni market, okay, ukiwa na kitu tutakuwa na nafasi tukimaliza mahali utakuja usimame hapa, au hapa vile inatakikana na utazungumza. Tutakuwa tunatoa proposals, pendekezo kwa sababu tunakagua sasa, hii kazi tunafanya ni ya kukagua kabisa muangalie. Wale wamesoma mbeleni watatusaidia pia na itakuwa kitu kizuri.

Ningependa sana wanafunzi wa shule wangekuwa hapa lakini sijui Chairman amefanya arrangements gani, ukiniambia nimewaambia, hiyo haitoshi, wako? Watoto wa shule wa Form four, ningependa wawe hapa. Chairman your work is mobilization, don't answer a stupid question.

Tunaanza na Preamble, if you are seating with these women you have to show them, huyu pia hajui vile anafanya, please get some people to seat here so that they can show them. Wewe nenda ukakae pale, yes. Ni muhimu sana mfanye bidii Katiba iwe translated kwa ki-Kabras, mnaelewa. Si muna bibilia ya Ki-Kabras?

**Audience:** Hapana.

**Com. Adagala:** Eh imeenda wapi? Mtengeneze yenu. Haya, kama hamna bibilia ya ki-Kabras mtatengeneza pamoja na Katiba na ni jukumu lenu, si jukumu la mtu mwingine. Okay, kuna Preamble. Preamble ni utangulizi, just say on the first page only, can you get someone between these two women, get this one to seat somewhere else so that they know.

Utangulizi mlituambia lazima tuwe na utangulizi, mlisema hivyo? Nasema hivi kwa sababu hakuna mtu anafaa kuwachwa nyuma, hata mtoto wa miaka tano anafaa kujua, mwishowe tutaweka Katiba kwa curriculum ndio kila mtu akae kama anajua Katiba. Only table of contents, don't open anywhere else. We have Preamble, hiyo ni utangulizi mlituambia tuweke, okay. Hii ni kweli?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Adagala:** Ninauliza kwa sababu tumeambiwa tumeenda ng'ambo tukatoa Katiba ya ng'ambo. Mlituambia iwe na utangulizi?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Adagala**: Okay, tutazungumzia hiyo. Hiyo sura ya kwanza hapo, table of contents, usifunue funue hapo tu, there are 20 Chapters, sura ishirini na ninataka tupitie juu halafu tuingie ndani. Hapo inasema ukuu wa watu na ukuu wa Katiba. Duniani hapa Kenya sasa, kuna vitu viwili tu ambavyo viko muhimu, wananchi na Katiba, mwisho wa mambo, okay.

Kwa Katiba hii ambayo tumependekeza, ile inafuata ni Jamhuri, Jamhuri ya Kenya ni nini? Iko wapi, inakaa vipi, okay? Haya hii ingine inafuata ni nia ya Kenya, lengo la Kenya ya kitaifa ni nini? Ni nini, tunakaa hapa kwa nini? Hii moja nikiguzia kidogo, ikiwa mtu amefanya maendeleo amejenga shule au amejenga kitu, alikuwa mpaka sasa anafanya kwa moyo wake mzuri, au pengine mlimulazimisha au iwe pengine alitaka kura. Lakini sasa iko kwa Katiba, hiyo ndio hiyo sura, tutazungumzia. Halafu sana tukishazungumzia haya mambo yote, itakuwa Mkenya ni nani? Mkenya ni mtu gani? Nani anastahili kuwa raia wa Kenya? okay.

Inafuatiwa na Bill of rights, kwa Kiswahili, translation hii inaitwa ukatiba, kuishi ki-Katiba na hiyo mambo yote iko hapo. Ya elimu, ya afya, ya haki za binadamu, haki za kupiga kura, hizo haki zote ziko hapo na ni sura kubwa sana kwa Katiba. Halafu kuwakilisha kwa wananchi, iko hapo tutazungumzia. Halafu sura ya saba, ni Bunge, iko vipi na Bunge itakaa vipi na kuundwa vipi na Bunge ya siku za usoni itakuwa vipi? Vile tumependekeza.

Halafu Bunge tumesema hapo, halafu sura ya 8 ni Executive, Urais, mumesikia ikizungumziwa sana hiyo urais, urais sivyo?

**Audience**: Yeah.

**Com. Adagala:** Halafu, Mahakama. Hii ndio Chapter walisema ni kama unachukua spounch kwa maji, halafu unafanya hivi na sponge halafu inakunywa maji. Walisema sponge hiyo, itolewe tusiizungumzie. Hapa polisi wakitaka wanaweza kutushika sote, mnajua, kwa sababu mahakama imesema 30 million Kenyans should not talk about this Chapter. Tukifika mtaniambia kama tutazungumza au la. Haya kwa sababu wamesema wamepiga marufuku Kenya yote, ni kama Kenya nzima ni jela, kwa sababu tunazungumzia hii na wametushona midomo, wanasema tusiizungumzie.

Hiyo ya kumi ni muhimu sana, inaitwa devolution of power. Kusambaza nguvu, devolution of powers, to spread the power na Act yetu ilisema, break the power, look at devolution and see where the power can go and I will tell you why we will have to spread the power when we get to it, because the power has been put in one place so it needs be to spread out. Hiyo ilikuwa Chapter ngumu sana kwa sisi na hiyo inayofuata ni ardhi na mali, sote si tunaishi kwa ardhi?

**Audience:** Mmh.

**Com. Adagala:** Plot, plot hapa. Na wale ambao hawana, hawana makao siyo?

**Audience**: Ndiyo

**Com. Adagala:** Hiyo ndiyo inazungumzia hivo. Halafu mazingara, hii mambo ya misitu ya Malava, si munayo?

**Audidence**: Mmh.

**Com. Adagala:** Na mazingara ingine iko hapa. Ile inayofuata ni fedha za umma na vile zinafaa zikae. Nafikiri mnajua zimeenda kombo kombo sana, utumishi kwa umma inafaa, hiyo pia imeenda kombo kombo sana ndio sababu pia tunarekebisha Katiba. Halafu ulinzi wa nchi, halafu kuna uongozi na ustahili, vile inavyofaa kukaa. Halafu tumetengeneza pia Tume zingine ambazo zitasaidia kutekeleza ukatibu au kuishi ki-Katiba ni kitu cha maana sana. Sasa hapa hizo zitatekelezwa, na walimu wanafaa kuwa wengi hapa kwa sababu mmoja wapo tuliyotengeneza ni Salaries and Emoluments. Hata ukisoma hizo haraka haraka, utaziona hapo.

Ukirekebisha Katiba kwa kupitia kwa Bunge na kwa referendeum na kuna sehemu ambazo hazitaguzwa na zingine ambazo zitabadilishwa. Inayofuata ni kufafanua Katiba zaidi. Halafu kuna kitu muhimu sana ambacho mnastahili kujua ili tusimangemange sana kwa mazungumzo yetu, kuna kitu inafaa tujenge daraja, daraja kati ya Katiba iliyoko sasa na ile iliyopendekezwa ili tusitatize wananchi sana na kutetemesha nchi yetu sana na kutoweka watu kwa hali ya wasiwasi mwingi sana. Hizo zipo hapo na tutakuwa tukiizungumzia tukiendelea.

Moja niwaambie tu ni kama ile ya Provincial Administration, we didn’t abolish the Provincial Administration because the Provincial Administration is not in the present Constitution. You cannot abolish what there isn’t, you cannot abolish what doesn ’t exist. So what we said is there, so let them report to their employer and huyo employer atafikiria na aone vipi watakua

deployed lakini kweli watu wanatulaumu hata Chief wa kwetu, mmetutoa, hatujatoa wala kufuta mtu kazi, wataenda kwa employer. We had to be kind, we had to think, you cannot just throw people in a dust bin, that is why we have this transitional thing, it has the Presidency, what MPs will do, we will talk about it as we go on.

Nimepitia kwa hii ili tuende pamoja, mjue nini iko mbele yenu tunapozungumza, sitaki mkae hapa ignorant, hiyo siyo njia ya ki-Katiba, hiyo ni njia ya kiimla, mtu anajua vitu na anakuficha, wewe unafuata tu bila kujua. Sasa huo ndio mpango wa Katiba.

Katiba hupangwa hivi, na mlisikia kama kulikuwa na Draft Constitution na watu wengi wa Kenya ni werevu sana, wengi waliandika Katiba zao full, kutoka Preamble mpaka mwisho and we have dozens and dozens of them in our documentation center. NGO's waliandika, watu binafsi wakaandika, wengine waka-publish, sasa Katiba ni nyingi na mtu yeyote anaweza, huyu kijana mkiketi naye, mtasema hatutaki hii, keti, tunataka uandike Katiba, yeye ni wakili ataandika. Na mimi ni public affairs, mkisema tu watu wa Kabras hatupendi tuanze mwanzo, tutaandika na iendelee, mnajua hivyo?

**Audience**: Ndiyo

**Com. Adagala:** Na tena mjitayarishe kwa sababu kuna kitu kinaitwa District Council inakuja, na kwa district mnaweza kuunda Katiba yenu. Katiba ya District eh, mnaelewa?
**Audience**: Ndiyo

**Com. Adagala:** Katiba ya District ambayo mtakaa nayo na haitagongana na hii lakini kuna vitu kwa District ambavyo mnaweza kupanga. Kenya ijayo ni Kenya wazi, Kenya huru na ni Kenya ambayo ukiwa na fikira utasema wala hakuna mtu atakukataza isipokuwa usitusi mwingine, mnasikia, wala msidhulumu mwingine. Basi tuendelee, kuna Preamble hapa.

Preamble ni utangulizi, haiko ndani iko hapo kwenye hiyo page. Hold your newspaper mama hivi, kwa sababu utachoka na hata utaweza kukunja ili iwe quarter ili tuendelee vizuri okay. Preamble ni utangulizi, tuliambiwa hakuna Preamble kwa Katiba yetu, wengine wakaandika ni nini itakuwa kwenye Preamble. Na tulisoma na kusikiliza pia na tukasikiliza ingine ambayo watu walisema, watu wanasema nini, ni nini watu wanalalamikia kuhusu mambo ya Kenya na tukasema kuna vitu fulani wananchi wanataka. Pengine tulikuwa tunasikia kwa *vavola vulogori mmsedi* mnasema hivyo pia huku. Unasikia tu halafu unajulia kwa spelling, okay ndio hii. Sasa tuna preamble, kitu kikubwa Kenya ni kitu kinaitwa wananchi. Sasa inasema, the people of Kenya. Sisi wananchi wa Kenya, Katiba yetu ya sasa haina hiyo, inaanza tu, Kenya is a sovereign Republic.

Na kweli Mwingereza hakuwa na haja na watu wa Kenya, kwanza alikuwa amekasirika tumekataa utumwa, tumepigania, akasema aah wacha wanataka nchi basi, Kenya is a Republic haya endelea. Hiyo Katiba ilikuwa ya kupea nguvu ya kujitawala na pia, Waingereza walikuwa na copy kama hii kwa shelve. Ghana wakipata independence, wanatoa wanasema Ghana is a

sovereign Republic, halafu wanaweka hapo vitu vya Ghana kidogo kidogo, juu juu. Tanganyika pia ilitaka wakatoa, Uganda ilitaka wakatoa wakafanya Uganda to be a sovereign, ilikuwa kama model, walikuwa wanatoa wakiweka. Basi ikafika Kenya, wakafanya hivyo tena lakini sasa inaonekana wananchi wa Kenya hawakuwa na cha kusema. Hatukuwa watu na hicho ni kitu kibaya sana ndio unaona tunarekebisha Katiba, nani anatengeneza Katiba, Katiba ni ya watu. Ukiwa Mkristo bibilia ni yako sivyo?

**Audience**: Ndiyo

**Com. Adagala:** Na wewe ni wa bibilia na Mungu, hiyo ndio inakaa. Hauwezi kusema wewe ni Mkristo kama haujui bibilia, inawezekana? Muislamu unaweza kuwa bila kujua Quran? Hatulinganishi neno la Mungu na hii lakini hii ndio inatufanya tuwe wa Kenya, unaweza kuwa Mkabras bila kujua mila ya wa Kabras?

**Audience**: Hapana.

**Com. Adagala:** Si mnaona mnalalamika watoto wanazaliwa Nairobi wajukuu hawajui, mtafanya bidii muwafundishe, kwa sababu hawawezi kusema Kabras, siyo damu pekee pia ni lugha, mila na mila ni sheria na mila pia ni mtindo wa kufanya vitu, tabia na hizo zote. Sasa hapo ndio tunasema, we the people of Kenya, wengine tulitaka isemekane, we the peoples of Kenya or we the people and the peoples of Kenya.

Sasa inasema tunajua na tunakubali tuko kabila nyingi, watu wa aina nyingi, tuko watu wazima, walemavu, watoto, wakongwe, walio soma na hawakusoma na dini tofauti tofauti, diversity. Na hiyo ndio tulipokuwa tunafanya hearings tulikuwa tukitafuta hiyo diversity. Nafikiri kuna division ingine hapa juu, zaidi hapa ni wa Kabras sivyo, lakini hapo juu nafikiri kuna wa Bukusu kidogo, Watachoni, na ?

**Audience:** wa kabras (inaudible)

**Com. Adagala:** Kule juu, upande ule. Hao wana hiyo diversity, inaitwaje hiyo division?

**Audience:** hayani

**Com. Adagala:** But it is there, so it is mchanganyiko, wao watu sasa wanaishi na diversity. Kuna sehemu zingine kama hizi za Kabras, sivyo. Sasa mnaishi hivyo lakini kule wanaishi ile ya kabila, unajuwa kuna wanawake na wanaume, kuna nini, sasa hiyo yote tuna accept, tumekubali. Tuko hivyo na tunaishi hivyo, okay.

**Interjection:** Inaudible

**Com. Adagala:** Haya hiyo ya pili inayofuata, mimi ni mgeni hapa ukitaka kunifundisha, sina shida. Sasa katika utangulizi wa pili, kitu muhimu sana msikize, tunafikiria maslahi ya mtu binafsi, ya familia na ya jamii. Hiyo iko hapo, mlituambia familia ni kitu muhimu sivyo?

**Audience:** Yes.

**Com. Adagala:** Iko hapo, okay. Sasa hapo tunahifadhi uhuru, siku hizi kuna uhuru nyingi, kuna Uhuru Park, kuna uhuru ingine, lakini hii ni ya uhuru wa kibinadamu, demokrasia ya ukweli na utawala wa sheria, just that, okay. Hiyo ndio tunaona inahifadhiwa kwa Katiba, endelea.

Kuna kitu kingine kinaitwa inalienable hiyo. Inalienable, haiwezi kutolewa kwa wewe, mtu akitoa kitovu chako, utakufa. Hiki ni kitu cha kitovu ambacho mtu hawezi kukukataza, kuna haki hiyo ambayo haiwezi kutolewa ya kuunda serikali bora, utawala bora na pia tumeshiriki kwa kutengeneza Katiba, nyinyi ndio mlitengeneza Katiba. Sisi tuliandika yale mlisema, muelewe hicho kitu -all mobiles off please.

Mkiwa hivyo inakuwa kitu, msiseme Commission ndio ilitengeneza Katiba, msingelituambia hayo mambo ya process, hatungelikuwa na la kuandika. Tulienda nyumbani na vitabu vyetu na kurudi headquarters na vitabu vyetu na hakuna hata kitu kimoja tuliandika. Kwanza mimi nilikuwa kwenye kamati iliyoandika Preamble. Hii Preamble ilichukuwa many writings, tunaandika tunafuta na kurudia, kwa sababu inatoka kama shahiri, hiyo ndio inafaa iwe na vitu vyote ndani yake. Katiba hii yote iko kwenye Preamble, hizo nambari na clauses.

Sasa inasema, tunapitisha na kuchukua na kujipea wenyewe, ni kama zawadi, tunajipa wenyewe hii Katiba na pia kwa vizazi vijavyo. Na hapo mwisho inasema, God Bless Kenya. Watu walituambia hakuna Mungu kwa Katiba yetu ndio unaona tunayumba yumba huku na kule, ndio unaona kuna corruption nyingi. Hasa wazee walikuwa wanasema, weka Mungu hapo hawakusema vipi. Sasa tukafikiria, mimi nilitaka ianze hapo juu na wimbo wa taifa, Oo God of all creation, believing or trusting in God of all creation, halafu tukazungumzia mtu mwingine akaweka hapo katikati, supremacy of God, tukaandika tena tukasema basi, wacha tuweke hii, God Bless Kenya. Tulifanya vibaya?

**Audience:** Hapana.

**Com. Adagala:** Tuko kwa nyumba ya Mungu nafikiri hata yeye amefurahi. God bless Kenya. Na hiyo iko kwa Katiba nyingi, modern Katiba, ya kwanza ilikuwa modern Katiba ya kuandikwa ya America na hapo hapo wana Mungu okay. One nation under God, sasa hauwezi kuenda na kutawanyisha hiyo America sababu wameapa, one Nation, indivisible under God okay.

Watu wa South Africa, wao wana yao pia wameweka inasema, *Nkosii sikelele South Africa*, okay, si munajua hiyo nyimbo

pia?

**Audience:** Mmh.

**Com. Adagala:** *Nsisi sikelele Africa*, hiyo wamesema *Nkosisi kaledi South Africa*. Hiyo ndio mlituambia mnataka Kenya ikae hivi, iwe nchi moja, watu wote wawe na usawa, familia iweko, demokrasia, hivyo vitu vyote viko hapo. Sasa sura hii nyingine itakuwa inafafanua mambo mengine okay. Tutakuwa tukienda sura kwa sura kama kuna comment hapa, njoo mbele utoe hiyo comment lakini hasa tunataka pendekezo kwa sababu tunakagua. Kuna mtu ambaye ana jambo la kusema? Kile unafikiria, unaweza kufikiri si kitu lakini ndio kitu kinachoweza kufanya hii Katiba iwe nzuri sana, kile unachohisia kwenye moyo wako, ndio inawezekana. Usikae bali una uhuru wa kuzungumza na mbele ya Katiba hakuna uoga, okay? Usikae na uoga ukijifikiria halafu nyumbani useme nilikuwa ninataka kusema, la, hiyo haipo okay. Tuendelee, tuendelee?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Adagala**: Kuna mtu ambaye ana la kusema?

**Audience**: Tuendelee.

**Com. Adagala:** Nasikia wakizungumza huko nyuma, njoo mbele useme.

**Audience:** …….(inaudible)

**Com. Adagala:** Okay**,** kweli mara nyingi kwa sehemu hii kwa sababu imekaa na vitu vingi ndani, saa zingine watu hawana la kusema zaidi halafu tutaendelea. Sura ya kwanza, nimemuambia kuna kitu kinaitwa, wananchi wa Kenya na ni nani?

**Audience**: Ni sisi.

**Com. Adagala:** Nataka mjue hivyo. Hakuna mtu mwingine, hakuna mtu kutoka nje au hakuna mtu aliye juu yenu. Kuna Katiba na kuna wananchi, mtu yeyote ambaye ako Kenya, akitaka kufanya kitu, anafaa kuuliza wananchi, okay. Sasa hiyo ndio ukuu wa Katiba na ukuu wa wananchi.

Nguvu zote, ukuu wote ndani ya Kenya wa wananchi. Hizi nguvu zitapeanwa kwa wakilishi wao kwa njia ya ki-democracia, zitawakilishwa kwa njia ya demokrasia. Hizo nguvu zote zimepeanwa kwa mikono mitatu ya serikali. Bunge, si munapiga kura ya Bunge?

**Audience:** Mmh.

**Com. Adagala:** Lakini wanaenda kule halafu wanakuwa wakubwa kuwaliko. Muwaangalie sana, sasa hawatakuwa hivyo tena, hao ni watumishi wala sio wakubwa. Bunge, Urais na Mahakama, mapacha watatu ambao ni serikali, okay. Na hapo pengine ni pa kufafanua tu.

Ukuu wa Katiba, watu wanatengeneza Katiba halafu Katiba ni kitu cha kukubaliana na ndipo tunakubaliana kuishi hivi halafu hiyo Katiba inawalinda na wao wanalinda Katiba. Mkipata hii Katiba, msifikiri mtu mwingine atailinda bali ni nyinyi mtakayoilinda, msifikirie mtu mwingine ikiharibika ila ni sisi wenyewe ndio tutailinda na kuirekebisha.

Sasa hii ni ukuu wa Katiba ambao umetoka kwa wananchai wala sio kwingine. Kwa Katiba kuna utawala wa sheria, Kenya itatawaliwa na sheria, hiyo ni kusema hatutakuwa na imla, dictatorship. Kitu cha kwanza Amin alifanya na Constitution ambayo ilitengenezwa na Obote ni kuteketeza kwa moto, ndipo unaona imla inaingia. Imla sio ya kijeshi peke yake, lazima tutafuata Katiba.

Watu wote wameshikwa na kuunganishwa kwa hii na ni lazima waifuate. Kutekelezwa, hatutakuwa na watu wa kupinga pinga, hiyo njia ya kutekelezwa itasimama imara daima. Kukiwa na sheria nyingine yeyote, ile niliwaambia ya kwamba mnaweza kutengeneza Katiba yenu ya District au ya wa Kabras, lakini ikiwa na sheria ndani ya sheria ya Kabras au ndani ya sheria nyingine au sheria nyingine yeyote iliyoko, ikigongana na Katiba, hiyo sheria itawekwa kando. Katiba ndio inasimamia.

Itatekelezwa ili iwe na utawala bora. Haki za binaadamu, na mambo ya maendeleo ita-promote. Kuna vitu vigumu vigumu kama Katiba hii yetu ya sasa, ukianza kusoma unaangalia unasoma sura mbili halafu unaacha. Na mawakili lazima waisome kwa darasa, lakini hata Prof. Ghai amesema hii Katiba haisomeki kwa sababu iko ngumu sana. Na pia kwa kutekeleza, ina vitu vigumu vigumu. Lakini katika Katiba hii ambayo wananchi wanapendekeza tunasema isiwe na vitu vyenye vikwazo ambavyo vitafanya iwe ngumu kutekelezwa, iwe rahisi, accessible na direct.

Kazi ya kuhakikisha Katiba itasimama imara ni ya watu wa mahakama, wao ndio wanafaa wasimamie. Sasa unaona ile shida tumeingia kwa sababu watu wa Mahakama hawataki Katiba iendelee na ni kitu wananchi wamesema ilhali judges wanasema hawataki iendelee, si mnaona hapo kuna shida? Wao ndio wanafaa kuilinda na wanataka itupwe mbali. Ni kama kuzaa mtoto na kutupa kwa pipa, kitu kama hicho.

Ikiwa mtu atajaribu kutengeneza serikali ambayo sio ya ki-Katiba, haitakubaliwa. Hatuwezi kufanya vitu ambavyo vitaharibu au kupunguza ukuu wa Katiba. Kitu kama hicho kimetupiliwa mbali. Huyu kijana ananisaidia kwa sababu macho yangu ni mabaya na yamepasuliwa lakini hayajapona, so ananisaidia lakini tutaendelea tu hivyo. Kuna sheria ya Kenya, msikilize vizuri sana na hapa ikipitishwa vile iko, ndio itakaa na hauwezi kusema baadaye lakini hii ndio sheria ya Kenya hapa. Hiyo sheria inatengenezwa na Bunge, mila za Kiafrika na sheria za asili ya kiafrika, mila ya Waislamu, wa Hindu. Kuna ingine inaitwa common law, halafu hiyo ya East Africa, tuko kati ya East Africa si mnajua hivyo?
**Audience:** Ndiyo

**Com. Adagala:** Mnajua hata Hon. Shamalla wa Kenya yuko huko? Halafu hiyo ya kimataifa ambayo imekuwa kama mila ya

kitaifa inayotoka kwa treaty na convention na vitu kama hivyo. Pia hiyo lazima tuiheshimu kwa sababu tunaishi kama nchi inaishi na taifa zingine, okay.

Hapo kuna miaka miwili ambayo Parliament itapewa, Bunge ambalo litakuweko uchaguzi ukifanywa, kuweka hizo zote pamoja ili zisigongane wala kutafautiana, ili ziwe-harmonized okay. Now, kuna schedule mkiangalia kwa table of contents after transitional government, kuna schedule. Hiyo schedule ndio details kulingana na vile kila section itaendelea, watu watakuwa wanauliza, kwa nini hii, kuna vitu vingi sana vitakuweko ambavyo Bunge ndio itaweka kwa sheria. Sasa hiyo yote iko kwa schedule, si kitu cha kuzungumzia au kuangalilia hapa, sasa usifunue huko, ukienda huko itakuwa ngumu. Ni kitu cha kuketi mahali na kusoma au kusomewa ya sasa ni schedule 6. Schedule 6 ndio inafanya kazi ya Parliament vile itafanya na kulinganisha hizo sheria zote, okay.

Ningependa hapa kwa sababu sitaki kuwa one-way, nataka pia nyinyi mzungumze. Kwa mambo hapa kuna pendekezo ambayo mnaona tumewacha nje. Kabla hatujasema hivyo, Katiba inatoa nia na lengo, inatoa principle. Parliament ndio itafanya sheria yenyewe iko, iwe kwa Parliamentary Act. Kuna watu ambao wangependa kusema kitu hapa? Njoo mbele mpange hapa laini na usingoje mwingine azungumze ndio unasimama, usimame sasa.

**Cllr. Luka**: Yangu ambayo ninataka kusema hapa ni kwamba ni Constitution supreme, lakini mtu akishapewa mamlaka, sasa amekuwa kama Rais, anachukuwa hiyo Constitution inakuwa ni yake na kwa hiyo Chapter sijaona mkizungumzia mtu kama huyo anafanywa nini?

**Com. Adagala**: Ako chini ya Katiba. Mwingine? Rais ako chini ya Katiba. Njoo, ukitaka kuzungumza njoo mbele, sioni vizuri. Okay Councillor, wacha nifafanue hapa kidogo kwa sababu hiyo ni, it is okay you need to write. Ukampa mfanyikazi wako kazi, umuambie lima kutoka hapa mpaka pale, sasa yeye ako juu yako?
**Audience**: Hapana

**Com. Adagala**: Rais, Councillor, MP wako chini ya Katiba na chini ya wananchi. Tumekuwa na Katiba ambayo ilikuwa ya power. Hii ni ya service, okay? Hii ni ya utumishi, tofauti kubwa sana muelewe kwa sababu kuna vitu vinaingia na ni vizuri Councillor ameuliza hiyo. Vitu vinaingia hapa kwa sababu hakuna mtu ako mkubwa kuliko mwingine Kenya na hakuna mtu ana nguvu kuliko nguvu za wananchi okay. Councillor tutazungumzia hiyo tukifika kwa hiyo sehemu ya Urais na vitu vingine na representation of the people, okay.

Nguvu zote za Kenya zinatokana na wananchi, hazitoki mahali kwingine. Hizi za dunia hii, okay? Mtu mwingine ana cha kusema? Kuna wazee wa kanisa hapa, church leaders? Look at the laws of Kenya, there where we have set the Constitution, Katiba. Kijana soma pengine hawasikii.

**Vincent:** Katiba kifungu cha tano kuna sheria za Kenya, na sheria hizi zimeorodheshwa ya kwanza ni Katiba, sheria za Bunge, sheria za utamaduni za kiafrika, sheria za Waislamu na wahindi, sheria common law, sheria za Africa Mashariki na sheria za kimataifa. Natumai mumesikia.

**Com. Adagala**: Wazee wa kanisa mumesikia? Mumekubali? Njoo mbele. Mtu yeyote anayetaka kuzungumza apange hapa laini. Mama fuata.

**Pastor Kisa:** Jina langu ni Christopher Kisa Pastor wa friends Quaker. (Inaudible). Chini ya sheria nimeona mumetambua Islamic na Hindu

**Com. Adagala:** Kabla haujaendelea, sisi Commission hatukutambua Islamic na Hindu. Walijitambua na hata kwa Katiba iliyoko sasa, walijitambua. Yetu ni kuandika wala si kutambua, walijitambua, wakaandika, wakaleta.

**Pator Kisa**: Asante kwa kuniambia, nilifikiria labda nyinyi wa Commission ndio mliwatambua. Ikiwa namna hiyo sisi wa Kristo hatukujitambua? Ingekuwa vizuri tungekuwa na sheria ya Ki- kristo.

**Com. Adagala:** Unajua mzee, wewe ni mzee wa kanisa, uniambie ni nini itakuwa kwa hiyo sheria ya ki-kristo. Usiketi.

**Pastor Kisa**: Kwa maana ninasema sheria ya Ki-kristo, kuna sheria ya utamaduni na kwa Ki-kristo kuna pahali ambapo tunasema hatuwezi kufanya hii, na utamaduni unasema tufanye hivi. Ingekuwa vizuri ….

**Com. Adagala**: Usizungumze mambo ya utamaduni, hiyo iko hapa, wewe sema ya Ki-kristo.

**Pastor Kisa**: Okay, basi ikiwa namna hiyo, sina jambo hapo sana.

**Com. Adagala**: Mzee mwingine wa kanisa? Hata kuna mama hapa wa kanisa?

**Audience**: Wako.

**Com. Adagala:** Njoo, nataka viongozi.

**Joshua S.M.:** Jina langu ni Joshua Solomon Mulati. Kuna sehemu hii ambayo ya the laws of Kenya ambapo vile tumeona ama vile imeandikiwa ni kwamba sheria ya Kenya zinatokana na Constitution, Act of Parliament, African and customary law, Islamic na Hindu personal law. Lakini hapa kuna wakenya wengi ambao …..

**Com. Adagala**: Tafadhali zungumza ukamilishe jambo ………..

**Joshua S.M.:** Asante, wa Kenya wengi haswa sana ni Wakristo ambao niko na hakika ya kwamba kama tungekuwa na hizi laws, lazima Wakristo pia wangekuwa wamechangia katika muundo wa sheria hizi. For example, katika Wakristo, kuna sheria ambazo ikiwa Waislamu walitoa zao, wa Hindu nao wakatoa zao, sijui ni kwa nini zetu nazo hazikuingia katika Commission hii?

**Com. Adagala**: Ninakuuliza kwa nini zenu hazikuingia?

**Joshua S.M.:** Basi inaonekana Commissioners, niko na wasi wasi ya kwamba, ikiwa wa Hindu na Waislamu waliingiza zao, inaonekana labda mambo yanarudi kwetu kwa sababu kwa nini hatukupeleka maoni yetu kwenu.

**Com. Adagala**: Ulikuwa hapa wakati wa hearing? Wazee gani walikuwa hapa wakati wa hearing, mlikaa nyumbani? If you want to talk unapanga laini kama haupangi laini hautazungumza, hapa. Mzee ukitaka kuzungumza panga laini, mimi nikikaa kwa kanisa lenu ninafuata sheria zenu, kwa Tume yangu mtafuata sheria zangu.

**Mameti Shaviya:** Jina langu ni Mameti Komo Shaviya. Yangu ni kwamba kwa kweli sisi hatukuingiza ya Wakristo na kwa sababu hapa ingefaa tuchangie kidogo, ingelikuwa vizuri tutaje Wakristo pia kwa mfano yaani Wakristo hata Friends church, ukienda kwa mahakama, haulazimishwi kuapa kwa kubeba bibilia. Ingelikuwa ni vizuri wataje hapo yaani kwamba Wakristo pia sheria yao isikike ili mambo haya yasikataliwe wakitaka.

**Com. Adagala**: Ninataka uniambie sheria ya Wakristo ni gani?
**Mameti Shaviya**: Nimesema kwamba hapo ni kutoapa mahakamani.
**Com. Adagala**: Okay, tutawacha hilo jambo kwa sababu wazee hawataki kufikiria, wakina mama wameketi kitako.

**Edward Makokha**: Asante. Mimi ninaitwa Edward Makokha. Nataka kutoa shukrani kwa sababu kwanza sisi jamhuri ya Kenya …
**Com. Adagala**: *Wa Kabras, kove ne sokoni hachova shimbii*? Ukitaka kuzungumza vile mnazungumza muende kwa soko, mbele ya Tume mtanyamaza. Mkizungumza hivyo, mambo ya huyu hayatasikika, hayatanaswa kwa mtambo. Tafadhali jikaze, hapa tunafanya recording tafadhali, heshima.

**Edward Makokha:** Nafikiri tutaenda. Kwa mkato. Kwa mfano vile tumeelezwa Waislamu wamewakilisha, wa Hindu wamewakilisha, sisi kama Wakristo najua tuko na tofauti tofauti. Kuna wa Katoliki, kuna wa Friends, kuna wa Seventh Day Adventist na kuna wengine pia wanachipuka chipuka. Na katika sheria za kidini, kuna kama sehemu ya ndoa, marriage ambayo katika hii marriage dini imehakikisha ya kwamba, watu watatenganishwa tu baada ya kupata mke kama amefanya uzinifu, lakini kwa jambo… hata kama mwanaume, akipatikana na uzinifu kwa upande wowote katika sheria ya kanisa, inasimamia ndoa.

Kwa hivyo ukija katika sheria kama hiyo unakuta hapo ndipo ki-kanisa ama kama wa Kristo wanakubali kulingana na mujibu wa bibilia ya kwamba pawe na utengano. Ndipo tena kunakuja sehemu nyingine ya kwamba sasa mke katika sheria ya ki-kristo, ni kwamba mume ndio kichwa cha nyumba na kila siku watakaa hivyo na kwa hivyo kama kutengana pia kumetokea kwa sheria ya ki-kristo, ni kwamba hapa mke anarudi kwao na hakuna ugawanyaji wa mali.

**Com. Adagala:** Na ni nani mkubwa wa mume?

**Edward Makokha**: Ni Mungu. Tukisema Mungu ni Kristo. Kwa hivyo sheria kama hiyo ya ndoa kwa sababu tunajua katika Waislamu, wanapotengana kuna kupeana talaka na mtu anakuwa na nafasi ya kuoleka mahali pengine. Sasa hiyo ni moja wapo.

**Com. Adagala**: Okay, nilitaka hivo ili mujue wa Kristo wa hapa mfikirie. Asante, you have helped me a lot. Nataka wa Kristo wa hapa, njoo uandike jina lako au you have not exhausted, a different one?

**Edward Makokha**: Yeah, jambo lingine ni kama tuko na wa Kristo ambao tumesema tumegawanyika, watoto wanapoenda shule kama Seventh Day Adventist, ni wa Kristo lakini watoto hao wanalazimishwa kuenda shuleni siku ya Jumamosi, je, hao nao wanapata haki katika hii Constitution namna gani?

**Com. Adagala:** Watu wanaitwa Seventh Day Adventist walijitetea nchi nzima, isipokuwa pengine North Eastern, walijitetea Jumamosi, Sabath day na iko hapa. Nchi nzima kila mahali tulienda mpaka mwisho tulijua watasema nini, walijitetea iko hapa. Ile nilitaka kusema, kuna personal law, hiyo ndio ya Waislamu iko hapa, lakini watu wa North Eastern na watu wa Coast, walisema wao wanataka kuishi na Sheria law, hiyo ya Qur'an yote, ukiiba unakatwa mkono, ukiiba tena unakatwa ingine, ukiiba tena unakatwa shingo. Na walisema hivyo wanaume kwa wanawake, lakini tuliwaambia kwa vile hatuko kwa Saudi Arabia au Libya, na sio Islamic Republic, hiyo personal law yao inafaa Muislamu kwa Muislamu. Lakini wacha niwaambie, wa Kristo tumekaa.

Na wao wanatuambia lakini hii sheria yote imetengenezwa kwa sheria ya wa Kristo na sio hivyo, hii ni ya dunia. Inaitwa secular okay, lakini sheria ya wa Kristo haipo. Kwa sababu wakubwa wa kanisa ndio wamelegea. Mtu akija, kama mimi nikitembelea halafu nitoe sadaka, leo sadaka ilikuwa juu sana huyu mama Commissioner alikuja, tumuambie awaambie wengine waje, sasa ninakuja na sadaka takatifu, tunakuja na marafiki wangu kumi, tunatoa, weka ceiling hapa lakini hakuna mtu anauliza hizo pesa zilitoka wapi? Pengine mtu ameuwa mwingine, ametoa pesa, *yasa kwerombera muno* hamjui, hamuulizi. Pengine mtu amefanya ufisadi zinakuja zinaiingia.

Wa-kristo imekuwa kwenda kanisa na kwenda nyumbani halafu unaenda kwa usharati halafu unaenda kwa uizi, unaenda kwa udangayifu, hakuna mtu anafuata Mkristo anamuambia unaishi vipi? Hii ya Waislamu unaishi vipi, hata wa Pastor wenyewe hafuati. Hiyo ni moja, ya pili, kuna hiyo ya Musa 10, halafu ya Deutronomy na nini halafu Yesu akaja halafu Paul akasema, it is a time of break. Waislamu wakiangalia wakasema, unajua Issa bin Maryam, ndio wanaita Yesu, alimuambia hakuna sheria tena, sasa nyinyi hamna sheria, sisi tunayo. Lakini inafaa wa Kristo waangalie principles za kuishi na inafaa muangalie hapa vile mtakaa kama wa Kristo kwa sababu itakuwa na sheria na mkikosa kuwa na hiyo ya kuongoza mambo, what can guide Christian life kama haiko hapa imewachwa nje? Mfikirie hata hapa wenyewe mnaweza kuandika na mpee District Co-ordinator, Chairman au wale watu ambao watamuwakilisha kwa National Constitutional Conference. Na mufanye haraka kwa sababu bado tunajadiliana lakini itakapopitishwa, hamwezi kuja nyuma na kusema, lakini itakuwaje na hivi na vile. My

advice, that it looks like something that should be in a Commission.

Wananchi walipeana kama kutupa tupa lakini haikuwa kitu na tunataka wa Kristo wenyewe watengeneze, hii ndio our personal law. Waislamu walitaka hata ya biashara yao ifuatiwe vile wanaendesha biashara yao. If you are lent money, there is no interest in their bank. I am dwelling on these kwa sababu ninataka wa Kristo wafikirie okay, haya mzee endelea.

**Opanda Wamalika:** Asante kwa kunipatia nafasi hii. Mimi ninaitwa Opanda Wamalika na ni wa Seventh Day Adventist. Nina mambo mawili ambayo ……..

**Com. Adagala**: Mambo ya Seventh Day Adventist ya Sabato iko hapa, imeshaingia. Hiyo ya kudhulumiwa katika shule au kazini iko hapa kwa sababu walichangia pengi sana. Una lengine la kuongeza juu ya hiyo, iwe tofauti kabisa. Tutakosana ikikosa kuwa tofauti.

**Opanda Wamalika:** Yangu ni tofauti si Sabato. Jambo la kwanza ni kwamba, tukiangalia katika hii draft, mwanzo wanazungumzia juu ya sources of law. Yaani pendekezo langu ni kwamba mahali penye pameandikwa sources of law, tuwe pia na religion ama vitabu ambavyo vinaongoza dini. Kwa sababu tumepata kama kuna customary law, Constitution, Parliament na mambo kama hayo. Sababu yenye inanifanya niseme hivyo ni kwamba, ikiwa Mkristo ataweza kutofautiana na mtu asiye Mkristo kwa mambo ya mila, halafu aje mbele ya koti, utaona ya kwamba katika Katiba wameandika customary law na hawajaandika religious law, mkristo ataweza kuwa aggrieved, wataweza kukata kesi in favour ya mtu ambaye ….

Jambo la pili na la mwisho ni kwamba sisi wa Kristo tunaamini katika mafundisho ya bibilia na katika Constitution imezungumzia juu ya usawa kati ya bibi na bwana. Ukiangalia katika bibilia, inazungumzia juu ya nafasi ya bibi katika ndoa na nafasi ya bwana katika ndoa. Sasa utapata ya kwamba, tunapofuata bibilia na tunapoangalia hii draft Katiba, kuna hitilafu kwa hivyo ninaonelea ya kwamba, turuhisiwe kufuata vile bibilia inavyozungumzia kuhusu nafasi ya bibi na bwana katika ndoa, Asante.

**Com. Adagala:** Lakini huyo bwana awe mkristo ambaye amesimamiwa na Kristo. Munawacha wanawake wanaishi na mashetani kwa nyumba halafu munasema mwanaume ndio mkubwa. Tena kwa bibilia, tumesomewa bibilia na watu wengi, sijui kwa nini wanataka kutumia bibilia kudhulumu wanawake lakini dini ninakumbuka inasema, there is no Gentile, there is now Jew, there is no woman, there is no man. Mchukuwe bibilia yote, mchukuwe ile sehemu zina …….. Haya nilitaka kusema hiyo mchangamke mjue mkiketi hapa tunakagua na lazima mkague. Wazee wa sehemu hii, mketi pamoja even this Sunday, whatever it is, mzungumzie muangalie hiyo section ya Chief Kadhi, Waislamu wana Chief Kadhi ambaye, he devices over Islamic affairs, personal law.

Muangalie, mlinganishe muone vipi ingekuwa okay, Okay? Haya, mmeona mambo ya kukagua, nataka kujua kama we are in the spirit now.

**Audience**: Yeah.

**Com. Adagala**: Yeah, okay. Kuna Jamhuri, sura ya pili ndiyo inazungumzia Jamhuri. Jamhuri ya Kenya ni nini? Kenya ni taifa ambalo linajisimamia, liko huru, na ambalo halisimamiwi na mtu mwingine ambaye taifa lingine liko juu yake. Mnakumbuka wakati wa ukoloni wazee na wakina mama wazee, tulikuwa tunasimamiwa na Muingereza na tukapigania vita na hata Katiba ya sasa inasema, Kenya is a sovereign Republic. Mnaona saa zingine, Rais au Minister wa Foreign Affairs anagongana na watu wa nje, Diplomats, ni kuhusu hiyo. Kwa sababu wanataka wakikuletea 1 million Dollars, wanataka sasa pia watawale, mnasikia? Na tunasema la, hata tukiwa masikini, bado tuko, okay?

Msingi wa Jamhuri ni serikali bora, utawala nzuri. Multi-party hiyo tulipigania vyama vingi vya siasa na demokrasia siyo imla ya hiyo vyama au kwa hivyo vyama, kila kitu wazi bila kuficha ficha chini ya … na pia wajibu okay. Kuna hiyo ya kutenganishwa matawi matatu ya serikali ya Bunge, ya Urais na ya Mahakama. Hiyo ni separation of powers, na sio huko juu peke yake. Inakuja mpaka chini mpka kwa likuru. Isiwe likuru au Chief ndiye anatawala, pia ndiye anachukua kesi, anahukuma na kutengeneza sheria.

Watu wasikia separation of powers wanafikiria ni huko kwa Bunge na wapi lakini iwe hivyo pia hapa. Iwe tofauti, haki za binaadamu na utawala wa sheria. Yaani hatuwezi kufanya kitu kiholela holela kwa sababu tukifanya tu vile tunataka, ni kama hii kelele tunafanya hapa, haina msimamo. Lakini tukikaa na tuna sheria ya kupitisha kwa kila kitu, lazima sheria iweko ili watu wasidhulumu wengine.

Kuna territory, eneo la Kenya ni eneo la aina gani. Watu ambao wanaishi kwa mipaka, kama wa Turkana walituambia hata haijulikani vizuri mipaka ya Kenya iko wapi. Halafu wakasema sisi ni sengenge ya Kenya, sisi ndio tunalinda mpaka na kwa sababu hao ndio seng'enge ya Kenya, walitaka wapatiwe vitu kulinda mipaka. Eneo la Kenya linapitia wapi? Longitude, latitude, geographers wako hapa. Longitude, Latitude iko wapi? Hapa Busia kuna mahali, visiwa ambavyo havijulikani ni vya Kenya au ni vya Uganda. Hata Commissioners wametoka huko, leo asubuhi walikuwa wanatuambia, wanasema hiyo irundishwe kwa sababu wakienda huko wanafukuzwa, na hawafukuzwi tu kufukuzwa.

Watu wa Uganda na wa Ethiopia tunaambiwa wanakuja na mshipi na AK 47, wanatembea huku. Sasa Kenya Police Reserve wana five bullets na ka-machine ka zamani. Sasa huyu akizungumza, Kenya Police Reserve anajiweka chini kwa sababu, ukimzungumzia huyu atakumaliza na hiyo, wao sio wanavita lakini ni wa kulinda mipaka. Watu wa Rarieda na watu wa Bondo walisema hata wameuwawa kwa visiwa hivyo, wanapigwa bunduki kwa sababu wanaambiwa mumekuja Uganda. Ndio mambo ya hapo inafaa ishughulishwe hasa upande wa Victoria na pia mahali popote inafaa ijulikane.

Unajua zamani haingekuwa ukoloni or hawangezidi sana, Kilimanjaro ingelikuwa Kenya, lakini mfalme wa Ujerumani alikuwa anafanya harusi na mfalme wa Uingereza wakazungumza wakamwabia, oh I will give you a present. Sasa wakachora

wakachukua zawadi. Sasa unaona ilienda kwa sababu mfalme alisema na wakati huo kulikuwa utawala ya wafalme kwa sababu tulikuwa kwa wakoloni. Sasa tunafaa kujua mipaka yetu iko wapi because hatuwezi kuitisha Kilimanjaro tena, na I am sure hapa Elgon kuna shida, mpaka unapitia wapi. Sasa hiyo yote itakuweko na hiyo description ya Kenya ni eneo gani, mipaka ya kimataifa iko wapi, iko kwa first schedule. Hapa nyuma ukitaka kujua zaidi, sio wakati huu kwa sababu ni kitu ambacho inafaa uketi uzungumze, kama mama una mtoto nyumbani ambaye amesoma na kufika hata standard eight anaweza kukusomea hiyo na kukuonyesha kwa sababu wamezoea kuchora ramani ya Kenya.

Watu wa mpaka wana shida nyingi sana ambayo inafaa ijulikane Kenya iko wapi, hiyo iko kwa first schedule. Kwa ki-Katiba ya sasa, hatuna mahali popote inatuambia mji mkuu uko wapi. Mkianza tu mseme eh, hata hapa Malava inaweza kuwa headquarters na mung'ang'anie, kwa Katiba ya sasa inaweza kuwa shifted au useme Kakamega ndio,mji mkuu tung'ang'anie na nini. Kwa sababu haisemi na hakuna mtu atakupinga lakini kwa sasa tunasema the Capital of Kenya shall be Nairobi, okay, tunakubali?

**Audience:** Yeah.

**Com. Adagala:** Okay, unajua watu wamebadilisha, Nigeria wamebadilisha walikuwa Lagos wakaenda Abuja ni huko juu, Dar-es- Salaam wakabadilisha ikawa Dodoma lakini hakuwa na pesa nyingi kama wa Nigeria, wa Nigeria wamejenga Abuja, nyumba zote ni mpya, nimefika huko. Vitu vipya, kila kitu, barabara wamepanga lakini wao wana pesa ya petroli na Dodoma nafikiri iko still half half lakini walitaka iwe kati ya nchi. Pengine watu wa kule juu kama wa Turkana na Wasomali, wanakuuliza, "Habari ya Kenya? Pengine capital ingekuwa Isiolo wangejisikia hapo ni katikati. Lakini hapo imejengwa, tumesema hapa Capital itakuwa Nairobi. Lakini itakuwa hivi kwa hii Katiba, tunaweza kuwa na idara ndani ya serikali ambayo itakuwa na headquarters mahali kwingine, okay.

Watu wa Coast wanasema tourism ministry kwa maoni yao iende Mombasa. Masaai pia wanasema hata sisi tuko humo humo sasa pengine idara ingine inaweza kwenda huko. Na watu wa Western region, hii yote, kutoka Marakwet mpaka Nyanza wamesema, sisi ndio wakulima, ministry ya Agriculture walipendekeza kutoka Provinces. Ministry ya Agriculture kwa nini iko Nairobi na juu yake, kwa ni nini imepelekwa Nairobi? Kenya Sugar Authority, miwa hakuna Nairobi. Yes, there are certain injustices like those ones, we want them corrected, lakini ya hapa ni ya serikali ambayo inaweza kutambua departments fulani ziende na tunataka zitekelezwe hivyo ili Ministry of Agriculture ikija hapa Kakamega, tutakuwa na kazi sio?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Adagala**: Hata ya kufagia. Haya sasa vijana wetu hawatukuwa wanaenda Nairobi. Barabara hizi zote zinaenda Nairobi si mnajua hivyo?

**Audience:** Mmh.

**Com. Adagala**: Wawe wanakaa hapa wanafanya kazi na kutunza jamii na wazee pia. Na sasa pia South Africa wamefanya

hivyo. South Africa Bunge liko kwa town moja, serikali iko Pretoria, Executive na Mahakama iko kwa mji mwingine. Watu pia wanatembea, ukienda na pesa zinatawanyika, ubaya wa Kenya, 50% nusu ya mali ya Kenya iko wapi?

**Audience**: Nairobi.

**Com. Adagala**: Yeah, yote. Haukujua mama, iko Nairobi. Ndio unaona watoto wanaenda, vijana wanavutwa na kuenda huko. Tunataka pia iwe hapa ili nchi iendelee, iwe inaitwa pia equitable development. Lugha ya Kenya, mko hapo?

**Audience**: Ndio

**Com. Adagala:** Lugha ya Kenya itakuwa lugha mbili rasmi, Kiswahili na Kiingereza. Kwa sasa lugha rasmi ni Kiingereza. Leo tunapendekeza iwe Kiswahili na Kiingereza na usiseme Kiingereza na Kiswahili, Katiba inasema Kiswahili na Kiingereza. Kiswahili kwanza Kiingereza ….

**Audience:** ………(inaudible)

**Com. Adagala:** Yeah, kwa sababu tunajaribu kujitoa kwa hii mambo ya ukoloni , na watu wengine wanasema hakuna nchi inachukua lugha ya nchi nyingine inakuwa rasmi. Pia hiyo tutaizungumzia juu yake, Kiswahili ni lugha ya taifa, mmeona?

**Audience**: Yeah.

**Com. Adagala:** Nguvu imewekwa upande ya lugha ya taifa na pia mkiwa na district yenu, mnaweza kusema hii district yetu lugha yake itakuwa hivi kwa sababu mtakuwa na huru wa kusema hivo. Kuna watu wengine kama wa Mt. Elgon wana lugha tatu, hiyo inaweza kuwa shida lakini hiyo sasa ni kama mchanganyiko pengine Kiswahili inatosha lakini hiyo ni pia kukuza lugha. Kama hapa tunasema oh watoto hivi, hapa kila mtu sasa atajua Kiswahili, hata mama mwingine alisema kwa vile lugha iko hivyo, sasa tufanye masomo ya wakina mama wajue Kiswahili zaidi okay.

Watu wanasema oh people don't like talking in Kiswahili because they are embarrassed, si attitude, si embarrassment, si kuona ni Katiba, Katiba ikisema hii, miaka mitano itakuwa imebadilika kwa sababu itakuwa kama hawa wa Tanzania, ndugu waenda wapi wewe, we shall be like Tanzania. Na magazeti yatakuweko ya Kiswahili, kwanza Tanzania nilikuweko wana magazeti mengi, I don't know if it is twenty or thirty in Kiswahili hapa tuna ngapi?

**Audience**: Moja.

**Com. Adagala**: Mmh, pengine watu wa Standard wangefufua baraza na wengine waongeze okay. Hapa pia tumekuja kwa serikali na nini?

**Audience**: Kanisa.

**Com. Adagala**: Kuna kelele huko ya nini, kuna kelele nyuma ya nini? We have only two hundred for every constituency, kama

umekuja umechelewa, keti mahali mtu akonayo okay, zingine zitakuja baadaye, lakini kuzungumza inakusaidia. Ukiwa ulichelewa, basi ilikuwa kama first come first served. Hapo dini na serikali zinatenganishwa hapa na hiyo ni kitu simple sana, hatutakuwa na kitu ya dini ya serikali ambayo serikali inasema hii ndio dini ya serikali, haitakuweko. Na dini zote utapata ziko sawa mbele ya serikali. Haya kuna nchi zingine zimechukua dini na dini ni ya serikali, hiyo ni Saudi Arabia, Iraq, Iran hizo ni Islamic Republics, okay. Kuna ingine ya Kikristo ambayo imechukua Ukristo, hiyo ni Vatican. Dini ya Vatican ni ya Roman Catholic, not just catholic, Roman Catholic. Na pia hiyo ni kusema Vatican is a state na Pope is a Head of State, okay. Hiyo tumeelewa, mbele ya serikali kila dini ni sawa.

National symbols, ishara za kitaifa, tunatambuaje Kenya ni Kenya? Tunaitambua kweli kwa ramani lakini tukiwa hapa hatuwezi kubeba ramani kila mahali, sasa inakuwa hiyo ya bendera ya Kenya. Na imekuwa described kabisa, wameieleza kwa third schedule, hapo nyuma schedule ya tatu. Wimbo wa taifa, unajua ukisema tu, ee Mungu nguvu yetu, inaeleweka hii ni Kenya, hata iwe bila maneno ni piano pekee inapiga, wanajua hiyo ni Kenya.

Hiyo tunaita crown, sijui inaitwaje. Tutaona kwa tafsiri wataita aje au kuna mtu hapa anajua vile inaitwa? Halafu mhuri wa hiyo serikali inatumia, pia inatambua Kenya, tulikuwa na mzee hapa alisema Wa-Quaker wanafanya hivi, ihifadhiwe kwa… umeiona mzee? Mzee M-Quaker?

**Audience:** Ndiyo

**Com. Adagala:** Yeah, oath and affirmation okay. Hiyo ni fourth schedule, tutaangalia affirmation inasema nini kwa fourth schedule na oath ile ya kuapa. Lakini ninataka kusema, Commissioner Baraza na mimi ni wa Quaker, tulipoenda kuapa kuwa Commissioners, tulibeba tu mkono hivi na wakasema oh, hapa hauwezi kuapa kwa bibilia na Waislamu waliapa kwa Qur'an na sisi tukafanya hivi, kwa sababu yetu inatuambia tunafuata hiyo maneno ya Yesu inasema, msiape kwa Biblia halafu tunaendelea. Umefurahi mzee wa kikwetu?

**Mzee**: Ndiyo.

**Com. Adagala**: Wa kwetu wakifurahi inaonekana wazi. National holidays, siku za kitaifa, moja ni tarehe mosi mwezi wa sita, inaitwa Madaraka day, ingine ni tarehe kumi na mbili, mwezi wa kumi na mbili inaitwa Jamhuri day. Tutakuwa na ile siku Katiba itatekelezwa, itaitwa Katiba day, hatujui hiyo itakuwa lini okay? Bado tuko kwa draft, bado tuko kwa mapendekezo, okay. Kwa hiyo sehemu, kuna mtu ana jambo lolote la kusema? Nataka muwe chemchem, wa Kabras mnajulikana. Ukitaka kuzungumza njoo mbele, usikae chini kwa sababu ukiketi chini hakuna mtu wa kuzungumza na tutaendelea.

**Speaker**: Just a correction madam.

**Com. Adagala**: Utakuja mbele na kufanya hiyo vitu, ukiketi huko itakuwa tutaendelea. Ukitaka kuzungumza utakuja mbele upange laini.

**Maikuva Shitanda:** Mimi naitwa Maikuva Shitanda. Madam Commissioner, maybe before tufike kwa National days, nilikuwa na comment kwa National symbols under the court of Arms. Under the court of Arms tulikuwa tunapendekeza kwamba tuwe na mabadiliko kidogo kwa sababu vyama vya kisiasa ambavyo vimesajiliwa hapa Kenya, vinatumia zile ishara zinafwanana na za serikali. Utapata kama Ford Kenya iko na simba na pia tuko na simba katika court of arms. Kwa hivyo nilikuwa ninaonelea, vile vyama ambavyo vimesajiliwa hivi nyuma, ikapata kama court of arms zimeshaundwa, ziwachilie zile ishara ambazo zinafanana na za kitaifa.

**Com. Adagala**: Na zile zilisajiliwa mbeleni?

**Maikuva Shitanda**: Hata zile ambazo zilisajiliwa mbeleni kama tuseme KANU, ukiona ile ishara ya KANU, utapata kuku imeshika mshale, jogoo imeshika shoka. Na utapata pia simba iko kwa ile ishara pia na hiyo simba inapatikana kwa court of arms ya serikali, ndio tunaonelea hata zile za mbeleni, wacha ile court of arms ya kitaifa iwe kama Katiba and the coming ones to be in consistence with them.

**Com. Adagala**: …….(inaudible)

**Maikuva Shitanda**: Ni lazima vile vile, sisi huwa tuna-changanyikiwa kidogo, hata ile bendera ya KANU na ya kitaifa, hatutafautishi kabisa. Tungeonelea kama tungeweza kutoa maoni ili hizi bendera ziwe na tofauti kubwa ambazo saa zingine vyama vingine vinajipendekeza hata kwa rangi karibu na ya serikali, na hata wa mama ambao hawajasoma sana wanaona KANU ni serikali ama chama cha Ford Kenya ni serikali, kwa hivyo iwe na …

**Com. Adagala**: Poor mamas, angalia kwa third schedule, kijana, utaangalia kwa third schedule na utafanya submission okay.

**Jotham Raban:** Kwa majina ni Jotham Raban. Mimi maoni yangu ni kuhusu the National holidays, mmeangalia Kenyatta day, labda tena Katiba day na tukakuwa na Jamhuri day. It is my proposal that we should have the heroes' day, ambapo ….

**Interjection:** (inaudible)

**Jotham Raban**: The National days…

**Interjections:**

**Com. Adagala**: Kuna mtu mmoja pekee anazungumza tafadhali wa Kabras. Mtu mmoja pekee ndiye anazungumza.

**Jotham Raban**: Yeah, Madaraka day, Jamhuri day and Katiba day.

**Com. Adagala:** …..(inaudible)

**Jotham Raban**: I apologise, it was my proposal that the heroes' day should also be included for the purpose of recognizing the heroes of this country in the various activities they did in coming up with a Constitution or creating multi-party or fighting for

the freedom of this country. So it is my proposal that the heroes' day be included in the National holiday, thank you.

**Com. Adagala**: ………..

**Jotham Raban:** A day that shall be agreed by Kenyans.

**Com. Adagala**: Already Kenyans (inaudible).20th

**Jotham Raban**: 20th of October to replace Kenyatta day.

**Com. Adagala:** You are a Kenyan.

**Isaya:** Maoni yangu ni juu ya currency of Kenya, upande wa pesa. Pesa zimekuwa… Pendekezo, symbol ya pesa tungeangalia kitu common katika nchi yetu .

**Interjections:** (inaudible)

**Isaya**: Tungeangali kitu ambacho ni common katika nchi ya Kenya,

**Com. Adagala**: ……..(inaudible)

**Isaya**: Na hiyo symbol ya Kenya, badala ya kuweka kila President ambaye anakuja anabadilisha…

**Com. Adagala**: Tunataka useme hiyo kitu ni nini ambayo iko common? Ukiingilia ma- President ………

**Isaya:** Okay kama Mt. Kenya, ingekuwa permanent symbol ya pesa.

**Com. Adagala**: Hata ukiingilia President, ameingiliwa sana kwa hii Katiba. Haya mwingine, I want someone to sit here and a committee member, someone who is not busy to sit here.

**Charles Wachiko**: My names are Charles Wachiko, when I look at the National holidays, my suggestion here is, why have you omitted this Christian holiday of 25th?

**Com. Adagala**: What?

**Charles Wachiko**: December.

**Com. Adagala**: What would you like?

**Charles Wachiko**: It would have been included in …

**Com. Adagala**: Don't ask a question have a (inaudible).

**Charles Wachiko**: Ningependa nyinyi mtuongezee hiyo tarehe ishirini na tano ya December, kwa hizi zingine ambazo mumeandika hapa chini.
**Com. Adagala**: Tarehe ishirini na tano ya December.

**Charles Wachiko**: I have seen it, Christmas
**Com. Adagala:** Okay, hizo zote, New Year, ……… St. Peters, St. Patrick, St. what, St. Teresa and Christmas na Iddul Fitr, hizo zote ni Public Holidays.

**John Kariuki**: My name is John Kariuki, I want to talk about the National symbols, the court of arms ama kirauni kwa Kiswahili. Ningelitaka zile kirauni zibadilishwe. Kwa upande wa nyuma kuna simba wawili ambao wanaonyesha kwamba hii society ambayo tuko ndani ni ya man eating man society. Kwa hivyo tungelitaka picha ya kuonyesha ya kwamba upande moja kwa sehemu ya Kenya tuko na wa mama na upande mwingine tuko na wanaume na symbol ya picha fulani kama ya Kangaroo imebeba mtoto na mama, inaonyesha kitu kama hicho. Hizo simba mbili ziondolewe, halafu pale tena kuna jogoo na shoka,

**Com. Adagala**: Kijana, you are addressing the Commission ……….
**John Kariuki**: Okay, pole. Halafu ile jogoo ambayo iko nyuma ya kirauni, tungelitaka iondolewe kwa sababu inaonyesha uchokozi, halafu kuna shoka, shoka haina kazi yeyote kwa taifa letu ni ya kupasua taifa, tungelitaka kitu ambacho kitaonyesha kinaunganisha taifa ama ni cha national unity.

**Com. Adagala**: Okay, unajua kwa pesa za nchi zingine, wanakuwa na President wengi kama America. Kama kwa centi moja they have picha ya President fulani, ndururu, wanaita dime na hiyo si dine hiyo ni 'dipo', wako na kichwa cha President mwingine. Kwa ten cents, iko na kichwa cha mwingine, kwa quarter, pesa nane wana kichwa halafu wana dola moja ambayo ni ya karatasi na hizo zingine ni za kichuma, wana kichwa cha President mwingine. Halafu dola mbili, halafu ya tano, kumi, hamsini na mia moja, tofauti tofauti, okay.

Ishara hiyo inaweza kuwa tofauti kwa kila pesa hata itasaidia watu wengine kutafautisha. Na za Holand wameweka maua, kama ua fulani, indigenous wanaweka kwa sababu hata economy yao ni economy ya maua. Maua inaleta pesa nyingi sana kwa nchi yao, okay. So mnafaa mfikirie, huyo kijana ameenda kabisa. Mfikirie zaidi, najua mnataka kuingilia hawa President wawili wamekuweko lakini pia mfikirie tunatengeneza kitu ambacho kitadumu lakini tumeandika bila (inaudible).Lakini kwa America lazima President kutoka tarehe alifariki imalize miaka hamsini ndio aweko. Vile wanapenda Kennedy, hayuko mpaka itakwisha miaka hamsini ndio atakuweko, sasa itakuwa arobaini.

**Elphas Ngongo**: Asante sana Commissioner, tunaweza kukosea kwa sababu wengine ni mara yetu ya kwanza. Jina langu ni Elphas Ngongo, Church leader, Salvation Arm Church. Na nilikuwa ninasema, Commissioner asante, mara nyingine huenda ni

mara ya kwanza wengine kuhudhuria Commission hii, sasa hata tukikosea kusimama ama kuchelewa lazima tuwe interested ndipo tusimame kusema lolote, ulinifukuza mara ya kwanza sasa usinifukuze tafadhali na neno langu ni kuhusu state and religion ya kwamba the state shall treat all religious equally. Lakini hiyo ni nzuri, mimi ningelipendekeza tuwe na Ministry for Religion affairs katika Republic ya Kenya ili dini zote, zitakuwa zikielekeza …. .

Ya pili, hatungelipendelea tuwe na devil worshippers katika taifa letu, kwa maana wa Kristo hatuamini kumuabudu shetani. Hiyo ndio maneno yangu na nimependekeza hayo, asante sana kwa kunisikiliza.

**Com. Adagala**: Asante mzee wa Salvation Army, ngoja kidogo. Inaweza kuwa Ministry, what we need is an institution, inaweza kuwa ministry, inaweza kuwa Commission. Mnafaa mfikirie ni ipi bora, okay? Also, when we were talking earlier on- were you here? about religious issues, about Chief Kadhi. You need to make… You know we need even to have courts which can talk about Christian people, mnatupwa huko kwa court za dunia. I have been told be in the world but not of it, lakini mumetupa watu kwa court ya dunia. Kuna vitu vingine vinafaa vishughulishwe. So you need to think about these things, inaweza kuwa ministry, Commission na pia court.

Nafasi ipo lakini hamjajitahidi wa Kristo kulete hayo mambo kamili. If you want a Ministry, how do you want it to be? If you want a registry of Christian churches, how do you want it to be so that you don’t register in the … I am trying to tell Christian leaders, you have a big responsibility which you need to take up and it needs to be taken up in very few days, otherwise mtakaa hivyo. Mnaweza kupewa Ministry lakini pengine haitatosha hiyo kazi yenu. Mnasikia we have many institutions, Wakristo wanasema they are 80%, wa Muslim ukiwauliza wanasema wako 40%, sasa Kenya yote iko 120%, unasikia? Mnafaa mfikirie, tutaweka Ministry, lakini you need to think yourselves.

Mkristo akikosea Mkristo mwingine anampeleka wapi? Ilisemekana kwa bibilia usimpeleke kotini, anapelekwa wapi?
**Audience:** (inaudible)

**Com. Adagala**: But you don’t say it just like that, this is Katiba now, we need to know that there are some cases that are decided outside the court. Do you want it to be outside? Waislamu wamesema yetu tunataka iwe kwa Katiba, you want it to be outside Katiba? Fikirieni hiyo vitu, Ministry yes, it can be a Commission also, it can be court also and you can have them. I don’t know if you are seeing that chance. It can be there but you have to think, angalia hiyo ya nini pia, it can even be… We have an Electoral Commission which will be registering political because political parties said we don’t want to be in that NGO place.
We are political parties, we want to be somewhere and they said and we put them, okay Electoral Commission, hii Commission itakuwa ina register. Look at the thing of the Electoral Commission, how it is proposed, look at the Chief Kadhi, and look at the court.

Wa Kristo mna nafasi kubwa but you don't exist because you have not said your it yourselves, okay.

**Elphas Ngongo**: Now kuna NCCK na viongozi wetu wanaotuwakilisha, sasa watu hao huwa wanatusaidia kwamba, tuwarudie na tutawapataje kwa maana hatuwapati humu vijini na nyumbani?

**Com. Adagala**: Hilo si swali la Commission, hiyo ni NGO, I am telling you there can be a stronger institution established, but Christians will have to say them and I don't know if NCCK is there. You can have a place where Christian churches are registered not with NGO's you can have courts for Christian cases, not hii mahakama ingine. It can be recognized in the Constitution, this is the time to do it. This is the time to do it, you will get together, you will do it.

**Patisi Koroti**: Thank you very much, kwa majina naitwa Patisi Koroti. Nafikiri wazo langu ama shuku langu liko kwa neno capital, na kama kwa fikira yangu nafikiri capital pia ni city na wakati wa kusambaza maendeleo, nafikiri hii Katiba inataka kulenga maendeleo yaje kwa wananchi na mfano mmoja, mkipewa kitu kama city status, maendeleo ya-harakakishwa. Kwa hivyo ningependekeza kwamba kila Provincial headquarters ziwe promoted to city status ili maendeleo yafikie wananchi, ni hilo tu.

**Com. Adagala**: Sawa, pendekezo nzuri.

**Japheth Kuronga:** My reactions is on territory part two …
**Com. Adagala:** …..reactions, pendekeza.
**Japheth Kuronga:** On the decision of the republic into district and provinces ….

**Com. Adagala:** (inaudiable)
**Japheth Kuronga**: Thank you I wanted to …

**Com. Adagala**: The territory of Kenya has international boundaries okay? Including hiyo ya Indian ocean. Hii ingine itakuja. I want a young committee member to come and sit here.
**Speaker**(inaudible)

**Com. Adagala**: Lakini he was standing, I want him to sit here.
**Speaker**: Kuna mbao hapo.
**Com. Adagala**: There no chairs, there was an extra chair. Bring a chair. Tunaendelea.

**Japheth Kuronga**: Sawa tutaendelea na …

**Com. Adagala**: Kwa sura hii vile nimemwambia, mzee unazungumza sana sijui kwa nini, poa, huyu mzee nataka ujiweke pole pole. Kuna watu ambao wamefanya vitu hata mtu ana ahidi, lakini hakutimiza sivyo? Hiyo ndio mambo ya siasa, lakini hata kwa maisha yetu, hatuna lengo pia. Tuliambiwa lazima tuwe na nia, lengo na njia tunaelekea na vitu ambavyo tunatarajia vitatendeka kwa wakati huu hakuna. Sasa hii ndio sura hapa, na wale ambao wamewafanyia maendeleo, muwashukuru kwa sababu ilikuwa kwa hiari lakini sasa haitakuwa hiari, bali itakuwa kitu ambacho kitafaa kutimizwa, report itolewe kila mwaka.

**Vincent**: Sura hii ya tatu inaongea juu ya maadili ya kitaifa, maadili haya katika sehemu ya kwanza ya kifungu hichi, maadili haya yatafuatwa na viungo tofauti vya serikali. Ikiwa ni kiungo cha Bunge, Mahakama na Rais, maadili haya ni kama umoja wa kitaifa kwamba serikali ya Kenya itakuza umoja wa kitaifa. Pia sisi wakenya tuko tofauti lakini tuko kitu kimoja, hivyo kuna adili ya despite the recognition of diversity, watu wa aina tofauti tofauti, sisi tutaishi kama jamii moja. Adili nyingine ni adili ya demokrasia kwamba Jamhuri ya Kenya, itakuza demokrasia, maswala ya kitaifa yatakuwa ya wazi na transparency na accountability wazi. Na kutakuwa na mfumo ambao utatupilia mbali hongo ama ufisadi.

Mahakama zetu zitakuwa huru na vyama vya kisiasa vitafanya huduma ama juhudi zao bila kuingiliwa ama kukorogwa na kuvurugwa kwa njia tofauti tofauti na serikali. Maswala ya mashirika yasiyo ya serikali pia yamepewa kipao mbele hapa, yatafanya shughuli zake bila kuvurugwa kwa njia yoyote na serikali ya nchi. Pia heshima kwa haki za kibinadamu ni adili ambalo limeangaliwa ama limesizitishwa katika Katiba hii.

Pia vikundi ambavyo vimebaguliwa, marginalized communities na wanawake wamepewa kipao mbele katika mswada huu kwamba wata perticipate katika maswala ya economic au social bila kunyanyaswa. Na theluthi moja ya afisi za umma iwe ya kuchaguliwa ama ya kuteuliwa itashikiliwa na wanawake.

Maswala ya watoto pia yametambuliwa kwamba watoto watakuzwa kwa njia bora ama watalindwa kwa njia bora. Haki za kimsingi na matarajio ya kimsingi kama vile chakula, makazi, elimu, maji safi, mazingara na ulinzi, pia zimepewe kipao mbele katika mswada huu. Pia jamhuri ya Kenya itahimiza maendeleo katika kila pembe ya Jamhuri hii, equitable development. Na Jamhuri ya Kenya itabidi iwe wanachama bora zaidi wa bara letu la Afrika, na mara moja kwa kila mwaka, Rais atatoa ripoti kwa Bunge ikionyesha jinsi maadili haya yametimizwa.

Kifungu cha kumi na tano katika sehemu hii, kinaongea juu ya majukumu ya wananchi wa Kenya, sasa kila mwananchi wa Kenya ako na jukumu fulani. Jukumu la kwanza ni la kujifundisha Katiba. Kila mwana Kenya anahimizwa ajifunze Katiba, awe tayari kulinda na kupigania Katiba hii, ashiriki kwa maswala ya demokrasia, awe ni mtu ambaye anasisitiza elimu.

Maswala ya welfare community pia imeangaliwa na serikali itahimiza umoja wa kitaifa. demokrasia na sheria pia itatekelezwa na serikali hii pia itahimiza ama itakuza maisha ya kifamilia. Katiba hii pia inalinda mazingara yetu na kila mwananchi itampasa ayalinde mazingara yake vyema.

Kila mwananchi ako na wajibu wa kutoa habari, ni muhimu kwa idara zinazohusika na usalama na kila mwananchi anahimizwa asiwe mfisadi. Kila mwananchi pia itampasa alinde mali ya umma na hivyo jukumu la mwisho itakuwa kwamba kila mwananchi itampasa aweke nchi yetu ya Kenya kwa ramani bora katika ulimwengu nzima. Kwa ufupi hayo ndio mapendekezo yaliyo katika sura hii ya tatu.

**Com. Adagala**: Haya mumeyasikia, kuna kitu chochote hapo mgependa kusema? Wacha tuendelee tukilinganisha na mahali kwingine mtaona lakini sasa Kenya ina nia. Wa Tanzania hata sasa wanasema nchi ambayo ina nia, walikuwa wanasema Tanza-nia. Kenya haikuwa na nia, sasa iko nayo na mumeona vile imetendeka.

Uraia, mmeona uraia, citizenship. Raia wa Kenya ni mtu wa aina gani? Unaweza kuwa kwa eneo la Kenya, lakini wewe ni Mkenya? Sasa hapo ndio kitu muhimu. Kwa kila raia wa Kenya atakuwa na haki sawa vile iko kwa Katiba. Pia kuna wajibu na vitu vya kutendwa ambavyo ni vya lazima, ambapo watazitimiza kwa usawa.

Kuna haki ya Passport na stakabathi zingine za kujitambua kama kitambulisho, una haki ya kupata hiyo bila ya kuhangaika sana. Sisi ambao tuko hapa na ni wanakenya, uraia wetu umehifadhiwa sasa katika hii Katiba. Tulipokuwa kwa ukoloni tukipata uhuru, walisema wale ambao walikuwa British subject sasa atakuwa Kenyan citizen. Sasa tunasema wale wako Kenyan citizen sasa, watakuwa pia na kuendelea isipokuwa hivyo, ingetubidi tufanye application sote, ingekuwa msongamano mwingi sana, isn’t it?

**Audience:** Yes.

**Com. Adagala:** Yeah lazima tuilete hiyo kwa sababu ni Katiba mpya, tuilete hiyo iwe hapa, hiyo ndiyo bridge tunafanya, *nguraro* mnaitaje bridge kwa kikabras.?

**Audience**: Vularo.

**Com. Adagala:** *Vularo ivenivwo*, so that you can walk from one Constitution to another. Hiyo ndiyo hiyo bridge okay? Na wale ambao wamesajiliwa kuwa Kenyan citizen, sasa sisi tuko. Kutoka siku hii ambayo Katiba itatekelezwa hiyo Katiba day kuendelea mbele itakuwaje? Wale watazaliwa kwa eneo la Kenya watakuwa wa Kenya, ukizaa mtoto hapa na wewe ni M-Rwandeese huyo mtoto ni Mkenya okay? Hivo ndio iko kwa nchi zengine kama US, nikienda huko, nikikaa huko nizae mtoto, huyo mtoto ni American citizen na si mchezo. Saa zingine unakuja hapa unasema mtoto alizaliwa America ako hapa anaishi lini. Wanakuja mpaka hapa Kabras, nafikiri tulikuwa hapa na Festo Mlenge, alikuwa America hata nilimjua, hawa watoto wake ni Americans.

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Adagala:** Haya ikiwa hivyo wale watazaliwa, unajuwa tulikuwa Hamisi ambayo ina watu wa kalenjin na hawakuwa wanafanye hivi, sasa sijui nini, sitataja kabila yeyote kwa sababu mnashida zenu sitaki kuingia. Mtoto mzaliwa atakuwa Kenya, yule atasajiliwa pia atakuwa Mkenya, yule ya kufanya application na kuhojiwa pia atakuwa Mkenya.

Hiyo inafuata ni maelezo tu, halafu tuende chini. Kuna watoto ambao wako adopted, tafadhali kama una mambo enda sokoni uzungumze huko, tafadhali, mnaharibu tafadhali. Na ninauliza halafu nitachoka, kazi yetu ni ngumu sana na mkifanya ngumu zaidi, nina njia ninaweza kufupisha hii yote halafu mtakaa nje na hamtajua nimefupisha.

The adopted children, watoto ambao mtu ana ..watu wengine wanasema kununua lakini jina nzuri ni nini kwa Kiswahili? Wale ambao hukuzaa lakini unakuwa mzazi. Hao pia watakuwa na haki. Dual citizenship, hiyo ya mara mbili, Lumumba anaita uraia marudufu. Hiyo itakuweko, unaweza kuwa raia wa nchi hii, na uwe raia wa America, Russia, lakini Ujerumani ni ngumu kidogo. Ukiwa raia wa Ujerumani wanakwambia utawacha hiyo nyingine. Nchi yetu pia sasa iko hivyo, kama dada yangu ako Zimbabwe, alipotaka kuwa Zimbabwen citizen kwa sababu anafanya kazi huko na aliolewa huko pia, aliambiwa lazima uache ya Kenya. Halafu Kenya pia wakamwambia lazima uache ya Kenya kwa sababu Katiba zetu zinafanana hapa.

Mtoto wake ambaye alichelewa kufanya application mwishowe alikuwa America alikaa bila mahali kwa sababu si wa Kenya, Zimbwabwe wala America. Sasa akafanya resident America lakini hawa wakenya walio ng'ambo waling'ang'ania sana hii dual citizenship ili wasipoteze ile ya Kenya. Nafikiri mnaelewa. Pia mpakani kuna watu ambao wako na shida sana, kama wa Digo wa Tanzania na wa Kenya, wa Samia hapa wako…Sasa unajua ndugu wawili Awori na Awori wote ni Presidential candidate.

Hao pia wanashida, wanasema unafunga ndoa halafu unakaa miaka thelathini, huyu mtu si Mkenya, anazaa watoto na yeye si Mkenya, watoto ni wa Kenya, sasa watu wa mpakani kwa hii hali ya mashinani wana shida. Pia kuna hiyo hali nyingine ya kimataifa ya kusoma na watu wafanyi biashara, wana shida.

Uraia wako unaweza kutupiliwa mbali ikiwa uliupata kwa njia ya corruption, ya chini ya meza hiyo au ya kufanya hivi na hivi halafu Godfather anakupatia halafu unapata. Siku hizi ninaambiwa uraia wa Kenya ni shilingi million tano, mtu akitaka kwa hiyo njia. Sasa kuonyesha uraia ni kitu muhimu, sasa muangalie hayo mambo yamesemekana hapo ili mchunguze kabisa.

Mzazi akifa kama mtoto hajazaliwa, mtoto huyo atachukuwa uraia wa hiyo… Ukitaka kuishi kuwa resident Kenya na hautaki uraia kama hao wakenya wako Germany, kwa sababu hawawezi kuwa na uraia mara mbili, wanaweza kuwa wakaazi, ni resident. Hata saa zingine mnaona wanaandika kwa gazeti resident in America. Wale walikuwa wamepoteza uraia wao kwa ile Katiba ya zamani, sasa ukiwa Ujerumani, unaweza kuwa resident na kuna haki ambazo mtu anazo kwa hiyo hali ya resident.

Mwanamke au mjane kwa sababu walikuwa wamekatazwa wanawake wasiwe na uraia wakiwa wanatoka kwa nchi nyingine, sasa wao wanaweza kuwa resident wakitaka. Mtoto wa raia huenda ikawa alizaliwa kwa nchi ingine, huyo pia anaweza kuwa.

Parliament itakuwa na mwaka mmoja kufanya haya mambo yote kuwa nyororo kwa sababu iko tofauti kwa Katiba ya sasa na hii mpya. Paliament itaketi na itatoa Act au sheria ambayo itasimia uraia yote. Kuna halmashauri ya kusajilisha uraia, watu wote watakuwa wakisajilishwa kwa halmashauri ya kusajilisha uraia.

Response? Kuna mambo ya kuongeza hapo, maoni, muwe chap chap ndio itokee. Niliambiwa watu wa Matete walikuwa na maoni mengi sana, sijui wali-lala njaa.

**Jonathan Masinde:** Mimi ninaitwa Johanthan Were Masinde. Maoni yangu kwa mambo ya uraia yote yanahusu mtu ambaye ana uraia mara mbili. Hii mumesema kwa Katiba hapa ya kwamba inakubaliwa.

**Com. Adagala:** Watu walituambia ….

**Jonathan Masinde**: Na mimi maoni yangu ni ya kwamba si nzuri kwa sababu Kenya saa hii mali yote ambayo inaweza kuonekana iko kwa mikono ya Asians ambao ni raia wa Kenya. Na hii ikiendelea, kukiwa na kitu kidogo kifanyike, hawa watu wote watahama Kenya na watakuwa wamehama na hiyo mali. Kitu gani mmefanya ili mtu aliye na mali ya hapa hawezi kuondoka nayo kwa sababu ya uraia mara mbili?

**Com. Adagala**: Unataka nini ifanyike?

**Jonathan Mashinde**: Ninataka iwe ya kwamba uraia wa Kenya, mtu anaapa kama anataka kuwa nayo mara mbili, ile mali ambayo anayo hapa hawezi kuhama nayo akienda kwa uraia ingine.

**Com. Adagala**: Sasa hiyo, kuja huku mzee Werengai, ngoja kidogo. Kuna vile nilisema Katiba inatoa nia halafu Bunge itatoa sheria. Hiyo tutapeana kwa Bunge tuseme inafaa aape mali itabaki hapa, okay?

**Joyce Kamuli:** Kwa majina ninaitwa Joyce Kamuli nataka kuongea juu ya wamama na watoto na pia kwa citizenship.

**Com. Adagala**: Pendekezo.

**Joyce Kamuli**: Pendekezo la kwanza ni kwamba, serikali imekuwa ikisema wanapitisha maneno kuhusu wa mama lakini haijawahi kuweka jukumu la kusema wakati wanapitisha kitu inakuwa inafanyika hivyo. Ndio unapata wamama tuna shida ..

**Com. Adagala**: Pendekezo lako?

**Joyce Kamuli**: Pendekezo langu ni kwamba wa mama wakati wamesema tukuwe na haki kama ya kupata shamba, iwe imepitishwa na iwe ni kupata shamba. Raia wa Kenya, inatakikana kama umeandikishwa kama ni mtu wa Kenya, uwe ni mtu wa Kenya na wakati unahama unaenda nchi ingine, inatakikana tujue wakati unahama kama ulikuwa umejiandikisha Tanzania na

Kenya, na wakati unahama ukija Kenya, utuambie ni nini ulipata Kenya na utawacha hiyo mali yote hapa.

Jambo la pili, tunataka wakati mtu anaandikishwa kama Mkenya ilhali siye, atuambie interest yake ya kuwa Mkenya ni nini. Kwa ajili mwingine anakuja na kumbe anakuja na njia nyingine fulani, sasa atuambie ni kwa nini anataka kuandikishwa kuwa mwanakenya. Na kama atafika pahali tuone hana uraia wema, tuwe na haki ya kumpa nafasi ya kurudi kwao.

**Com. Adagala**: Hiyo kuwa uraia pengine anaweza kusema na nia nzuri na hiyo ni uongo. Sasa hiyo ni njia ya kujipatia uria kwa corruption. Uongo ni corruption.

**Thomas Kasaya:** Majina ni Thomas Kasaya, na ningependa kusema hivi kuhusu uraia, ningependekeza ya kuwa, tungekuwa na vipengele hasa kuhusu wale ambao wanakuwa na uraia mara mbili, wale ambao tunasema dual citizenship. Kwa mfano tuko na ndugu zetu ambao wanakaa mpakani karibu na Uganda, umetoa mfano wa Awori na ndugu yake Henry, ndugu yake alikuwa ana contest Urais huko na ndugu yake alikuwa anahitaji ku-contest Uraisi upande huu. Na hiyo tukitoa mfano mwingine unaona wasomali wa Kenya na wasomali wa Somaliland.

**Com. Adagala**: Una-takaje?
**Thomas Kasaya**: Kile ningependekeza ni kuwa tuwepo na vipengele ambavyo vitazuia zile practices au mtu ambaye ako na uraia mara mbili, vitu ambavyo anaweza kujihusisha navyo na vitu ambavyo hawezi kujihusisha navyo.

**Com. Adagala**: Usingoje, utapanga laini kama wengine, usingoje mtu atoke halafu unatoka tafadhali. Really, I am trying to establish some order here na you don't want to follow it, ukitaka kuzungumza utasimama mwanzo, uje.

**Interjection:** ….(inaudible)

**Com. Adagala**: Wewe ni Councillor, you are a law maker.

**Cllr. Nalyanya**: Sorry for the inconvenience. Mimi ninge-suggest kwa hii Constitution kwanza juu ya uraia. Naitwa Cllr. Nalyanya. Tusikubali ama Constitution yetu isikubali mtu awe na uraia mara mbili, kama mtu anataka kuwa raia wa Kenya, awe ni raia wa Kenya lakini kuwa raia wa Kenya tena Uganda ama nchi nyingie, sio nzuri.

**Com. Adagala**: Tulikuwa na hilo pendekezo sio mara ya kwanza tulikuwa nalo mwanzo. Huyo mama ndio mwisho kwa hii laini, sitaki watu kufanya madharau hapa. Ni madharau kwa mimi na ni madharau kwa hawa wengine. Tulikuwa na hilo pendekezo Cllr. Nafikiri unaweza kusikia na kutembea, lakini vile tulifanya kazi kwa Commission kwa mambo yote, tulikuwa tunaangalia mambo yote halafu tunapanga, kuna hii ya upande ule zaidi, extreme right na extreme left.

Wengine walitaka multiple citizenship na kuna kitu kama hicho. Unaweza kuwa na uraia wa nchi tatu au nne lakini vile tulikuwa tunafanya tulikuwa tunachukua maoni halafu tunachukua ile ya katikati, ile iko na watu wengi ambpo wamesema. Watu wengi walisema dual citizenship, sasa hiyo ndio tulichukua, wakati huu si wa kutoa, tutaandika maoni tuseme bado mtu huyu anasema hivi, lakini sasa tuko Form two, siyo Form one, Form one ni vile tulikuja hapa tukiwa Commissioners watatu na kuchukua maoni. Sasa tuangalie hii na kuendelea mbele, hii siyo ya kurudisha nyuma ni ya kuendelea mbele, mumeelewa ya Form one na Form two?

**Audience:** Yeah.

**Peter Kabwegu:** Mimi ninaitwa Peter Kabwegu na ningependa kupinga pendekezo ambalo linasema mtu akioa mwanamke kwa muda wa miaka tatu tu, anaweza kuandikishwa kama raia wa Kenya. Hiyo nasema sio ukweli kabisa, afadhali mtu angeoa kwa sababu kuna wanawake wengi ambao wako tayari ku…..

**Com. Adagala**: ……nataka uwe corrected, hiyo ni kuoa mwanamke au mwanaume na sio mwanaume ndio wa nchi, najua mnaanza halafu mnaingilia wanawake, na ikiwa mwanamke ana nia mbaya kwa nini wewe ni mjinga sana unadanganywa? Endelea………..

**Peter Kabwegu**: Kuna wanaume hata wanawake ambao wako tayari kuchukua hongo ili wapatishe hao matajiri kupata uraia, sasa mimi ninapendekeza miaka kumi ambayo hata inakubaliwa na sheria ya sasa iwe ndio mtu anaweza kukaa na bibi au bwana ndio aandikishwe kama raia wa Kenya.

**Com. Adagala**: Tumesema hongo, ikipatikana ulifanya hongo, hiyo tumeshazungumzia hapo mbeleni utapoteza uraia. Ya pili, wewe unafaa uwe raia mwema na ukichukua hongo kwa kupata pesa ili mtu awe raia utakuwa na shida na pia ikiwa una-funga ndoa na huyo mtu anaenda na hakuambii kabisa, kile anataka ni uraia. Inafaa uwe raia mwema na mwerevu, usidanganyike. Inafaa ulinde uraia wako na nchi yako, inaitwa uzalendo.

**Grace Fedha**: Kwa majina naitwa Grace Fedha nami kuhusu uraia kama mtu ni raia wa Kenya, ninapendekeza mali yake iwe Bank, ili huyu mtu akienda mahali nje akuwe na uraia mbili, ako hapa ako kule nje, neno likifanyika hapa mbaya, mali yake yenye iko nje ndio anaenda kutumia na anawacha wa Kenya kwa taabu. Kwa hivyo ninapendekeza akiwa raia wa Kenya, mali yake yote iwe hapa Kenya na wakati neno linatendeka, naye pia aende hasara vile wengine wanaenda hasara.

**Com. Adagala**: Asante mama, sauti nzuri nyororo ya mama, nimefurahi. Hiyo yenye mzee Werengai alitoa imeungwa mkono lakini unajua pia kuna raia wengine hapa wazaliwa wa Kenya lakini mali yao iko nje. Hiyo pia inafaa pengine ilikuwa na jambo .. mimi siwezi kusema lakini ninamjulisha tu kwa information, lakini ikiwa kuna mtu ana kitu cha kusema hapo, pengine mzee Werengai ungeongezea

**Masinde**: Hiyo ninaongeza nikisema ya kwamba sio wale wageni tu ambao wanaomba, kuna wengine ambao walizaliwa hapa kama wenyeji kabisa na automatically ni watu wa Kenya. Lakini kwa sababu ametengeneza hapa mali na ameipeleka nje, mtu kama huyo hata kwa Constitution yetu, ingekuwa wazi ya kwamba hafai kupewa uongozi wowote na ikiwezekana, a- declare hiyo mali yake ili aweze kuchukua uongozi wowote kama mali imerudishwa hapa.

**Com. Adagala**: Asante mzee Werengai, juzi kulikuwa na mtoto wa tajiri wakasema ameenda kuuza mali ngambo, sehemu kidogo tu na ikawa 60 billion, haya tuendelee. Haya mzee, hii sehemu sura ya 5 kwa Katiba ya sasa tuko nyuma sana wale mumeangalia, tuko nyuma huko mwishoni na inaonekana wale walitengeneza hawakujali sana maisha ya wananchi kwa sababu kwa ile tafsiri ya Kiswahili, hii sura inaitwa ukatiba. Kuishi ki-Katiba, haki na wajibu wa ki-Katiba. Najua civic education mliambiwa, freedom and rights lakini pia kuna responsibility and duty, hizi zinaitwa Bill of rights. Ki-Katiba, kuishi ki-Katiba lazima ujisikie kwa maisha yako, Katiba inatekeleza au wewe unaitekeleza, isiwe sasa serikali tu au wakati wa kura tu au political party tu. Kwa maisha ya kila mwananchi, na wananchi millioni thelathini, nafikiri thelathini na moja sasa wanasema.

Lazima ujisikie na lazima ujue vile Katiba inafundisha na vile inafaa wewe ulinde Katiba by performing your duty and responsibilities, okay? Sio upande tu unaitwa Bill of rights, yes, lakini pia ina duties, responsibilities and freedom there okay? Haya kijana ataendelea.

**Vincent:** Sawa tuko katika sura ya 5 ambayo inaongea juu ya Ukatiba ama haki za binaadamu. Katika sehemu ya kwanza ya sura hii, tunaambiwa kwamba hiki kifungu ama sura hii ndio nguzo ya demokrasia ambayo Jamhuri ya Kenya itafuata. Na yafaa tuelewe ya kwamba haki zetu za kibinadamu ni za mwananchi hazitoki kwa serikali ama kwa nchi lakini ni za mwananchi mwenyewe. Na serikali imepewa jukumu la kuimarisha na kukuza haki hizi. Katika sehemu hii tutaona ya kwamba tumebuniwa Tume ya haki za binaadamu na pia mahakama imepewa nguvu ya kufafanua Katiba hii kwa mujibu wa kupata manufaa zaidi kuhusu haki za binaadamu.

Yafaa pia tuelewe kwamba haki hizi zitapunguzwa tu kwa mujibu wa sheria hii, they are not a (inaudible) they can be limited by the Constitution itself. Sasa tuangalie haki ambazo ziko katika sura hii. Kwanza ni haki ya uhai, na katika haki hii hukumu ya kifo inatupiliwa mbali, pia kuna haki ya usawa ama equality, persons, kila mwanadamu katika nchi ya Kenya ni sawa. Pia kuna haki ya kutobaguliwa kwa misingi mbali mbali, msingi wenye njia, msingi wa kifamilia, msingi wa tabaka, rangi, umri, ulemavu, dini, mawazo yetu, lugha ama kuzaliwa. Hivyo hakuna mwana Kenya atakaye baguliwa kwa njia hiyo.

Wanawake pia wamepewa katika sehemu hii, kifungu hiki kinasema kwamba wanawake na wanaume ni sawa, na kila mwanamke atanufaika kwa haki sawa kama mwanadamu yeyote yule, mila na desturi ambazo zinawabagua wanawake katika jamii, zinatupiliwa mbali. Wakongwe katika jamii pia wako na haki fulani fulani, wako na haki ya kuwa huru, ya kufanya maswala yao bila kuingiliwa kwa upande wowote na pia watapewa heshima na maslahi yao yataangaliwa na jamii. Watoto pia wamepewa haki katika Katiba hii na yafaa tuelewa kwamba, tukisema watoto ni watoto ambao wamezaliwa katika ndoa ama

nje ya ndoa.

Haki za watoto katika kifungu hiki, kifungu cha 37. Haki hizi ni kama haki ya kupata uraia, haki ya malezi, haki ya kupata elimu na yafaa tuelewa kwamba elimu ya msingi itakuwa ya bure. Pia watakuwa na haki ya kutobaguliwa, hawatalazimishwa kufanya kazi, watapewa makao, chakula, afya na matakwa mengine ya kimsingi. Kuchapwa kwa watoto na viboko haswa shuleni pia imetupiliwa mbali, watoto hawatasajiliwa katika jeshi, watoto pia hawatashikwa na kuwekwa pamoja na wanadamu wazima katika korokoroni. Na iwapo watashikwa watapewa mtetezi, watapewa wakili wa kuwatetea.

Yafaa tuelewe tukisema mtoto katika Katiba hii tunamaanisha mtu ambaye ako chini ya umri wa miaka kumi na nane, samahani. Kwanza katika Katiba ya sasa hakuna ufafanuzi wa mtoto ni nani, lakini ufafanuzi huo uko katika sheria ya Bunge, lakini Katiba hii inafafanua mtoto ni nani. Pia familia iko na haki fulani, kila familia itapewa heshima na kila mwanakenya ambaye amefikisha miaka kumi na nane na zaidi atakuwa na haki ya kuoa.

Kila mwanakenya atakuwa na haki ya kuanzisha familia na Bunge itapitisha sheria fulani, fulani kuhusu maswala ya ndoa. Walemavu pia wamepewa haki fulani katika Katiba, haki hizi ni kama watakuwa sawa na binaadamu yeyote yule, watapewa elimu na katika vyombo vya usafiri hasa magari yatatengenezwa kwa njia ambayo itawezesha walemavu kuvitumia vyombo hivi kwa njia iliyo sawa.

Utu wa kila mwanakenya utaheshimika, ama human dignity. Kila mwanakenya atakuwa na haki ya ulinzi, pia mwanakenya amepewa haki ya kutokuwa mtumwa, na haki ya kutofanya kazi ya lazima.

Katika kifungu cha arobaini na tatu, kinapeana haki ya siri. Haki hii inahusu siri ya kimwili, hakuna mwanakenya ambaye atakaguliwa kwa siri ama kwa mali yake ila tu kwa mujibu wa sheria. Pia kuna haki ya dini na haki ya kuwa na maoni fulani. Kila mwanakenya atakuwa na haki ya kujiunga na dini atayependa na pia atakuwa na haki ya kuwa na maoni fulani.

Uhuru wa kujieleza pia unatambuliwa katika Katiba hii, uhuru huu uko katika kifungu cha arobaini na tano. Vyombo vya habari vimepewa uhuru wa kufanya mambo yao bila ya kusumbuliwa ama freedom of press, haki hii ya kujieleza imepewa wanasayansi ambao wanafanya utafiti, watakuwa na haki ya kutoa utafiti wao kwa umma bila kusumbuliwa.

Kila mwananchi pia atakuwa na haki ya kupata habari zozote zile, kifungu hiki kinampatia mwananchi kupata habari hata zile ambazo hapo awali zilikuwa siri- the freedom to access information. Mwanakenya pia amepewa haki ya kujumuika na vikundi mbali mbali, freedom of association, unaweza kujiunga na vikundi mbali mbali. Mwanakenya pia amepewa haki ya kuandamana na haki ya kufanya migomo.

Kila mwanakenya pia amepewa haki ya kujiunga na chama chochote cha kisiasa bila kubuni chama cha kisiasa mradi tu yale

mapendekezo ambayo yapo katika sheria tofauti tofauti yawe yanafuatwa. Kila mwanakenya pia amepewa haki ya kutembea katika sehemu yeyote ile katika Jamhuri ya Kenya bila kusumbuliwa.

Wakimbizi pia wamepewa haki fulani katika Katiba hii na Bunge limepewa mwaka mmoja kupitisha sheria ambazo zitawatenga wakimbizi. Pia kila mwanakenya amepewa haki ya kutekeleza taaluma yake bila kusumbuliwa. Kila mwanakenya pia ako na uhuru wa kumiliki mali, mali hii mradi tu imepatwa kwa njia iliyo sawa, italindwa lakini wale ambao wamejipatia mali kwa njia ya ufisadi watakaguliwa.

Kila mwanakenya pia amepewa haki ya kujiunga na vyama vya wafanyikazi, wanaweza kubuni vyama vya wafanyikazi ama kushiriki katika maswala ya vyama vya wafanyikazi. Wastaafu pia wamepewa haki fulani, social security. Katiba hii pia imetambuwa haki ya afya,elimu, imesema kwamba elimu ya msingi itakuwa bure. Makao sasa pia ni haki ya kila mwanakenya.

Chakula, maji, usafi, mazingara, lugha, tamaduni ni haki ambazo kila mwanakenya pia amepewa. Wanunuzi pia wamepewa haki fulani fulani kulingana ama kutokana na bidhaa, kila mwanakenya sasa analindwa kutokana na bidhaa ambazo ni hafifu.

Kila mwanakenya pia ako na haki ya kunufaika na utawala bora, fair administration. Mwanakenya hatalazimika kufuata masharti ambayo sio ya halali, obeying unlawful instructions. Kila mwanakenya pia atakuwa na haki ya kuwasilisha malalamishi yake mbele ya mahakama bila kusumbuliwa.

Watu ambao wako korokoroni, wako na haki fulani pia watakuwa na haki ya kukimya katika mahakama, watakuwa na haki ya kuwasilishwa na wakili ambaye wanampenda na iwapo hawana uwezo wa kuajiri wakili, watapeana malalamishi yao kwa ofisi fulani ambayo iko katika Katiba hii ambayo itawapea huduma za wakili.

Watoto ambao wako korokoroni na wale ambao wako Jela, wako na haki Fulani, watapewa mafunzo fulani wakiwa korokoroni. Utu wao pia utaangaliwa, human dignity. Wakati wa hali ya hatari ama wakati wa emergency, kila mwanakenya atakuwa na haki fulani na Bunge limepewa uwezo wa kupitisha sheria fulani ambazo zitawezesha mwanakenya kunufaika ama kupata haki zao ama kulinda wanakenya dhidi ya matendo ambayo yanakiuka haki za kimsingi za Wakenya.

Katika kutekeleza haki hizi, kumebuniwa katika sura hii Tume ya haki, Tume hii pia itakuwa inachunguza maswala ya haki za kibinaadamu, itakuwa pia inachunguza ukiukaji wa haki za kibinaadamu na itakuwa inatoa repoti kwa Bunge. Katika ufafanuzi wa haki za kibinadamu, mahakama imepewa uwezo wa kufafanua mapendekezo kuhusu haki za binaadamu. Kwa ufupi tu hayo ndiyo mapendekezo ambayo yako katika sura hii.

**Com. Adagala**: Haya, vitu vilizungumuziwa zaidi vilikuwa hii Bill of Rights. Wananchi wa kawaida hasa walikuwa kwa hii,

kwa sababu maishani mwetu imekuwa shida, tunaenda upande huu, unajigonga kwa ukuta upande huu, unajigonga kwa ukuta upande huu, unaangamia kwa shimo upande ule mwingine unakanyaga kwa miiba. Hiyo ndiyo sasa tunatengeneza hivi iwe smooth na usawa, nafikiri pengine sitaingilia sana nitaona vile mtazungumzia, kwa sababu kila jamii ina mambo yao. Haya kujeni mbele wale wanataka kuzungumza.

**Esther Welangai**: Asante sana, mimi ninaitwa Esther Werengai. Mimi ninaonelea ya kwamba, for the parents who have separated and they both have children, the children must have a say in their mother's affairs. For example a mother has been away for many years and the children are in the home, they must decide if the mother is to come back in the home. This is thing is still... (inaudible).

**Com. Adagala**: Listen mama, mama African customary law is part of the … okay, na hiyo sasa si haki ya mama ni haki ya watoto. Watoto wana haki hiyo lakini aandika kijana.

**Cllr. Nalinyanya**: Mimi nina mapendekezo mawili, moja ni kuhusu mtu unaweza kutafuta mali yako, ukipata shida, ukishapata hiyo mali, wakora wanakuja wanakukata kata ili wachukue hiyo mali. Kwangu ninge-suggest kwamba, mtu ambaye amemkata kata mwingine kwa kumnyang'anya mali yake kwa nguvu, huyo angeliuawa. Hiyo ingebaki hapo kusudi watu waogope.

Ya pili nikuhusu NSSF, tuna wazee ambao labda hawakuajiriwa kazi na wamekuwa tu wakulima na amefika miaka hamsini tano na sasa anaelekea hawezi kulima tena na hana malipo mahali popote. Mtu kama huyo akishafika miaka sitini, ningependekeza kwamba, serikali ama hii Constitution iamuru serikali kulinda mtu kama huyu ili apate chakula chake, mtu hana nguvu ya kulima.

**Com. Adagala**: Vitu viwili na hiyvo viwili vinaambatana pia na African customary law. Haya hapa kwa Katiba hiyo ya kwanza kuuawa, watu wengi isipokuwa Waislamu wa North Eastern, hiyo mambo ya kuua mtu hata kama mumefanya hatia si ya mila yenu. Ninawaambia vile walisema, walisema death sentence is repugnant, tukiweka kwa lugha ya lawyer, wanasema si ya mila yetu, hatutaki na watu walisema afungwe kifo lakini kwa mila yetu tulikuwa tunamfukuza aende mbali. Sasa vile wamesema kifo, Councillor njoo hapa umalize vitu vyako. Kifo hakiko kwa mila yetu, sijui kwa nini, hata sikutarajia watasema hivyo, lakini tulichukuwa hiyo mambo ya majority ikatoka hiyo death sentence ikawa repugnant, so it is difficult for now us to put it.

Nilifikiri wale wasomi walienda ng'ambo ndio watasema hilo jambo, lakini ikatokea wananchi ndio walisema hiyo haiko kwa mila yetu, na tulitoa maoni kwa nchi. Sasa pia tulikuwa na hiyo maoni lakini tuseme ilikaa upande huu na ikawa kitu kama kile cha wachache. Sasa hiyo ni ya kwanza swali la pili lilikuwa nini?

**Cllr. Nalinyanya:** Ilikuwa kuhusu wazee.

**Speaker:** (inaudible)

**Com. Adagala**: Hiyo iko hapa na ninataka kufafanua hapo vizuri kwa sababu pia ni mila yetu na ni kibinaadamu. Inasema family and state will take care of the elderly, ili tusiwe kama nchi zingine, wanajenga nyumba na wana-weka huko wazee, sasa hata watoto wako wakizaliwa hawajui wana babu au guka. Wanakaa huko peke yao na huyo nyanya anakosa. Na pia state ifanye hivyo, kitu kinaitwa state, ukiambia state take this elderly people, take care of them, they will say alright, they will build a house for them and put them there and there will be nurses to take care of them. It is true, mzee ambaye hakuwa na kazi, hawa wengine wana pension na wale waliajiriwa, lakini huyu mzee alipokuwa analima alikuwa analinda familia. Sasa hapa wamesema familia na state watalinda, hakuna kitu cha kuelewa, hiyo ingine itakuwa ya Parliament the law.

Familia na state. Wale ambao hawana nguvu za kulima au kufanya ile kazi walikuwa wakifanya na hawakuwa wameajiriwa pia watalindwa, na watalindwa na state na family. Na watu walituambia hivyo. Kuna watu walisema tu vile unasema, kuna watu ambao hawakuajiriwa na wote tunasema state and family vile watu walisema.

**Cllr. Nalinyanya:** Tukisema hivyo tuna baadhi ya waze hata wameelemisha watoto wao, wamepata kazi lakini hawataki kuwalinda. Suggestion yangu ni kwamba, mzee kama huyo afunguliwe account pesa zikitoka huko yeye mwenyewe awe anaenda kuchukua na kujisaidia nazo badala ya kumjengea nyumba awe …

**Com. Adagala**: Hakuna mtoto atakataa kulinda mzazi.
**Interjections:** (inaudible)

**Com. Adagala**: Watu wa Matete wacha niwaambie, mnasikia, tulipata hiyo hasa upande wa Ujaluo. Iko kwa Katiba itakuwa kwa sheria, kama iko kwa Katiba-huyo mzee anazungumza na sauti nzito nzito- kama iko kwa Katiba itatekelezwa. Akikosa anavunja Katiba, atapelekwa korokoroni, very simple matter. Ana sehemu yake hata hiyo pesa inatoka kwa state haiwezi kuwa ile ya kudhaminia maisha yote, hata ikitoka pesa ya state, hiyo pesa haitampenda mzee, haitamtoa hapa na kumpeleka pale. Baba yangu alikuwa mzee mkongwe na alifariki juzi, vile niliona hiyo siwezi kusema ni shida. Kwa sababu sote tulipenda kumlinda lakini inatokea wengine wana… lakini ni kazi ngumu, lakini familia lazima ilinde. Huenda pesa itawekwa kwa account, mzee hata hawezi kwenda kuchukua, itakuaje? Hana nguvu ya kuenda, huenda pesa ikaletwa halafu watoto waseme ana pesa zake, na wamuache kando, itakuaje?

Familia na state watachunga wakongwe na hata ilikuwa na umri na Parliament wataweka hiyo, ukifika umri fulani utalindwa sehemu hii na state na sehemu hii na familia. Na wale ambao wanakataa itakuwa koti, kwa sababu koti ndiyo inalinda Katiba, endelea.

**Opanda Wamalika**: Mimi nina mapendekezo mawili. Jina ni Opanda Wamalika. Pendekezo la kwanza linahusu section 35 ambayo inasema ya kwamba, wanawake watapewa usawa katika mambo yote na wanaume. Ninaona ya kwamba it is not

exhaustive na ningependa Constitution iseme ya kwamba, that the equality between men and women is based on the fact that both belong to the human race, however because of women;s special marital role and also because we regard them as weak sex, to that extent they are not equal and therefore they should be accorded special treatment for example, being given 30% representation in Parliament. Otherwise if we can give them 30% representation in Parliament then we are implying that they are not equal. So if they are equal, why can't they be left to fight for their own? That is the first, nimesema pendekezo langu.

Two, na huko mbele katika hii Bill of Rights inasema ya kwamba, serikali ina jukumu to divulge information to the public for public scrutiny. Ninaona ya kwamba, this should be limited for the crucial reason kwa sababu ikiwa serikali inatoa every information regarding the running of the government, you never know somebody can take advantage and use it for clandestine activities. Kwa hivyo lazima tuwe na siri ambayo inaweza kupelekwa kwa umma na siri ambayo inaweza kukaa kwa serikali, asante.

**Com. Adagala**: Hiyo ya kwanza, kuna kasumba fulani kuhusu wanawake uko nayo. Hiki kifungo kinakuwa hivyo, wanaume ambao wana kasumba wanasumbua wanawake, wanafanya hivi wanafanyi hivi, ili hiyo one third itolewe. Itakuweko, ni kitu tume find kimaitaifa, it is part of the law of Kenya kwa sababu we find it in affirmative action. Affirmative action inakuweko, hiyo theluthi moja, one-third inakuweko for a time because the culture weakens women. Women are not weak by nature, they are very strong, if they are not strong, you wouldn't give/leave them all the work that they do.

You wouldn't leave them all the hard child bearing that they do, they are very strong but it is (inaudible) marital status, the culture makes it like that. So what is needed here, ni kuinua ili basi huo usawa utatoka. Na affirmative action ni kwa muda tu halafu inatolewa.

Ya pili, hiyo ilikuwa ya information, hiyo ni ya Parliament na Parliament watachagua ile itakuwa state secrets of secrets defence are not to be divulged.for instance, okay? Sasa Parliament watatengeneza hiyo Act, lakini nimekutana na wanaume wengi sana kama wewe, unaonekana kama unaunga wanawake mkono lakini unatoa ile inawasaidia, chunga. Think of your daughter, don't think of your wife because I know ni *musigo*, a wife is *numusigo*, a wife is numusigo isn't?

**Audience**: Yeah

**Com. Adagala**: Think of your daughter.

**Wakith Muchenye**: Kwa majina ni Wakith Muchenye na niko na mapendekezo matatu tu. Pendekezo langu, wameongea zaidi na mimi ninaongea kulingana na walemavu, wametudharau sana, katika Parliament hatuko, katika ma diwani hatuko. Na sisi walemavu tunapiga mpira kabisa, tunapitisha wabunge wazima miguu, lakini sisi tukiitisha, wanasema hatutaki kusaidia mtu mwingine juu.

**Com. Adagala**: Haya pendekezo?

**Wakith Muchenye**: Pendekezo langu ninasema kwamba, inatakikana mwaka huu, kura hii vile Katiba hii itaendelea tunataka viwete pia tukanyange Parliament.

**Com. Adagala**: Kwanza association of disabled people ni ile people with disability wametuambia, tusiite watu kiwete na walemavu kwa sababu hiyo sasa ni kama kikombe na vikombe, sasa wewe mwenyewe utajirekebisha ili usitumie vipofu, vi-nini. Ni walemavu ambao wana ulemavu wa shida nyingi, okay? Utajirekebisha kwa lugha.

Ya pili, nimeona Nyanza ilikuwa kwa Television huko Nyanza Province, walemavu walikuwa na mkutano wao na wao wote walikuwa hapo kwenye siasa na wakajitokeza watagombania Bunge, udiwani lakini walemavu, wote tuliwaita walemavu pia, kama tulifanya na the late Ombaka Ombaka was better than the whole Commission put together mtu ambaye hana macho, infact alikuwa na super ability, alikuwa na nguvu sana. Sisemi hakuna shida, kulikuwa na shida mingi, kweli hata yeye kutembea hatua mbili tatu lakini ya hapa na ability alikuwa na nyingi sana.

Ya tatu, nataka hapa iwe, ulisema siasa, kuna Josephine Sinyo ako kwa Bunge, nataka mkisema, mseme mambo ya kweli na ya haki, Okay? Josehpne Sinyo haoni hata tulikuwa na DC ambaye hatembei, na ulemavu pia ni kitu ambacho kina degree.

**Audience**: Hata Wamea alikuwa huko.

**Com. Adagala**: Wamea alikuwa huko, unaona, tafadhali mjifungulie milango, hata Mungu anasema ukibisha, itafunguka. So ni mzuri unabisha lakini urekebisha lugha na facts of life. Pia unaweza kusimama lakini hata hivyo… Excuse me watoto wa Matete mna kelele, mna kelele kupindukia, I have not heard this problem in other venues. Kama mnaona mnajua zaidi, bila nyinyi, nitapata sitting allowance yangu na nitaenda, nimeshaketi. Tafadhali, you will make my job difficult for me and I will make the submissions kuwa fupi. Sasa sitaruhusu watu, laini.

The other thing I was going to say is that walemavu, ile ungetuambia ni walemavu wako 15% ya nchi, unajua hiyo?

**Wakith Muchenye:** Ninajua.

**Com. Adagala**: 15% wapate nafasi ya 15%, hiyo ndiyo ungesema okay? Lakini ubaya upande wa culture… Usilete soda tafadhali. Nani, mfungulie soda zote nje kwa sababu zinafanya kelele sana, muache huko hiyvo vipekee vipekee. Ile nataka kukuambaia iko hapa, 15%. Hata Anjere Chairman wa (inaudible) amesema hiyo iko hapa, ubaya ni utamaduni. Nani hana jamii hata mmoja mlemavu hapa, weka mkono juu? Mumewaacha wapi? Nyumba, sivyo mwenzangu?

**Wakith Mukenye**: Ndiyo.

**Com. Adagala**: Culture ndio inafunga watu, okay? Ni vibaya.

**Wakith Mukenya**: Sasa nilisema point yangu, ilikuwa mapendekezo matatu. Halafu kuongezea wamama ndio wanatuzaa, muhula huu, pia vile nilisema lazima mama pia nao wakanyage Parliament na nominated Councillors. Halafu nyingine, mashamba kama baba amekufa, koti irekebishe mambo ya kustaki kaburi inatusumbua sisi wengine ambao hawana pesa.

**Com. Adagala**: Kwa vile watu hawataki kukaa kimya, mtaketi chini na nitaendelea. Watu wa kubali kukimya, soda hiyo isilete kelele, mama stop. Kama hiyo soda italete kelele na kama watu hawatakaa kimya sita-ruhusu distraction, nita-present tu mfululizo, tufunge virago tuende. Kama mnataka mshiriki mtu mmoja peke ndio anazungumza. Mumekubali?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Adagala**: Haya wewe na jirani yako mjichunge.

**Jackson Nalika**: Kwa majina najulikana kama Jackson Nalika, nilikuwa na mapendekezo mawili lakini moja nasikia umegusia. Pendekezo langu ni kusema ya kwamba nilisikia kijana akisoma habari ya watoto na wazee. Watoto walipewa muda wa miaka kumi na nane, akifika miaka kumi na nane ametoka kwa utoto, na wazee ningependekeza ya kwamba, nao wakifika miaka fulani iwe ameingia kwa uzuri. Iwe ameingia uzuri na hiyo ni kuwa umefikisha (inaudible).

**Com. Adagala**: (inaudible) sema mwaka ngapi.

**Jackson Nalika**: Mimi ninaonelea mzee akifika miaka sitini,
**Interjections.**

**Com. Adagala:** Nataka kumaliza hii kitu niende kwa sababu hawa watu hawataki kuheshimu mtu akizungumza, utapata nafasi yako.

**Jackson Nalika**: Mimi ninaona miaka hamsini na tano ni ile nimepewa na serikali awe retired na akiwa retired aje nyumbani, atajisaidia kwa miaka mitano, akifika miaka sitini, ihisabiwe ya kwamba sasa huyo amekuwa mkongwe alindwe na state. Neno la pili…

**Com. Adagala**: Na watoto je?
**Jackson Nalika:** Si huwa tuna watoto, si mzee amelinda watoto, wewe sasa mama hivi, ..

**Com. Adagala**: Mzee kwa nini alindwe na state, na family imeenda wapi?

**Jackson Nalika**: Mimi ninasema wewe kama (inaudible) hata wewe vile ume …

**Com. Adagala**: Nataka kujua familia imeendwa wapi?
**Jackson Nalika**: Familia iko chini yake.

**Com. Adagala**: Sasa mzee ..
**Jackson Nalika**: Familia yake iko inashirikiana ndio lakini state naye iweze …

**Com. Adagala**: Kuwaangalia.
**Jackson Nalika**: Eh, hapo ninasema hivyo. Halafu neno la pili ni neno la korokoroni. Ninapendekeza ya kwamba, watu wengi sana hata mkikosana na askari mambo mengine,..

**Com. Adagala**: Hatujafika kwa hiyo.
**Jackson Nalika**: Ulikuwa umeongea korokoroni hapa,

**Com. Adagala**: Hatujafika kwa hiyo ninakuambia ya kweli
**Jackson Nalika**: Okay, sawa.

**Christopher Musamali**: Mimi kwa majina ni Christopher Musamali, neno ambalo limekuwa… ..
**Com. Adagala**: Tunataka tu pendekezo lako.

**Christopher Musamali**: Pendekezo langu ni kwamba, mtoto akizaliwa hapa na baba wa ki luhya mama wa kikuyu, mtoto atakuwa wa hapa. Ni hiyo tu.

**Com. Adagala**: Mila za mama, Mkikuyu anasema mtoto ni wake, ukifunga ndoa mtafikiria.

**David Vududi**: Kwa jina ni David Vududi, pendekezo langu kwa vile nimesikia kuhusu mtoto mwanafunzi, hiyo kitu haingekuwa namna hiyo. Ninaonelea mtoto yeyote, hata mimi nilipigwa kiboko kwa shule ndio nikawa mwanafunzi shule. Na sasa mkisema ipitishwe mtoto asifunzwe kwa shule namna hiyo, mtakuwa mumepeleka mtoto kufundishwa ama namna gani?

**Com. Adagala**: Wakina nani wanasema? Wananchi walisema.
**David Vududi:** Nimesikia, wananchi ndio walisema, huyo mwananchi alikosea kidogo.

**Com. Adagala**: Walikuwa wengi na hata hivyo sheria hiyo iko kwa Childrens' Act 2001. Kuna njia nyingi za kurekebisha mtoto na sio kiboko na walimu wanajua na hata wazazi wanajua na inafaa tupelekane kama watu ambao wako kwa jamii bora.

Tunapiga watoto, mwishowe wakiwa violent kwako kwa election, tunasema hao watu wako violent na ulikuwa unampiga. Mtoto ukimpiga, atapiga mtu mwingine.

**Maikuva Shitanda**: Kwa majina Maikuva Shitanda, naongea juu ya Bill of Rights.
**Com. Adagala**: Pendekezo lako?

**Maikuva Shitanda**: Pendekezo langu kwanza kuhusu chakula.
**Com. Adagala**: Pendekezo?

**Maikuva Shitanda**: Pendekezo langu ni kwamba tuweke sheria ambayo italinda wananchi wa Kenya kutokana na vyakula ambavyo vinakuwa imported na wafanyi biashara ambavyo vina haribu agriculture hapa Kenya. Hasa sheria kuhusu liberalization of trade na hii maneno ya COMESA policy lazima irekebishwe ili wananchi wa Kenya waweze kuwa na chakula cha kutosha.

**Com. Adagala**: (inaudible)
**Maikuva Shitanda**: Pendekezo la pili ni kuhusu freedom of trade, na hii nitagusia kidogo mahali Mheshimiwa Werengai alisema, yule mwananchi ambaye ako na dual citizenship ama ana biashara nje ya Kenya.

**Com. Adagala**: Pendekezo lako?
**Maikuva Shitanda:** Pendekezo langu ni kwamba, mwananchi wa Kenya ambaye anataka kuwa na biashara nje, serikali yetu kupitia kwa sisi, tuwe na Tume ambayo itakuwa ina-lent wale watu wanataka kufanya biashara nje, tujue biashara gani hiyo anataka kufanya nje ya Kenya ambayo hawezi kufanya hapa vile nchi zingine mtu akitaka kuja hapa Kenya anakuja mpaka kwa investment promotion center to access or know whether this man is a serious business man.

**Samuel Sifuna**: Majina ni Samuel Sifuna, nina mapendekezo mawili. Moja inahusu watoto ambao wanazaliwa nje ya ndoa, kuna wengine mama yao aliolewa, akazaa watoto na akawaacha ama wakafukuzwa. Ningependekeza ya kwamba watoto kama hao wawe wanahudumiwa na yule mzazi ambaye ako ama mama wa kambo. Sasa kwa hizo dhuluma ningependekeza ya kwamba, angeshtakiwa kulingana na sheria ya watoto ili kama ni kufidia, hao watoto wafidiwe.

Halafu upande wa wamama, kuna sheria ambayo ni ya kwamba, mimi na mke wangu tukiachana ni lazima tugawane mali. Ningependekeza ya kwamba kama ni kugawana mali, tugawane ikiwa mimi nimemfukuza, lakini ikiwa amejifukuza mwenyewe, tusigawane na yeye mali. Ni hayo tu mawili asante.

**Com. Adagala**: Ngoja huku una kazi, ngoja huku kwanza. Unajua huyu mama kwa Katiba hii, atarithi mali yake kutoka kwa wazazi, sasa haitakuwa na hiyo kasumba ya wanaume, nyinyi ndio mna mali, huenda akawa na mali nyingi kuliko wewe.

Tumeandika lakini huenda akawa na mali nyingi kuliko wewe, sasa wewe ndio utahitaji akugawie kidogo.

**Shako Mark Ochira:** Kwa majina naitwa Shako Mark Ochira na pendekezo langu ni juu ya watoto. Ninapendekeza ya kwamba, ingekuwa ni vizuri serikali iweze kuchukua jukumu la kuelemisha watoto, kuanzia nursery, primary, secondary na university. Kwa sababu nimeona ya kwamba sio watu wote ambao ni sawa, wengine ni matajiri wengine ni masikini. Na tunaona ya kwamba, watoto wa masikini hawaendelei kwa sababu hawana pesa za kutosha.

**Com. Adagala**: Pendekeza?

**Shako Mark Ochira**: Ninapendekeza ya kwamba serikali iweze kuchukua jukumu lote la kufundisha watoto kuanzia pre-primary mpaka university na wafanyikazi ..

**Com. Adagala**: Wewe uko Form one, sisi tuko form two.

**Shako Mark Ochira**: Na wafanyikazi kutoka kiwango fulani wakatwe pesa kwa mishahara yao ya kusaidia hao watoto ambao hawawezi kuendelea mpaka university.

**Com. Adagala**: Mambo ya primary imeshawekwa, primary education iko hapa kwa Bill. Hiyo unatoa sasa, mzee sikiliza nilimwambia tulikuwa na maoni, were you here when hearings were going on? You are in Form one, we are in Form two now, okay? Zungumza mambo ya hapa, tuende mbele.

**Samuel Misiko**: Majina yangu ni Samuel Misiko, pendekezo ni kwamba, on the rights of property..kuna wale watoto ambao ni wa kiume na wa kike, kuna wale wa kike ambao pengine hawawezi kuolewa kwa sababu Fulani. Ninapendekeza ya kwamba yule ambaye anaweza kuolewa, asipate mali ya baba yake kama shamba.

**Com. Adagala**: You are in Form one bado.

**Samuel Misiko**: Okay, kama ni Form one, pengine nitarudia hilo somo lakini sasa limeisha. Pendekezo langu la pili ni kwamba, tuwe na rights of an individual, the state has to cater for the rights of an individual especially when we have meetings that have been called by the state, whereby those rights have to include even health and food. Kwa maana siku hizi utakuta ya kwamba, mkutano umeitwa na watu wamekuja saa mbili, na unatoka hapo saa kumi na mbili na hakuna muelekeo wowote kulinda maslahi yao. Kwa hivyo pendekezo langu ni kwamba, tuwe na proposal kwamba serikali ikiita mkutano hasa kabisa hata kama huu, ijali maslahi ya wale ambao wamekuja kuhudhuria huo mkutano sio tu wakati ambapo tuna siasa, tunakuja kwa siasa na watu ndio sasa wanajali maslahi ya watu. Nikimalizia ..

**Com. Adagala:** Pendekezo peke yake, bila maelezo.

**Samuel Misiko**: Pendekezo bila maelezo ni kwamba wakati tumesema ya kwamba wanaume…

**Com. Adagala**: I want a proposal from you, hakuna mtu unaelemisha hapa.

**Samuel Misiko:** Proposal on marriage, the Constitution has to specify who is marrying who because, when it comes to the Kenyan society ….

**Com. Adagala**: There many people who want to speak na mnaenda kwa maelezo mengi na hii ni dunia yetu tunaijua, okay? Na hilo swali la pili lilikuaje? Just tell me? What was it is about?

**Samuel Misiko**: Well, it is about marriage.
**Com. Adagala**: Okay, that is the last one.

**Samuel Misiko**: And I think we are going to…
**Com. Adagala**: Tell me the one before that?

**Samuel Misiko**: Ninapendekeza ya kwamba ..
**Com. Adagala**: Nataka uniambie tu ilikuwa kuhusu nini? Haya basi, ukikaa hivyo shauri yako. Marriage is understood in our society between men and women and hata Prof. Ghai alijibu hiyo kwa Radio on Sunday, watu wangapi wanasikiza Radio on Sunday 11? Na afternoon 2 – 3, Sunday KBC. Mtabaki nyuma, asubuhi kwa Kiswahili lakini nyinyi wengi ni wa Kristo msikilize in the afternoon okay? Next, pendekeza?
**Elphas Ngongo:** Jina langu ni Elphas Ngongo, Salvation Army Church leader. Napendekeza kwa ajili ya ….

**Com. Adagala**: Kama mumemaliza kuzungumza tunaweza kuendelea, nitasikiliza mkimaliza.

**Elphas Ngongo**: Niliambiwa ningoje kelele iishe na nilikuwa nimesema …
**Com. Adagala**: Ngoja, hawajamaliza kuongea. Endeleeni tu,wewe na rafiki yako endeleeni kuzungumza ………

**Elphas Ngongo**: Nilikuwa nimesema jina langu ni Elphas Ngongo, Salvation Army Church leader, ninapendekeza kuhusu rights za mwananchi wa Kenya, hatungelikuwa na ma-squatter na hali wanakenya wengine wana mashamba makubwa, hayo mashamba ambayo mtu ana zaidi ya elfu, itolewe kisha ma-squatter wapewe mashamba.
**Com. Adagala**: Uko Form one. Wacha nikueleze mzee, we have, mzee niambie hadithi ya new wine na old wine, there is old wine and old wine skin, hiyo ni Katiba ya sasa. We have new wine in old wine skin, inafanya nini ikiwa hivyo? Inafanya aje kwa bibilia? Inapasuka. New wine in new wine skin is this, nataka mzungumzie new wine in new wine skin, kama haukuweko wakati wa hearing, tafadhali ujue tuko kwa hatua ya pili. Tuko new wine in new wine skin, okay? Tuelewane, nafikiri hapa watu ni Wakristo wengi sana,mnaelewa?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Adagala**: Tuendelee.

**Thomas Kasaya**: Jina ni Thomas Kasaya, natoa pendekezo kwa kifungo cha 59 kuhusu nyumba. Ningependekeza ya kuwa mahali mtu hajaweza kuwa na nyumba nzuri vile Katiba inavyopendekeza, iwekwe kifungu ambacho kitafanya serikali iwe na huo wajibu kutekeleza ikiwa huyo mtu hajafikiriwa.

Pendekezo lingine ni kifungo cha sitini kuhusu chakula. Kwa vile Katiba inasema ya kuwa inatakikana kila mtu awe na chakula asikumbwe na njaa, ningependekeza ya kuwa kwa vile serikali wakati mwingine ina-dharau sisi, huyo raia apewe uwezo wa kisheria for a legal reference mahali serikali inaweza kuwa compelled impe chakula.

Kifungo kingine ni kile cha 65 kuhusu utawala wa haki, Katiba inapendekeza kila raia kuwa na utawala wa haki na ningependekeza ya kuwa tuongeze kipengele kwa kile cha kwanza ili mahali haupokei utawala usio wa bora, uende kotini kutafuta kuondoa ule utawala usio bora, asante.

**Com. Adagala**: Njoo huku, simama hapa kwanza. I have just said new wine in new skin, new wine in new bottle. Kuna shida zilizungumziwa wakati wa hearings, tukaenda tukakusanya zote, tukaweka hapa, tukatengeneza proposal ya kuenda mbele. Kwa nini mnataka kurudi nyuma, kwa nini mnataka kurudi Misri. Kwa nini mnataka kurudi kwa utumwa, hivi vitu unasema, tuko kwa hii tuende mbele, mengi umesema ni hiyo ya kurudi nyuma, lakini kile ninataka kukuambia, nyumba serikali inaweza kukujengea hata chakula inaweza kukupa. Serikali tumesema itasomesha watoto, mjue state ni kitu gani, state si kitu cha mchezo. State imesema hapa, wananchi walisema tunataka free education, na wakasema okay free primary education, iko hapa, mumekubali nayo?

**Audience:** Yeah.

**Com. Adagala**: Mmeipenda?

**Audience**: Sana.

**Com. Adagala:** Halafu inasema watoto wasipigwe viboko. Serikali ikikupa kitu pia inafuata, watu wengine walikuwa wanasema, sheria itoe ushuru kwa kanisa, sawa lazima watakuambia utahubiri nini. Uelewe, serikali ikitoa nyumba, itakuwa na masharti, hapo muielewe. Serikali ikitunza wazee vikongwe itakuwa na masharti hapo ndio mnaona mnachukua tu rights, hakuna mtu amesema responsibilities. Responsibilities ya wananchi ni nini, iko rights na responsibilities, freedom okay? Nataka tusonge mbele sitaki kurudi nyuma.

**Alphayo Musungu**: Kwa majina naitwa Alphayo Musungu. Pendekezo langu liko kwa pensioners. Ikiwa watu wa pension ambao wali-retire zamani kama sisi, kama ni grade 1 ama P1 na anapata nini ya chini sasa, kwa sababu alikuwa mbali wakati

wengine wame-retire kama sasa na wako grade one, ni heri pension yako iongezwe ikuwe pamoja na wale kwa sababu wako kwa grade moja.

Neno la pili, employment. Watoto wengi wamesoma na hawana kazi, tunapendekeza ya kwamba wale watoto wamemaliza shule ni heri wawe registered kwa chief na halafu wa forward yale majina katika district. Employment ikifika, waje wapewe pahali chief wao yuko na wawe selected hapo. Kwa sababu mara nyinyi wakienda kama Kakamega, wengi hawapati, unaona tu family moja ndio inaandikwa na ingine hapana. Neno la mwisho, wakulima wakishalima chakula ..

**Com. Adagala**: Pendekezo.

**Alphayo Mzungu**: Pendekezo, tunataka waelimike na serikali ipange bei mapema ili wakilima wajue cost ni nini kwa sababu mara nyingi wakulima hupata hasara. Yangu ni hayo tu.

**Gladys Sirisia:** Yangu ni maoni kuhusu afya. Mimi ni Gladys Sirisia. Mimi ningeonelea hivi, wamesema ya kwamba tuwe na cost sharing katika hospitali lakini tunaona ya kwamba tukienda hospitali ..

**Com. Adagala**: Tunataka pendekezo mama?

**Gladys Sirisia**: Tunataka ya kwamba serikali ..

**Com. Adagala**: Wewe na mimi tunaenda hospitali, tunajua nini inatendeka huko, wewe pendekeza, utupe nuru zaidi.

**Gladys Sirisia**: Pendekezo tunataka serikali itusaidie hii cost sharing na madawa ipatikane hospitali.

**Com. Adagala**: (inaudible)…..tulisema nini kuhusu Afya, nataka ukija uketi hapa, uzungumze mambo ambayo tumezungumzia Werengai tulisema nini kuhusu afya?

**Werengai:** (inaudible)

**Com. Adagala:** Tunasema kwa Kiswahili kwa sababu watu wote wasikie okay endeleeni.

**Joseph Wabosya:** Kwa majina ninaitwa Joseph Wabosya, pendekezo langu ni haki na huru. Unapokosewa ukienda usaidiwe kama hauna chochote unadhulumiwa halafu mwenye amekukosea anazidi kukosa.

**Com. Adagala**: Ulisikia huyu kijana alieleza nini? You are not listening, kwa nini hamtaki kusikia? Kwa sababu unazungumza na jirani yako. Huyu kijana amesema hayo. Na mambo ya kudhulimiwa yako hapa, mambo ya kutokuwa na uwezo yako hapa, lakini hamsikii.

**Interjections:** People want them to be repeated.

**Com. Adagala**: Hiyo ni Form one, are people really interested? No, hiyo ni kubaguliwa, that is what they do and then they (inaudible). Tunataka kuwe na nia ya kuketi hapa kama ulikuja hapa kuzungumza na jirani ambaye umeketi naye, utuambie

tujue. Tunaeleza mambo, mambo muhimu, mambo ambayo yatatengeneza Kenya iwe Kenya mpya na kama hauyajui, utakuwa na shida nyingi sana, na wale ambao hawajakuja watakuwa na shida nyingi sana. Mchukue nafasi hii iwe special day ambayo haitatendeka tena kwa miaka mia moja, nina-muahidi hiyo.

Kurekebisha Katika haitafanyika kila every other day na this is not Chief's Baraza. I want to let you know that hiki ni Kikao cha Tume ya Kurekebisha Katiba, tuko na very serious work, kama hauko serious kindly step outside. Na sijakuwa na shida hii, tumekuwa huko Vihiga nini, hatujakuwa na shida hivi. Unaambia watu mara mbili mara tatu wanaheshimu lakini nyinyi mnataka kuzungumza hamjui, ninaweza kukatiza hii mambo na mtakuwa mumepungukiwa na hamta …. Haya, nataka tuchukuwe break, mumekunywa soda?

**Audience:** eeh.

**Com. Adagala**: Nataka tuchukuwe break tuzungumzie mambo yale tungezungumzia mwanzo lakini watu hawakuwa wengi, tukaona tukizungumza itakuwa inaenda kwa benches. Haya, si kuna nia ya kuwa hapa. This day, siku hii haitakuweko tena, tutakuwa na ingine pengine ya referendum, ingine ya kurekebisha kitu kidogo na hii siku haitakuweko tena, okay? Nataka muelewe hivyo, ndio iko muhimu sana. Tulichukuwa maoni yenu tukaweka pamoja, tukachanganyisha na ya wengine ndio tumekuja na maoni haya, na haikuwa kazi rahisi, huyu mama Mwangi, yeye ndio mkubwa wa idara ya Verbatim, neno kwa neno anaandika.

Watu wake wote wako kila mahali walikuwa wanachukuwa neno kwa neno, hapa anaandika kila kitu tunasema hapa, hata nikisema, 'please keep quiet,' okay? Yeye hiyo ni ujuzi alitoa kwa Parliament, idara yake ilikuwa ikifanya kazi 24 hours a day shift. Walikuwa wanatoa maoni yenu kwa tape wanaandika kwa computer, wengine wanakagua iko sawa au la? Halafu tukatengeneza ripoti ya hapa, na tutampea hiyo repoti ili mjue mkague muanglie kama mambo mlisema yako hapo au la, okay?

Tumekuwa na hatua fulani, tumekuwa na Act iliandikwa na Parliament kwa sababu watu wengi walitaka hii Katiba ibadilishwe kwa sababu haikujulikana pengine iliundwa kwa Kiingereza kigumu, ndio Public Law Institute ikajaribu ikaweka pocket Constitution kwa Kiingereza na Kiswahili kidogo, ile wangeweza na watu hawakuijua. Tulikuwa tunaishi kama watu ambao hawakai kwa ki-Katiba, hata ninyi hapa ndio mumeona ndio imeandikwa mambo ya uKatiba. Bill of rights, Constitutionalism, hii ndio Bill of Rights hapa kuliko ingine.

Tulitaka wananchi wenyewe wajue Katiba yao na waitengeneze wenyewe kwa sababu hii ingine ilitengenezwa Uingereza. Watu walienda wachache na hata inasemekana inaonekana wengine walizungumza na wengine hawakuzungumza sana, inaonekana kwa Hansard. Na mtu mwingine alituambia hivyo lakini walituwakilisha na wakataka uhuru hata walikuwa wanaambiwa mambo yoyote wanasema tu alright, alright lakini tunataka uhuru, tukapata uhuru. Na walipokuwa wamekosana mambo ya majimbo, wakaambiwa mkienda kubishana namna hii hamtapata uhuru lazima msikilizane, wakasema all right nafikiri majimbo.

Wakafika hapa 1964, wakafungua hiyo Katiba amendment ikianza mwaka wa 1969 kwa miaka arobaini. Na ya America imekaa 250 years na wana amendments kumi na tano. Lakini kwa vile ilikuwa inafunguliwa na pia vile ilikuweko bila vitu kama Preamble, Bill of Rights imewekwa huko nyuma kabisa. Hiyo pia ndio sababu ya kurekebisha. Katiba ya independence ile ya mwaka wa uhuru wa 1963 iko tofauti na ile iko sasa kwa sababu ilifunguliwa sana na Ooko Ombaka alikuwa anasema, hiyo Architecture yake iliharibika sana, mlango wamechukua wameweka huku nje, hapo wameziba hakuna madirisha, hiyo ndio kutoa uhuru hiyo. Wanaziba, hakuna madirisha kama hiyo unaweza kusema multy party, hauna madirisha mengi, ilikuwa tu dirisha moja basi hiyo ingine yote imezibwa.

Jikoni imewekwa kwa choo, hiyo nyumba ya kulala iko nje, paa ingine imewekwa huko, iko chini, hiyo ndio Katiba yetu ya sasa, iko mbaya sana. Hata mkasikia watu waki-ripoti ni mbaya sana.

Kitu kingine kiko kibovu sana kwa Katiba ni hicho kiti au Ofisi ya President. President alichukuwa na huyu alikuwa End of tape, word lost. There was no need to stand for election. Sasa hiyo ndiyo ilianza hii mambo na Kenyatta hakuwa na siku moja alisimama kwa kura, mnajua hivyo?

**Audience:** Yeah.

**Com. Adagala:** Yeah, sasa sio sisi tu, unaweza kuwa umependwa sana, basi inakuwa tu waendelee lakini hiyo ilitoweka halafu akachukua nguvu za Parliament akaweka kwa President, hizo za kuvunja Bunge na za kuchagua watu, akachukua akaweka hapo, huyo ni Kenyatta. Moi aliposema ninafuata nyayo, watu hawakuuliza walisema tu, eh ndio tunafuata nyayo, hawakuuliza ni nini. Sasa hatukutaka pia mseme tu Katiba Katiba, hawa vijana wakili wangeandika ten of them. Wangeandika Katiba kwa miezi miwili, iko tayari hata miwili ni nyingi sana, so it is like that. Pia hii ya Presidency ilichukuwa nguvu ya wananchi, ilipotoa hizo, Councillor anajua vizuri, Councillor anachaguliwa lakini hana kile cha kutengeneza, Councillor kweli au la? Local Authority, ndiyo mnasema lakini huyu Councillor tukimpigia, na ona hii barabara. Hana la kufanya hizo nguvu zilichukuliwa.

**Audience:** ………

**Com. Adagala:** Haya kuna ingine ya mahakama, mahakama pia (inaudible) Ukitaka kuwa judge lazima nijipendekeze kwa mtu fulani ambaye ana god-father fulani na yeye ananitetea Haya ukienda njia hiyo ukihukumu, utahukumu vizuri kweli?

**Audience:** Hapana

**Com. Adagala**: Utafikiria yule anasema nini. Sasa mahakama haina hiyo uhuru. Bunge pia vitu vingi vilitolewa kwa Bunge, na nyinyi mkatuambia hiki na hiki kirudi kwa Bunge. Appointment to top jobs, Bunge halafu Rais anakagua, anaangalia, anaweka sign, kitu kama hicho eh? Sasa hii ofisi ya Rais in ofisi ambayo mtu amepatiwa, ni vichwa sita. Ukizaa mtoto na vichwa sita, hata ngombe saa zingine wanazaa vichwa viwili au unasema eh, lakini hii sasa ni sita. Sasa tulisema chonga kidogo, chonga huku, chonga huku ndio tulifanya, tulifanya hiyo surgery, na tulifanya vile mlisema na ilikuwa reduce Presidential powers,

Presidential powers trim, Presidential powers limit, mlituambia, iko kwa submission zenu, okay?

Kitu kingine ni Provincial Administration. Provincial Administration ilivuka kutoka colonial days ikaja kwa uhuru. Provincial Administration in kitu cha ukoloni, mkatuambia Provincial Administration pia iko huko. Halafu ikawa hivyo na tukasema well, haiko kwa Katiba ya sasa kwa sababu ilivuka tu ikaja na ikatengenezwa na Provincial Administration kuna sehemu inachukua nafasi ya watu ambao wamechaguliwa. Inatekeleza kazi fulani na hiyo ni appointment.

Tukasema Chief akiwa appointed awe transferable lakini kama ako elected awe hapo hapo kwa sababu tume-mu-elect. Mkatuambia hiyo na ukisema hiyo kuhusu Chief, unajua sasa unasema hiyo familia yake yote ya Assistant chief na likuru, hiyo yote ni familia yake. Sasa hiyo ndio tuliangalia tukasema kweli haiko kwa nini, lakini hiyo pia ni kichwa kinaongezwa kwa nguvu za President.

Provincial Administration ina report kwa President, OP. Ukiangalia ofisi ya Chief imeandikwa Office of the President, sasa hiyo yote ndio ikafanya tukarekebisha haya mambo, tukawa na mengine madogo madogo lakini muhimu. Walemavu wakasema hatuko, tukasema okay, mtindo wa sasa lazima tufikirie walemavu wawe hapo. Wakina mama wakasema ubaguzi uko hapo, wakarekebisha kidogo kwa IPPG?? lakini tukasema wacha tukague tena vile watu wangependa.

Tukaangalia watoto wanasema, hata jina mtoto haliko kwa Katiba, isipokuwa wanazungumzia mambo ya divorce na nini. Lakini sisi watu kama watu wengine hapo pia. Sasa hiyo ndio tumefika kwa hii na vitu vingi vilitufanya tukarekebisha. Kabla, wananchi hawakujua na hata hiyo kurekebisha ilikuwa inafanyiwa Parliament na hamukuwa munajua kuna amendments au wametoa hiki wameweka hii. Nafikiri ile tulijua pekee ni ya multi party na ipi?

Hiyo ndio mliona vile imebadilisha Kenya. Believe me, niamini kitu kinaitwa Katiba kina nguvu, ikisema tutakuwa na chama kimoja, mtu mwingine akijaribu kuunda nyingine anaenda detention au korokoroni. Ikisema ni multi-party ukijaribu kuipunguza, kutakuwa na shida nyingi sana kwa sababu wamesema lazima iwe moja. Ndio tumeweka hapa kwa Katiba, Kenya shall be a multi-party state, imehifadhiwa hapa, haiwezi kubadilishwa isipokuwa wananchi wauulize tena vile tunamuuliza sasa na mlete hapa okay?

Hivyo ndio tumekuwa na tulikuja Kakamega tuka-launch process. Kwanza Commission ilitengenezwa, tuli-apply. Hii yetu ni ya Parliamentary, tulifanya application, haikuwa oh mtu anapenda mtu fulani, ilikuwa application tukaenda interview, tukakuwa short listed, tena interview, tukapata kazi. Na hiyo kazi tuliambiwa tufanye bila uoga au mapendeleo, tuliapa ndio mnaona tunaendelea hata mambo mengine ambayo haisemekani, tunasema, iwe ya mila, siasa au ya nini. Hakuna uoga, pia wewe ukija mbele ya Tume, haifai uwe na uoga, okay?

Sasa kitu ambacho kiko, Constitution ni kama tulikuwa constituted. Kwanza tulikuwa constituted kama colonial state, sasa

wakoloni, si wazungu ndio walikuwa na mambo yote?

**Audience:** Mmh.

**Com. Adagala:** Na sisi tulikuwa subjects, tulikuwa watu wa kufanya kazi na kutumwa huku na kule na kutoka kwa sehemu hii, wa Maasai ndio wanaijua yote. Wanasukumwa tu wanapelekwa kule, wazungu wanachukua mashamba. Haya hiyo ilikuwa colonial days, halafu tukatengeneza Republic lakini vile nimemwambia hiyo Jamhuri ilikuwa kama haiko na watu ndani, okay? Ndio tunatengeneza na kuunda sasa, na kama Katiba yetu kwa sababu watu walikuwa hawaijui ni kama unaweza kuchukua maji, uchukuwe kuni, sufuria uweke uji uwe na *mbango,* mnaitaje hiyo?

**Audience:** mugoo

**Com. Adagala**: Halafu unaanza kusonga mugoo, itaaiva kweli? Itaiva?

**Audience:** Hapana

**Com. Adagala**: Kwa sababu hakuna moto ndani na moto nguvu ni mwananchi. Mkijua ndio mnaweza kuendelea ndio tuko hapa na tunawaambia haya mambo yote ili isiwe tena mtu anasema sijui Katiba, okay? Ikiwa umemuacha mtu nyumbani, uende umueleze maisha inayokuja ni tofauti, ikifika wakati wa kura na umeacha mama na watoto nyumbani au mke au mume nyumbani, halafu anasema, "Ah situtapiga tu mlolongo, huku upande huu tumezoea mlolongo. Haitakuwa mlolongo kwa sababu hapa inasema secret ballot. Kura ya siri.

Sasa unaona huyu mtu sasa mtabishana all morning kwa sababu anasema, lakini mlolongo tutapiga, hiyo inafaa mjue, au mnasema Councillor na chief amekuwa hii na chief, itabidi mueleze, msikie hii mambo na ndio tunasema hii mambo mnaturudisha kwa Form one inafaa tuendelee mbele mshike ili ndio mtakuwa mnazungumzia.

Tulichukua maoni yenu na tulifurahi sana watu wengi walichangia na watu wakaja wakawa na maoni mazuri, kazi yetu ndio ilikuweko, msingelitupa maoni, tusingeliandika na vile mnaona kuna shida fulani fulani kwa maoni fulani. Hii ya mahakama wanasema wanataka sisi tuende jela kwa sababu tumezungumzia mambo yao, tumesema sawa Prof. Ghai amesema hiyo ni sawa, wanipeleke Kamiti Maximum kwa sababu nilizaliwa Ruiru, itakuwa karibu na nyumbani. Wengine tunasema sawa tutaenda korokoroni na tutafanya civic education huko kwa sababu wakenya wako huko pia na hatuko na uoga kwa sababu tuliapa hatutakuwa na uoga.

Sasa hiyo ya judges, ya mahakama hata hapa mlitoa maoni na mtaona kwa kitabu chenu cha hapa, na maoni hayo yalisema hivi, kuna shida nyingi na mahakama, kuna shida nyingi na judges, hata huyu alikuwa ameanza pia kutoa hiyo ya mahakama, wawili watatu, lakini tumeshapitia hapo. Tumechanga na maoni ya mahakama yaliyotolewa na wananchi pekee ni kurasa elfu moja mia nane, 1,800 pages, four reams of paper na yote ni negative. Hata kulikuwa na wengine walipendelea Provincial Administration wakasema lakini hiyo ni positive huyu ndio mwenyewe lakini hawa nao, ilikuwa hivyo kwa Provincial Administration. Lakini kile

kilitoka kwa mahakama, kila mkenya aliyezungumza alisema vitu vibaya, vingine vichafu sana kwa mahakama.

Niliwaambia kwa mkutano mwingine, ingekuwa wanajua mambo ya Judiciary, mahakama, vile wanajua Provincial Administration, wangesema transfer, wacha turudi kwa sheria ya kiafrika. Kwa sababu hii ingine imeleta shida sana, corruption, watu wanakuwa promoted wakiwa na god father, kwanza magistrates wako huko wanasema tu, "Eh, wacha hawa watu waende tupate kazi. Tumeketi kwa sababu hauna god father, hata ukifanya nini, hata iwe vizuri, hauwezi kuenda juu."

Sasa hiyo ni moja, ingine ni hii mambo ya ufisadi, rushwa. Mtu mwingine aliniambia hakuna mtu mmoja awe sweeper awe policeman, awe judge mkuu, awe judge gani, ambaye ame deal na case ya Pattni ambaye maisha yake imebaki hivyo. Mwezi moja tu na unaona amebadilika, nguo tofauti, mtoto aende shule ingine, gari inaingia, anabadilisha makao kwa sababu ya nini?
**Audience**: Corruption.

**Com. Adagala:** Kuna-kuwa na matajiri wengine wanaenda kwa judges, judge anaandika submission, anaandika vile lawyer anafaa amuambie halafu tajiri anachukua anampelekea lawyer anamwambia, ukisoma hii, nitakupa pesa fulani. Halafu anapelekea lawyer, lawyer akiwa mtu mfisadi anachukua anapata pesa pia yeye maisha yake inaendelea, pia huyo judge atapata lakini wengine wanakataa. Sasa judge akuandikie vile unafaa useme ili atoe judgment, hiyo ni kama kutoa mtihani kwa watoto wengine na wengine hautoi, eh? Haya hiyo ikawa hivyo.

Halafu tukazungumzia miaka yao, tukasema tufupishe judges wawe wana serve miaka 65 na kwa sasa tutazungumzia, na wale wako wakitaka kuendelea, akiwa miaka hamsini na tano kuendelea mbele, anaweza kustaafu na inakwishia hapo. Lakini akitaka kuendelea, basi kazi yake na maisha yake itakaguliwa, okay? Hiyo ni old bottles, old wine, ukitaka kuenda, unaenda halafu yako inakwishia hapo, lakini ukitaka kuendelea na service inaisha, ndio old bottle old wine.

Ukitaka kuendelea kwa hii new bottle, new wine, tutasema basi tutakukagua tuone kama unastahili, ninakwambia hata hizi kazi zingine za public service na hizi zote zitakuwa hivyo, zitakaguliwa, mali yako ulipata wapi, kazi yako ulikuwa unafanya vipi? Hiyo yote ulikuwa unachukuwa wananchi vipi? Ulikuwa na heshima kwao au la. Hiyo yote itakaguliwa halafu akiwa mzuri ataendelea lakini akiwa atapewa benefits akitaka kustaafu, wa kwanza huyo atapata benefits, lakini huyu sasa akikaguliwa na akipatwa na hatia, ataenda mahakamani na hivyo ndiyo tunataka iwe kwa sababu tunataka judges first, wale wanaheshima kwa wananchi, wale ambao wanatekeleza kazi yao bila rushwa, wale ambao wanafanya justice mzuri na wale ambao hawana upendeleo. Hiyo ndio public service itakuwa hivyo, haitakuwa hii kitu oh, huyo ni dada yangu na mtoto wa cousin wa my sister, na nini, my sister's husband, hiyo yote ni kupendelea, hiyo yote haiko. Mtu mwingine anaenda oh file imepotea, file imepotelea wapi?

Halafu unafikiria unasema kesi yangu, halafu unatoa, hiyo judges hawakutaka, hawakutaka tukague kazi na maisha yao, tutazungumzia zaidi. Tulichukua maoni yenu yote na tukaenda, hawa wakatoa hiyo report, kuna data mambo ya computer,

vijana wako huko, wakaweka kwa computer, ndio ninaambiwa hizo kurasa zilikuwa 1,800 kwa sababu yote ilikuwa, ile kuandika kidogo kwa computer ikatoka hiyo yote. Na pia tukachukua maoni yote, tukaenda Mombasa, mlisikia tuko Mombasa, wengine wakasema oh, wako huko wanaogelea.

Bahari ilikuwa kama hiyo gate na mimi sikukanyaga hata siku moja hapo, na sio mimi peke yangu. Siku moja tuliambia Prof. Ghai umechoka sana, wewe nenda utembee kwa bahari, na hakuwa amefika huko hata siku moja, akaenda akatembea kidogo, wacha hawa vijana wafanye hii kazi. Sasa akasema nitafanya nini, tukamwambia, nenda utembee kwa sababu hakuwa amefika huko. Tukaenda Mombasa na Mombasa tulifanya kazi, hata Vincent alikuweko, tulifanya kazi kamili na tulikuwa tunafanya usiku na mchana, hata watu wa Leisure Lodge walisema hatujawahi kuona watu wakifanya warsha kama hii.

Na hiyo haikuwa kazi nyingi, ilikuwa kujadiliana kwingi halafu tukawa na kitu, kwa sheria yetu inasema mjaribu sana kufika kila jambo lolote mjadiliane mpaka msikizane. Kwetu tunaita consensus, mnaita nini huku Werengai?

**Werengai:** (inaudible)

**Com. Adagala**: Hiyo Mluhya anafanya halafu anasema mmh zote? *Khuyamana, uhulizana* is another thing, khuyamana means, yes hii ndio tunakubali.

**Audience:** *Uhumia*.

**Com. Adagala**: *Uhumia* eh, hiyo pia iko kwa kikwetu, hiyo ndio tulikuwa nayo mwishowe. Ukiniambia mambo ya Katiba hii, hii tulizikizana tukapita hiyo consensus na tukaendelea, ilikuwa majadiliano. Sehemu zingine ilikuwa ngumu sana kwanza pengine ile ilikuwa rahisi ilikuwa bill of rights kwa hii Katiba, pahali pengine ilikuwa nyingi lakini tulisema wananchi walisema hiki na kile, na kuendelea.

Lakini hii nyingine ya serikali, na ya devolution ya kuleta nguvu chini, ya kufunbua hilo fumbo la urais na kuleta, tulikuwa na majadiliano sana mpaka usiku, asubuhi ukilala zaidi unapata wengine wanaendelea, sasa hakuna mtu alikuwa ana-miss. Isipokuwa wale wanne hawakuweka sign, kuna wengine hawakuweka sign kwa sababu hawakuweko na hawakufanya kazi.

Walikuwa wanafuata mambo ya mahakama, nimwambie wazi, walikuwa wameenda nyuma na kuzungumza na hao judges, wao ndio walikuwa wanapea information, ati tufanye hivi tufanye hivi, na hiyo .

**Audience**: Wasaliti hao.

**Com. Adagala**: Hiyo ndio mara ya kwanza kusikia wakiitwa wasaliti. Na hatukufurahia kwa sababu tulijua wenzetu wanafanya, hatukuwapa hiyo na haikuwa vizuri, sasa tulifanya na tukaleta hiyo ndio draft iko hapa, na pia hii ni draft. Tulitoa pia report, report ilikuwa, Co-ordinator ako wapi? Lazima iko kwa documentation center, sura yake ni hii, okay? Report yenyewe tuliona wananchi hii ni ngumu sana, report yenyewe iko four volumes, mara nne. Hiyo ndio full report, hii ni *mdondolo*

, lakini ni kamili vile iko.

Na pia tukamaliza report halafu tukaanza hii, tukaanza ku-draft Bill kwa sababu walituambia mu-draft Bill ambayo itarudi kwa wananchi hapa ndio inaitwa Constituency Constitutional Forum. Wale wananchi wa constituency wote, ndio muhimu, wako kwa hiyo forum, okay? Itatoka hapa itaenda kwa National Constitutional Conference ambayo itaanza tarehe ishirini na nane, walikata siku zetu, tulitaka tukae na nyinyi muda mrefu lakini walikata wakisema hii mambo ya kura, oh tufanye hii, Parliament ikitoka itakuwaje, hiyo yote.

Na ikawa tulitaka tukae na nyinyi tukitembea miezi mwili lakini wakasema ni 60 days, wakasema mwezi mmoja. Hata National Constitutional Conference ambayo itakuwa Bomas of Kenya mwezi November, pia siku zikakatwa, zikawa mwezi mmoja badala ya miezi miwili, tulitaka wananchi wazungumzie sana, hata Bunge ikitaka lakini mwishowe sasa wanababaika kura.

Tukitoka hapa tutaenda kule, nikukagua hii, mko na representative wenu, Esther Werangai wako? Wale wataenda kwa National Constitutional Conference, Chairman wako?

**Chairman**: (inaudible)

**Com. Adagala:** Okay, kweli Councillor is in a better position. Haya wako, wao ndio mtahakikisha watazungumzia mambo yenu. Mkikaa hivi hivi, mtapata imepotea, kama tulikuwa na watu hata walienda mahakamani, wakasema original 42 districts ndio ziko kwa Constitution tusiongeze zingine, sasa mkiendelea sana hizi zingine, Vihiga, Butere, Mumias, Lugari, na tukapigania wengine tunatoka kwa hizo district, tukapigania tukasema la, kwa nini tupunguze watu? Walikuwa na sababu, ilikuwa na sababu siku hizi ukiangalia Kakamega vile ilikuwako, ilikuwa kubwa sana, hata unashangaa, sasa hiyo pia iko.

Vitu viko vya kupambana, ukichagua watu, peleka watu wa kupambana ni kujadiliana lakini ni vita. Katiba ikitengenezwa mahali kwingine pengine hata nchi yetu ya Kenya, it is after vita vya wenyewe kwa wenyewe, civil war au ile na National liberation, kama ile yetu ya Mau Mau lakini sasa sisi tunafanya kwa amani. Na tunafanya kwa amani na inafaa tujue tunafanya kwa amani, huenda ikawa vita, vile ninaona watu wanafanya vitu dunia hii huenda ikaanzisha na sasa itakuwa ni damu tu ina -mwagika na tungefanya kwa amani.

Mpeleke watu wenu, ikitoka hapo ikiwa tumesikizana, itakuwa tu majadiliano kama hii na itaendelea mpaka kwa Bunge. Ikifika kwa Bunge, Bunge wataangalia huku na kule, waone kama inakaa vizuri, yao si kubadilisha bali ni kukagua waone kama imekaa vizuri na kusema. Wao ni law makers, wanatengeneza sheria sasa wanajua, wanasema oh, hiyo inafaa, hii inaweza kutengenezwa na Bunge au hii imebaki au tumewacha kitu kingine muhimu hapo, na watu wako huko. Kwanza nafikiri half of Parliament ni wakili, wakili na socialogists na watu ambao wamesoma. Hiyo ndio itakuwako, watu mia saba kwa hiyo kongamano, hiyo conference. Wabunge wote watakuweko, Commission itakuweko, tutakuwa tunafanya ile kazi yetu ya clerical ya kawaida. Unajua watu wanafikiri Commission, sisi ni watu wakuandika tu, tutakuwa secretariat, watu wa kanisa

watakuweko, watu wa NGOs watakuweko, political parties zitakuweko, hata share ya walemavu iko, wote watakuweko okay? Sasa itakuwa kuzungumza, mtu anauliza au watu wanauliza lakini ikifika Bunge na wa Bunge wakatae, tunasema yule Mbunge ambaye anasema sasa hapendi hii, yeye hausiki na wananchi na tena haendi Bunge, kwa sababu yeye anasema sasa hapendi hii, yeye hausiki na wananchi na tena haendi Bunge, kwa sababu Bunge ndilo lilibuni sheria, Act ya Commission.

Tumekuwa nao kwa launching, tunakutana na kamati kila mara kwa mara ya Bunge, na mwenyekiti ni Raila. Tumekuwa na district na hata tumekuja district, tumekuja civic education, tumechukua pia maoni na wako hapo kwa kamati ya Constitutional committee, mbunge ako hapo. Kwa National Conference, wabunge watakuwa huko, sasa utafika Bunge ndio utakataa au sasa ndio utakataa? Kwa sababu wamejua kila hatua na tumewapa hii report hata hii pia tumewapa na hawawezi kufika mahali waanze kusema hatukujua, ndio ilipangwa hivyo ili isifike Bunge halafu Bunge litupe mbali okay.

Na mbunge wa hapa tumeshirikiana naye nafikiri huyu wa Malava, Shitanda, tumezungumza na Shitanda kabisa, sasa akifika huko anasema na hii si kitu tupa nje, ninamwambia imekuaje hata kamati tuliunda pamoja, hata hii tulitengeneza pamoja, sasa imekuwaje? Eh, sasa tunaweza kukagua hiyo tuseme pengine wanakataa kwa sababu ingine, lakini hawakuhusika na hawakusikia maoni yenu, waliisikia, okay. Hiyo ndio tutafanya, tutaendelea hivyo.

Nimesema tu juu juu lakini hivyo ndivyo tumefika kwa wakati huu, tumeleta hii mkague vile tunakagua na tafadhali nataka tuende mbele, heshimu. Wale walikuweko wakati wa Form one, wale walikuweko wakati tulichukua maoni kama haukuweko, jua hata sasa kuna watu wachache sana wanaweza kutoa maoni ambayo hayakuweko wakati huo au maoni machache sana hayakuwa wakati huo. Tutengeneze hii tukiendelea mbele, tukifanya iwe nzuri, okay. Asante.

Tuzungumzie process, hiyo ndio inaitwa process, hiyo ndio inaitwa njia ya kutengeneza Katiba, vile tulichukua, kama kuna comment au maoni hapa tunaweza ku…ni maoni pia ni vile mna… Hapa sana inaweza kuwa na pendekezo vile ungependa iendelee kutoka sasa mpaka. Watu wanatuuliza, je tutakuwa na nini kwa Katiba mpya au kutakuwa na elections kwa Katiba mpya au inawezekana. Kwa sababu tuko na Katiba iko sasa, kwa sasa kwanza sisi hatuna uwezo, sisi ni wazaliwa wa Parliament, hatuna uwezo tunafanya tu kazi kama mfanyikazi ameandikwa kazi. Unafanya unafika pale, anasema sasa ng’ombe peleka pale, unapeleka. Maji leta, unaleta hiyo. Ni jukumu la wananchi wakisema vile wanataka, hiyo inakuwa pendekezo, tunapeleka mbele lakini sisi hatuwezi kujibu elections itakuwa kwa wakati huu, kwa sababu wakati huu, Rais ndio ana uwezo wa kuvunja Bunge na kuendelea mbele. Na ninafikiri itakuwa tu mwisho wa October wakimaliza budget, kutoka hapo mpaka December anaweza kuvunja wakati wowote. Ikiwa tutakuwa extended, hiyo ni mambo ya Bunge, until January 3rd, hiyo ni mambo ya Bunge.

Ikifika January 3rd, kwa Katiba hii, Presidential term itakuwa imeisha kwa Katiba ya sasa na pia tutakuwa na mambo mengine. Sasa inafaa nyinyi wenyewe mzungumze na tuta-report lakini pia ni majadiliano yenu.

**Cllr. Nalyanya**: Kwa niaba ya watu wa Matete hawa, hii ni maoni yangu. Kwanza ninarudisha shukrani kubwa …

**Com. Adagala**: Hauwezi kuzungumza kwa niaba ya watu…..

**Cllr. Nalyanya**: Unajua tumezoea kusema kwa niaba ya hawa watu, sorry.

**Com. Adagala**: Sitaki madharau, watu wa Matete sote tuko darasani. Asante councillor kwa kusema sorry kwa sababu sote tuko darasani na hiyo kitu ya 'nka' ni madharau, na sitaki kuisikia mbele ya Katiba, hakuna mtu hata utadharau. Pili, ni mazoea Councillor anaye lakini hapa kwa Katiba kila mtu anajiwakilisha okay, tuelewe tu hapo. Mumemchagua kweli lakini hiyo ndio iko na kila mtu ajue hiyo. Hata mtu wa kanisa akizungumza, sikilizeni. Tulikuwa na Pastor Kakamega akaniambia, "niliakilisha kanisa langu kwa kutoa maoni." Nikamwambia, walikuja wenyewe. Akasema la Mimi ndio nikamwambia ni vizuri ulikuja lakini ungekuja nao ishirini. Wao pia wawe wawepo. Sasa tuelewane tu mbele ya Tume, hakuna mtu anasimama kati ya Katiba na mwananchi hata mmoja, hiyo ndio Ukatiba.

**Cllr. Nalyanya**: Asante kuturekebisha,ni vizuri tumezoea, sorry, mimi ..

**Com. Adagala:** Ikiwa mtu anataka kuzungumza asimame, huyu mzee ndio wa mwisho kama watu hawaulizi.

**Cllr. Nalyanya**: Mimi ninasema kwamba shukrani kwa Commission ambayo ilifanya hii kazi kwa vile mumefanya fairly. Na wale Commissioners wenzenu ambao ni wasaliti, sisi ama mimi, singependa kuhusiana nao hata kidogo. Kusudi yale maoni mumeandika yote hata mengi vile mumeona kwa draft, ni yale tumepeana. Kwa hivyo hiyo inaonyesha kwamba, yale nilipeana na yale wengine walipeana, mlikuwa mnaisikiza individually.

Ya mwisho ni kwamba, muendelee vile mumepanga. Hii Katiba ni nzuri ila marekebisho kidogo kidogo ambayo sasa tunafanya vile tulivyo hapa, tu-include kitu kidogo ama kutoa lakini Katiba iko nzuri. Mimi nimefurahi kama mtu, na majina yangu ni Luka Nalyanya.

**Opanda Wamalika**: Jina langu ni Opanda Wamalika. Pendekezo langu kuhusu President ni kwamba tusikubali kuenda kwa election kama hatuko na Katiba mpya. Ni afadhali hata maisha ya Bunge yasongezwe mbele kidogo, Katiba mpya itengenezwe ndipo tuende kwa kura. Nina- suggest ya kwamba, tuwe na kitu ambacho kinaitwa civil disobedience. Ikiwa watasema lazima tuende kwa kura na old Constitution na hapo ninauliza viongozi wetu, wanasiasa, watu- mobilize tususuie hata uchaguzi ambao unakuja ili tuende kwa uchaguzi kama tuko na Katiba mpya. Kwa vile hatujui serikali ambayo inakuja, inaweza kuja na kutupa hii Katiba yenye imetengenezwa kwa trash basket.

**Com. Adagala**: Okay, maoni yako yamechukuliwa. Kuna mtu anaitwa Chiluba, ni Rais wa wapi? Zambia. Alikuwa kwa opposition wakati wa Kaunda na akasema yeye anapigania Katiba, atatekeleza Katiba akiwa President, watu wakampigia kura kwa sababu ya hiyo. Alipofika kule, aliweka kwa stand hata Prof. Ghai alipitia huko, alikuwa consultant akamuuliza Rais hiyo Katiba, akasema oh it was a very good document, ni kitu kizuri sana, akamwambia, wakazungumza tena akasema lakini unajua

inafaa iwe inatekelezwa, oh yes it is very good yeah. Wakaendelea halafu Chiluba akamwambia unajua Prof. wakati huo, I was in the opposition now I am President, alifika hapo, alikiuka hiyo na akakaa na ile ya zamani na ikaendelea. Nafikiri hiyo bado iko kwa shelves kwa sababu hakuna mtu ata .. sasa huyu kijana vile anasema, ninataka tu kumuambia kuna historia ya hiyo mahali kwingine.

**Joseph Wambusya:** Kwa majina naitwa Joseph Wambusya, ninapendekeza ya kwamba, hii siku ya uchaguzi ingekuwa kama national holiday ya Kenya kwa sababu hiyo siku ni muhimu.

**Com. Adagala:** Hiyo ni new submission, kuna public holiday kijana ngoja una kazi nyingi bado. Kuna public holiday, kuna national holiday. Ulikuwa wakati nilieleza, nilieleza Jamhuri day, ulikuwa hapa, ulikuwa haujakuja?

**Joseph Wambusya**: Ndiyo.

**Com. Adagala**: Kuna national day na kuna public holiday, okay. Na pia watu wameseme kuna siku fulani, no unasema heroes ' day au ya uchaguzi? Huyu anazungumza siku ya uchaguzi anataka iwe national day, inaweza kuwa public holiday okay. Presidential election okay, itakuwa public, vile umesema ni sawa ili watu wote waende na watu wa Seventh day wamesema isiwe Jumamosi na Waislamu wamesema isiwe. Ijumaa, wa Kristo hawajasema.

**Joseph Mabutsi**: Kwa majina ninaitwa Joseph Mabutsi, pendekezo langu ni kuhusu mabusi.

**Com. Adagala**: Haya tutafika hapo, sasa tuko kwa njia ya kuchukua mapendezo.

**Baraza Luvembe:** Majina ni Baraza Luvembe, pendekezo langu ni kuhusu uchaguzi wa Rais, ningependekeza kwamba Rais akuwe na running mate wake …..

**Com. Adagala:** Hiyo tutafika, tuko kwa processof collecting views. Chairman eleza hiyo.

**James Mawanja**: Kwa majina mimi ni James Mawanja. What the Commissioner wants now ni process yenye wamefuata kupata maoni kutoka kwa wananchi, mnakubaliana nayo au la? Hiyo, comment on that one, njia yenye wametumikia.

**Interjections:**

**James Mawanja:** *(in Luhya dialect) (Tape four)*

**Elphas Ngongo**: Jina langu ni Elphas Ngongo Salvation Army church leader na mimi ninapendekeza ya kwamba zile njia ambazo zimefuatwa na Commission kwa ajili ya uchaguzi ujao ni sawa na ikamilishe tupige kura chini ya Katiba mpya, isiwe ya zaman kwa maana ya zamani tutaendelea kunyanyaswa.

**Com. Adagala**: Okay, pendekezo hilo mumeisikia?

**Audience**: ndiyo.

**Alphayo Nyakomi**: Majina yangu ni Alphayo Nyakomi. Mimi nimeunga yale ambayo mume-propose, hiyo ni vizuri lakini sijasikia upande wa business?

**Com. Adagala**: Hatujafika hapo

**Alphayo Nyakomi**: Yale ambayo mumefanya mimi niko satisfied, hakuna neno lolote.

**Joyce Kanuli:** Mimi kwa majina ni Joyce Kanuli nitasema ya kwamba Tume ya Kurekebisha Katiba, ninaona imeendelea vizuri sana kwa ajili mwanzo imetufunza kupitia kwa radio, imetufunza kwa magazeti, imetufunza kupitia kwa makanisa, na pia kwa mabaraza, na ninasema yule mtu mwenye bado hajakuja, sijui kama atapewa muda lakini hapo baadaye yeye ndiye atakuja kujilaumu bure. Kwa ajili yale yamebaki tunasema ni asante kwa ajili tumefikia kilele chake na hiki kilele tunataka wakati watapiga kura, wapige kura kwa Katiba mpya ndio President mwenye atakuja, isiwe kwanza anaanza kusema wacha kwanza nikalie hii Katiba ya zamani kwa ajili nilikuja, tunataka ikuwe ni mpya na kila kitu kiwe ni kipya ndio hata sisi raia tukae tukijua kazi yetu iliendelea vizuri.

**Com. Adagala:** Wale wameachwa nje, nimesema muda wetu ulipunguzwa. Unajua, ingekuwa tuwe hapa Matete, Malava, tungekaa hapa hata kuchukuwa maoni ingechukua muda. Lakini tumefanya kazi ambayo hata kwenda around the country, muda ulifupishwa, sasa ungependa wale waliachwa nje ikuaje?

**Joyce Kamuli:** Asante tena kwa mara ingine, unajua kwa vile hawa wenye waliachwa nje kwangu mimi nitasema that is negligence, kukosa kuelewa kwa nini yeye ni Mkenya. Wakati wanasema wanataka kubadilisha Katiba, yeye anataka ibadilishwe lakini yeye hataki kukuja kusema ni nini anataka kibadilishwe. Sasa hiyo vile mwenyewe alijitakia, basi atafuata vile tutakuwa tunaamua.

**Com. Adagala**: Bado yeye ni Mkenya, nini itatendeka kwa yeye? Huyu ni Mkenya, okay, wewe mwenyewe ndio umesema ni Mkenya, ana responsibility ana hilo jukumu lakini pia ana rights.

**Joyce Kamuli**: Basi achukulie kwa hii muda chache yenye imebaki apate nafasi ya kutoa maoni yake na iwe kama yatasikilizwa.

**Com. Adagala**: Unajua mara nyingi wale ambao wanabaki nje ni wale ambao hawajiwezi, kama watoto, walemavu, wakina mama, baba na mama wakongwe. Na tulitaka tufikie wao wote, hata wengine tulikuwa tunasema, mass education, door to door, kitu kama hicho lakini muda ukawa mfupi, asante Joyce.

**Major Engwe:** Asante. Kwa majina ninaitwa Major Engwe, mimi ninashukuru kazi ambayo imefanywa na Constitution Review Commission, na hasa tuko na haja ya election, kazi ambayo imefanywa kwa Constitution Review imeridhisha sana,

tumepata mafunzo mengi kwa hivyo ninasema kama ikiwezekana kumaliza mara moja, election ifanyiwe kwa Constitution mpya, ndio labda ufisadi unaweza kukomeshwa.

**Edward Makokha**: Mimi ninaitwa Edward Makokha ningeweza kusema hivi, ni shukran kubwa katika kazi ambayo inaendelea lakini pendekezo langu ninaona itakuwa ni hatia kubwa sana tuweze kufanya uchaguzi kama hatutatumia hii Constitution. Kwa sababu kwa hakika zamani hatukuwa watu, lakini sasa kupitia kwa hii Constitution ni kwamba sasa sisi ni watu. Kwa hivyo ikiwa sisi ni watu, ninapendekeza ya kwamba kusiwe na kuharakishwa ili tukaweze kuingia kwa serikali ile inayokuja kwa Constitution ya zamani. yale ninayo pendekeza ni kwamba watoto wamepata haki zao, kila jamii imepata haki yake, kwa hivyo wakapewe nafasi ili kila mtu, kila mkenya, kila citizen akajue ya kwamba sasa yeye ni mtu, aishi ki-Katiba na alinde Katiba, asante.

**Jotham Laban**: Kwa majina ni Jotham Laban nina maoni kuhusu the process. Commissioner maoni yangu ni kwamba mlifanya mipangilio nzuri hadi mkafika mahali mumefika despite other hitches, but I suggest this, because Kenya Constitutional Review Commission was formed as a result of an Act of Parliament, it was not formed along the road, it was not formed in a public rally, I want it to be permanent so that Kenyans should continue learning the Constitution a day after another. So I propose that the Kenya Constitutional Review Commission becomes a permanent Commission in this Country, thank you.

**Irene Juma: (Shairi)** Kwa majina naitwa Irene Juma nina shairi, karibu. Jukwani ni mtoto wa darasa la sita kutoka shule ya msingi ya Cheptai katika tarafa ya Matete wilaya ya Lugari, mkoa wa Magharibi nchini Kenya. Nataka kuwaimbia shairi ‘ elemisha msichana, ulimwengu utaelemika’. Burudikeni.

*Jukwani na baba yangu malalamishi nitoe.*
*Nisomeshe baba mimi ujinga uniondoke,*
*misita kubeba …..baba,*
*elemisha msichana ulimwengu utaelemika.*

*Mama ni wakati gani nioshe viombo nimechoka,*
*ndugu wangu nipe sahani nilee mtoto … ..*
*(inaudible)*
*elemisha msichana ulimwengu utaelemika.*

*Baba, mama hapa duniani msichana ng’ombe,*
*wacha mahari pani mkate dakika kupata, ….*
*(inaudible)*
*elemisha msichana ulimengu utaelemika.*

*Na mkoa huu wasichana elimu bora tupate,*
*endesha ndege juu walimu nasi tupate …..*
*(inaudible)*
*elemisha msichana ulimwengu utaelemika.*

*Asanteni kamati hii kwa kuzingatia wasia wetu,*
*wacha sasa tutasoma vitabu vya ….*
*.elemisha msichana ulimwengu utaelemika.*

*Beti tano natamatisha zingatia wasia wangu,*
*asanteni walimu pia tutawa… (inaudible)*
*elemisha msichana ulimwengu utaelemika.*

*Asanteni.*

**Com. Adagala**: Asante sana msichana, asante. Tunajua wazee wana madharau wanazungumza tukiimba lakini usisurutishwe na hayo yote, unasikia? Usiogope. Ya pili, ninataka kumjulisha kuna Children Act 2001, hiyo mwambie mwalimu wenu atafute, aipate kwa District Co-ordinator halafu amusoe ile sehemu ambazo zinahusu watoto kwa Katiba, unasikia? Okay, akiwasomea hiyo ninataka kumjulisha, serikali, kusema state, serikali itadhaminia masomo ya watoto kwa Katiba mpya kutoka nursery mpaka Standard eight full, bila malipo lakini, mnasikia? Mnaelewa? Sasa hakuna kusema sitaki kuenda na hakuna ya mzazi kusema mtoto hataenda, hakuna kitu cha kutoa mtoto kwa shule, aende kwa ndoa. Mpaka awe miaka kumi na nane, mnaelewa? Muwaambie watoto wengine hiyo.

Mtasomeshwa na serikali mpaka standard eight kwa Katiba mpya. Ndio inafaa wazazi hawa ndio wanazungumza zungumza pengine wao si wazazi, inafaa msimaie hii Katiba kwa sababu ikikosa kutengeneza, sikiza, watu wote wanasikiliza?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Adagala:** Ikikosa kutekelezwa, *vasakulu vammoloma shirangani*. No, sio heshima, kutosikia mambo. Ujue, hii Katiba ikikosa kutekelezwa, kama haitapitishwa, ile Bunge itakuja itaweka kando na watasema mpaka mwaka wa 2007, ndio itatekelezwa. Sasa kweli inaweza kuwa watu wa siasa wanasema oh, tunataka Bunge hivi, tunataka rais hivi, lakini nyinyi watoto mjue mtakuwa bado na ile shida mnayo sasa, ya kuenda shule. Yule msichana ameimba, sio msichana peke yake asome, pia mvulana lakini wazazi wanabagua. Tunataka wasichana na wavulana wasome pamoja mpaka Standard eight, wewe una miaka mingapi?

**Speaker:** (Inaudible)

**Com. Adagala**: Kumi na mbili kwa class gani?

**Speaker**: (inaudible)

**Com. Adagala:** Six, inamaanisha seven and eight ungesoma bure, lakini wakikaa sana na hii, utakuwa na miaka kumi na saba ambayo utakuwa bado class six? Utakuwa bado uko?

**Speaker:** … (Inaudible)

**Com. Adagala**: Utakuwa pengine umekosa school fees, pengine umekosa hiki na kile. Sasa ndio nyinyi watoto inafaa mfanye bidii mzungumze, museme hii Katiba itekelezwe. Hiyo Bill of Rights, huo ukatiba wote utasimama, wananchi nataka msikie sio mambo ya siasa peke yake. Hiyo yote yatasimama mpaka mwaka wa 2007 ndio yatakuweko. Haya, asante, Mungu awabariki watoto. Tumefurahi, kama una maoni mengine, unaweza kutoa kama watu wengine, mnapanga laini tu na mnatoa. Asante.

**Student:** Karibu, mbele yenu ni watoto wa shule ya msingi wa Cheptai, kata ya Chebaywa, kanda ya Chebaywa, tarafa ya Matete, wilaya ya Lugari, mkoa wa Magharibi nchini Kenya. Tayari kuwakariria shairi kwa mada, natumai mutamakinika.

*Tunayo mengi ya kusema, tegeni masikio musikie tunalotaka kungamua ….*
*hongera kamati ya Katiba, ………. Katiba yenye ……. ………….. imezidi kutunyanyasa asanteni kwa kuzingatia iliyo njema. Hakika sisi …..*

***Wasichana**: Sisi wanawake tumechoka kubaguliwa, katika elimu, afya na uchumi. Nafasi tupate ……. Hakika kitu njema ni gani?*

***Wavulana**: Hamjui kazi ya wanaume, wanawake kazi yao, kuzaa, wanaume ku……. Kiboko, ee siku njema ni gani?*

***Wasichana**: Wanaume sikizeni tunataka tuwe sawa, kusema kweli tumechoka kuomba sana, kama tungekuwa chombo hamungetupenda, hakika siku njema ni gani?*

***Wavulana**: Mmh, bure, munajipa moyo, wanaume tutashinda, mpende msipende, tutawaachia maviketi, kuni na maboma. Ee, siku njema ni gani?*

***Wasichana**: Tumecho kubaguliwa, twendeni twendeni bunge, kila siku kujaza mikopo, hakika siku njema ni gani?*

***All:** Watoto tutasomesha sasa, mavasi tutanunuliwa sasa, chakula na matibabu tutapata, hakika siku njema ni Katiba mpya.*

*Aah, maoni, Bunge la wanawake,*

*Bunge la wanaume,*

*Bunge la wanaume,*

*Bunge la wanawake,*

*Bunge la wanaume,*

*hongera kwenu, hongera Kenya, asante kwa mapendekezo hayo, Mungu awalinde nyote. Hakika siku njema mumeandika Katiba ya umoja wa kitaifa, asante.*

**Com. Adagala**: Ngojeni watoto, ngojeni, hii Katiba ni Katiba yenu hasa. Ni nyinyi ndio mtaishi nayo for a long long time. When you are fifty five years old like me, you will be telling people, I was there, isn't?

**Students:** Yes.

**Com. Adagala**: Yes, it will be history, this is a historical day. Maybe there will be some other time for your children or grand children to do this, but this is very important that you have come here and tumefurahi sana. Sasa mtafundishwa ile na mwalimu wenu kuhusu yale yajayo, ile siku njema iko hapa kwa Katiba, hiyo kurudi tena kwa kubishana wanaume na wanawake okay? Na vile nimemuambia watoto wote watasoma na hakuna mtoto atasema mimi sitaki kusoma, kwa sababu serikali inasema, nimekulipia, utaenda okay? Na mtie bidii, mtie nguvu na ongojea yule atakuja kuchukua nafasi yangu university of Nairobi kule ninafundisha awe Professor, okay? Na ngojea tu kutoka hapa. Salamieni wazazi pia muambie wazazi, mnajua watoto ndio wanafundisha wazazi? Muwafundishe muwaambie siku njema ni, Katiba mpya Asante.

**Grace**: Mimi kwa majina ninaitwa Grace Fedha na ni asante wanaoingia stage ni Kaburengo umoja women group, wangependa kuwatumbuiza kwa dakika mbili, wataimba dakika mbili msiende mbali. Wanaimba wimbo wa Katiba, uzuri wa Katiba, wanawake sasa ni watu mbele ya watu. Walikuwa wanasema watu na wanawake, sasa sisi ni watu. Karibu.

(song)

**Com. Adagala**: Okay, akina mama asante ngojeni kidogo. Wakina mama mumesema vizuri tumeenda kwa siku ya kusonga mbele na kushirikishwa lakini nataka wakina mama wajue ni jukumu lenu kutekeleza Katiba, wasichana lazima wasikie wako kwa Katiba, okay? Kitu kimoja wakina mama wanashiriki na wanarudisha wasichana nyuma, ni hiyo ya kutowapeleka shule. Sasa shule itakuwa bila malipo, watoto wote waenda. Usibakishe mtoto msichana nyumbani, oh, niko mgonjwa, ukibakisha msichana, mvulana abaki siku nyingine. Hiyo ndio kutekeleza?

**Wa mama**: (inaudible)

**Com. Adagala**: Yeah, wote washiriki. Mnatenga kazi za watoto wasichana na wanaume, nyinyi wakina mama ndio mnatengeneza vibaya, muache hivyo. Mtoto akizaliwa ana haki zake kama mwingine, ugawe shamba na mali kwa watoto wote sawa, na hapo mjue iko kwa Katiba.

Binti lazima waridhi kama wale wengine, okay? Hakuna kitu cha msichana, nyinyi wakina mama ndio mnarudisha mambo nyuma kawaida kwa watoto wasichana, na ukiwa na daughter in law, unamfanya mtumwa sivyo? Mnamfanya mtumwa? Mnapenda hivyo?

**Wamama:** Hapana.

**Com. Adagala**: Muache hiyo kasumba ya kulalia mtoto wa mtu mwingine kwa sababu amekuja kwako, na ikiwa hivyo wacha nikuambie atarudi kwao kwa sababu atakuwa na makao kwao, mnasikia?

**Wamama:** Ndiyo.

**Com. Adagala**: Na Katiba itamsimamia, asanteni mama, mfanye bidii, muunge mkono kwa sababu mkikosa nyinyi ndio mtapoza zaidi kwa sababu yenu mengi yaiko kwa Katiba. Yakikosa kuchukuliwa sasa, uchaguzi ufanywe kwa hii Katiba, vitu hivi vyote tumefurahia
vitalala kama shamba ambalo halijalimwa. Mpaka mwaka wa elfu mbili na saba ndio itaanzishwa, okay?

**Wamama**: Haya.

**Com. Adagala**: Wao watu wa utamaduni tunafurahia lakini tu ..

**Geoffrey Makina (Band) song:** Hii ni Chapwelale band, tutawatumbuiza kidogo. Jina ninaitwa Geoffrey Makina.

**Com. Adagala**: Na hii group yako?

**Geoffrey Makina**: Group yangu inaitwa people (inaudible). band. Tuko na vituko kidogo.

**Com. Adagala**: Mna dakika mbili.

**Geoffrey Makina**: Sawa

(SONG)

**Com. Adagala**: Asante sana, asante sana kwa utamaduni wenu. Na inaoneka wa Luhya tuna kitu ambacho kinafaa tusambaze nchi nzima na dunia nzima, hii shiriri inafaa ijulikane kwa sababu inazungumza vizuri sana. Asante, utamaduni wetu

umehifadhiwa kwa Katiba, okay?

Tamaduni zetu, lugha zetu, mila zetu ziko kwa Katiba. Sasa muendelee na mjue ikiwa hivyo, hata unaweza kuenda kwa mbunge na umuambie hii nini yetu inafaa iendelee, Councillor hii nini yetu inafaa iendelee, hii band yetu tunataka tupate njia, sio saa zote pesa, njia saa zingine inapanua sana. Na nimefurahi ninashukuru kamati na District Co-ordinator kwa sababu mpango ni mzuri, imesema mengi asanteni. Mzee asante, Mungu akubariki na vijana wako.

Mlisikia vile nilisema, don't just get lost in political debate about President, this or that one you can do but know that your bill of rights which you have just talked about will not come to fruition if the Constitution is delayed until the year 2007, know that okay? Hii mambo ya watoto kulipiwa school fees, haitakuweko na watoto wengine wengi sana hata walikuwa wamekwama kwa sababu shule ni ghali na ikiwa na hiyo Katiba ya sasa, uchumi utaendelea kuwa mbaya.

Sasa hiyo inafaa tujue, tuendelee lakini tutapitia kwa njia ya haraka kwa sababu sasa tumezoeana okay? Wacha tupitie unajua wakina mama wengine wamechoka na kuketi kwa sababu kazi yao sio ya kuketi, yangu ni ya kuketi na kufundisha sasa hiyo …..

Kamati iko wapi, committee Chairman, muite Chairman, simameni nyote na District Co-ordinator. No, no, watu wa kamati peke yao. Sorry, Kiswahili changu ni kibaya, nataka kumkabithi na kulete report ya Malava Constituency, yenyewe ambayo imechapishwa na imekuwa bound iko njiani inakuja lakini hii ndio inasema Malava Constituency, Chairman ako wapi? Chairman, chair run run, kimbia nione kama uko bado. Ndiyo, mimi nilikuwa champion wa 100 yard, sasa ukiniangalia, simama hapa.

Hii ni report ya Malava Constituency, tumemletea na sisi watu wa Tume tumefurahi kila mara tumekuwa tukipeana report na vitu mlizungumza viko hapa ndani yake na ninamletea ili mkague, Chairman una mahali? Hapo kwa DO mna ofisi hapo? Haya utakuweko, mkitaka ile ingine itakuwa rahisi kama kufanya photocopy, sasa ukitaka utatoa (inaudible) still keep this one and you will have the one which is spiral bound na mtatumia hiyo, ndio itakuwa yenu kuangalia na muiweke vizuri. Do a photocopy of the one which is something smaller, that is the one which you should be giving people to photocopy, okay? Or you make photocopies and you know how much it cost, don't go into an expensive undertaking and wachakue. Wataona majina, kama ulitoa maoni Malava, jina lako litakuwa hapo na maoni yako yatakuwa hapo, okay? Mnashukuru?

**Chairman:** Kwa niaba ya watu wa Malava Constituency, ningependa kurudishia shukrani kwa Commission yote ya Constitution Review na hasa sana Commissioner Adagala na team yake wenye wamekuja ku-launch hii report hapa leo. Na kitu chenye kimetustajabisha ni ya kwamba walitengeneza hii report haraka sana hata mimi sikutarajia itakuwa tayari wakati huu. Sasa ni pongezi kwa niaba ya watu wa Malava ya kwamba mumefanya kazi nzuri, upeleke hiyo report.

Tena kazi yenu imeonekana, iko very thorough, mtu mwenye anataka ku-complain, mko tayari kumuonyesha, ilikuwa hivi na kutoka wapi na kila kitu. Sasa ni shukrani kubwa kwa kuja kwenu, hata pia Commissioner watu wa Malava wamefurahi sana vile tulienda uko, tulianza kama tuko wachache, sasa ninaona kama hall yote imejaa. Asante sana.

**Com. Adagala**: Pia watu wa mahakamani wakitaka maoni ile mlitoa, mnaweza kuwapelekea hiyo nakala iko hivi eh. Hakuna kile hakiko humo ndani, mtu wa education akitaka, anaweza kuuliza watu walisema nini kuhusu education na itakuwa hapo okay. Mtu wa nini, chief akitaka kujua walisema nini kuhusu chief, iko hapo okay. Haya kila mtu, na ninataka kumjulisha tukifanya kazi, mimi nimeajiriwa karibu miaka thelathini sasa na wakati nilifanya kazi nguvu hivi ni wakati nilikuwa kwa masomo ya Masters ng'ambo. Una- lala masaa mawili unaamka unaenda darasani, unasoma, unaandika karatasi, hivyo ndivyo tumefanya.

Na hata tulikuwa tunaenda kulala saa tano za usiku, saa sababa za usiku, saa tisa, saa kumi. Na lazima uamke mapema uende, na tukitoka hapo hata tukienda kulala hauna usingizi, unajilamisha tu kwa sababu mawazo bado yako halafu unaamka tena. Hapo pia tulikuwa tunafanya hasa mwisho mwisho, hiyo mambo ya kutengeneza daraja, hiyo daraja niliwaambia kufika kwa Katiba, ilikuwa ngumu sana. Na tuliandika, hata hiyo Preamble nimewaambia ilichukuwa maandishi mengi sana ndio ikafika hapo. Si kitu tuliketi tu na ku-copy mahali na tunaendelea, na tulikuwa tunaenda kulala, na Prof. Ghai ako hapo kwa computer yake, anasema tu good night na anaendelea na kuandika.

Halafu ukienda nyumbani ukirudi unapata ameshaenda nyumbani amelala masaa mawili amerudi, wewe umelala tatu, amekushinda amerudi. Na hiyo ndio ilikuwa kazi yetu na tunatarajia siku moja itakuweko watu wa Kenya watafanya kazi na bidii hivyo. Kwa sababu kuna bidii ingine hatujashika sana lakini ninapenda kusema wa Luhya wanayo. Kile kinawashinda ni biashara lakini bidii wanazo, kufanya kazi, wanayo.

Na hiyo ninataka kusema, tunashukuru kwa sababu tulijua hata watu wakitaka kusaliti, tunajua wananchi wako na sisi. Tuko hivi tumesimama imara, na hivyo ndio Katiba inafaa ilindwe. Mtu mwingine alisema hapa inafaa tuwe na Tume ya Constitution iko, iko kwa Tume kumi ambazo zimetengenezwa na ninataka kuwaambia hii mambo tumezungumzia ya Katiba, the Bill of Rights, hiyo ni nzito kama ile ya Preamble. Hiyo ni mambo mazito sana, hii ingine tunasema inatokea tu hapo, si ngumu.

Kijana ataendelea, kuhusu process tumemaliza? Process tumemaliza, kuna mambo mengine magumu magumu kwa process lakini tutaendelea.

**Vincent:** Sasa tutapitia sura ya sita kwa muktasari tu.
**Com. Adagala**: Tunaendelea lakini kwa vile mumezoea, tutafanya … okay?

**Vincent:** Sura hii inaongea juu ya uwakilishaji, representation. Sura hii iko na maadili ya ki- jumla ambayo yako katika

sehemu ya kwanza ya sura hii kwamba uchaguzi utakuwa wa uhuru na haki na kila Mkenya anapewa haki ya kupiga kura na kusajiliwa kama mpiga kura.

Kila Mwanakenya ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na minane ako na haki ya kusajiliwa kama Mwanakenya. Lazima atimize masharti Fulani, awe mkaazi wa Kenya kwa kipindi cha miaka Fulani. Kuna maelezo kadhaa ambayo yako chini ya kifungu hicho. Na Mkenya atapoteza haki ile iwapo hatakuwa na akili timamu ama labda alipata uraia wake kwa njia ya udanganyivu. Pia Tume ya kura imebuniwa katika sehemu hiyo, Tume hiyo itakuwa na mwenyekiti na wanachama wasio zidi kumi na wasio pungua nane. Pia watu hawa itabidi watimize masharti fulani ambayo yameorodheshwa katika kifungu cha themanini na tatu.

Kazi ya Tume hii pia imeorodheshwa katika kifungu cha themanini na nne, natumai mtapata wakati wa kusoma. Kazi ya kutenga maeneo ya upigaji kura yamepewa Tume hii. Pia Tume hii ndio inasajili vyama vya kisiasa na kila Mkenya ako na haki ya kubuni chama cha kisiasa iwapo tu itatimiza masharti Fulani; iwe ni chama ambacho kina malengo ya kitaifa na sio malengo ya kidini na malengo yale duni.

Katiba hii pia inapatia Tume hiyo uwezo wa kufuta usajili wa chama fulani ambacho kimekiuka masharti ambayo yako katika sehemu hiyo. Vyama vya kisiasa sasa vitapewa msaada ama fedha ama pesa za umma, vyama vya kisiasa vitapata marupurupu kutoka kwa fedha za umma.

Lazima kitimize masharti fulani ndivyo kiweze kupewa senti hizi. Na vitabu vya vyama vya kisiasa vitakaguliwa na iwapo itapatikana kwamba fedha zile zinatumiwa kwa njia isiyo-faa, vyama hivi vitapoteza hati hiyo.

Hayo yote mtayasoma katika sehemu ya tisaini na nane. Vyama vya kisiasa pia, shughuli zake, the role, imetaratibiwa katika Katiba, itaongoza wananchi katika shughuli za demokrasia na utunzi wa sheria. Kwa muktasari tu, hayo ndio mapendekezo ambayo yako katika sura ya sita. Tutaendelea hivo hivo sura ya saba, ambayo inaongea juu ya Bunge, sasa yafaa mjue kwamba Bunge litakuwa na nyumba mbili, ama milango miwili.

Kutakuwa na Bunge la National Council ama baraza la kitaifa na Bunge la National Assembly ambalo ni Bunge la sasa. Bunge ndilo litakuwa na uwezo wa kupitisha sheria fulani fulani lakini uwezo huu pia utapewa serikali za mashinani, tutaona hapo mbeleni. Bunge pia limepewa uwezo wa kuidhinisha uteuzi wa Rais, wa watu ambao watashikilia nyadhifa tofauti tofauti kwa serikali, watu hao ni afisi ambazo zimebuniwa katika Katiba hii na uwezo huu uko katika kifungu cha mia moja na tatu.

Nimewaambia kwamba kutakuwa na nyumba mbili za Bunge. Nyumba ya kwanza, National Council itakuwa na wabunge 70 ambao watachaguliwa kutoka kwa kila wilaya ama wilaya ya Bunge na wengine 30 ambao watachaguliwa kutoka kwa vyama vya wanawake, vyama vya wasiojiweza na vyama vingine vya kabila ndogo ndogo ama marginalized communities na pia katika

kila mkoa kutakuwa na at least wanawake wanne.

Mkoa wa Nairobi nao utawasilishwa na wanawake wawili nayo National Assembly itakuwa na wanachama ama Wabunge mia mbili na kumi ambao wameteuliwa kutoka kwa maeneo ya Bunge. Wengine 90 ambao wameteuliwa na vyama vya kisiasa. Watu hawa lazima watimize masharti fulani. Kama ni mbunge ambaye atakuwa mbunge wa National Council, lazima awe amefikisha umri wa miaka thelathini na mitano na zaidi na mbunge wa National Assembly ama Bunge la sasa lazima awe ametimiza miaka ishirini na moja.

Hayo ndio masharti muhimu, atapoteza haki hii ikiwa labda hawezi kulipa madeni yake ama hana akili timamu.

**Com. Adagala**: Kuna maoni hapo kuhusu hizo mbili, wakilishi wa wananchi na pia Bunge. Kuna mambo, hiyo lazima Council… Councillor uko hapa?

**Councillor:** Niko.

**Com. Adagala**: Okay, unajua Council ilikuwa inafika kwa County Council, Town Council halafu kule juu, nyadhifa za juu kule, hawakuwa na kitu, sivyo Councillor?

**Councillor:** Ndivyo.

**Com. Adagala:** Sasa tumeweka National Council, hiyo ni Upper House, na hiyo Upper House inaanzia kwa village, defination ya village ni Sub-location, inaenda kwa location, inaenda kwa district, inaenda kwa Province, na njia ingine… Tungekuwa tunachora, na njia ingine inaenda kwa National Council, Upper House.

Lower House ni Wabunge wale wako sasa, wa kutoka kwa Constituency, wanaenda wakina Shitanda hawa, wanaenda National Assembly, unaona? Okay, hiyo ndio iko. Tumebuni nyumba mbili kwa sababu watu waliuliza vitu fulani, waliuliza village elders wawe recognized, tume-waweka kwa Katiba. It is a Constitutional office now, village elders, vile walikuweko walikuwa tu wanafanya, Chief ndio alikuwa kwa Constitution hata Assistant Chief vile tu Chief ako ndio alikuwako.

Village elders ambao watu wote nchi nzima waliwapenda, watu walipenda watu sampuli mbili, village elders na nursery school teachers. Hao ndio watu walipendwa na nchi yote, tukawaweka hapa. Sasa mjue hiyo serikali ya nyumba ya pili au mlango wa pili wa Bunge, tunaenda huko na inaitwa Parliament yote, lakini National Assembly na National Council, haya maoni?

Kitu kinaitwa watu walisema, wabunge wengine wanachukua kura wanaenda Nairobi anakaa, miaka tano wanarudi. Sijui kwa nini mnawapigia kura tena. Kama Orengo, Orengo hata akikosa kwenda nyumbani atapata kura, hata akiwa kwa chama gani, atapata kura. Ni kama Shikuku alikuwa. Alikuwa anapata, anaenda na mahali pengine tulikuwa tunawaambia, salamia mbunge wenu hatujamuona, Commissioners mumusalimie hakuja hata leo kwa siku ya maoni lakini msalimie.

Wengine wakatuambia, tulienda na ndege huku kwa wa Borana, huko Moyale, na tukaambiwa, mumefanya vizuri mumekuja na mbunge wetu, tumempigia kura miaka kumi na tano, hata hatujui tunapigia nani lakini mumefanya vizuri kumleta. Na kweli kwenyewe ni kugumu sana hata hiyo constituency ni ngumu sana, sasa wanasema mumefanya vizuri, sasa tunamuona tunamjua. Na yeye ni Minister of Foreign Affairs, okay? Sasa hiyo ndio tunasema mbunge akikosa kutekeleza wajibu wake, na mbunge nilimuambia, muangalie hawa wabunge mara ya mwisho, haitakuwako tena na wabunge wa aina hii, wala Councillors wa aina hii, wala President wa aina hii kwa sababu haitakuwa na mambo ya power na pesa na itakuwa ni, mtu mtumishi.

Pengine hata tutabadilisha hii term itoke, 'mheshimiwa', iwe mtumishi, ili wajue. Sasa mtu akitaka kuwa ataenda na kutumia wananchi, akikosa kuna ile kitu kinaitwa, right of recall, haki ya kumrudisha nyumbani arekebishe au atoke.

Na nyinyi mlisema wenyewe, wananchi walisema hivyo, sikizeni, akiwa Rais, sikilizeni muende kuambia watu wa nyumbani. Akiwa Rais itakuwa vote of no confidence, ikiwa Prime Minister itakuwa vote of no confidence, ikiwa mbunge itakuwa power of recall,mnamuita, mnamuita mnachukua majina halafu mnasema 30% ya watu kwa constituency kuanzisha hiyo process lakini inapelekwa kwa Speaker, Speaker anamwambia kwako wanakuita, tutakagua tuone wanakuitia nini. Lakini hiyo ni ya …watu wengine wanasema inafaa iwe 50% of the voters, nusu ya wale walipiga kura ndio arudishwe.

Hiyo ndio kitu muhimu ndio tumeweka hapo na walisema wabunge wawe na ofisi kwa constituency, wengine kama kwetu Sabatia already there is an office, wakasema hiyo iko lakini tunataka kwa location, okay. Sasa hii kazi ya ubunge haitakuwa rahisi, Councillor pia anafaa atekeleze na watakuwa na pesa ya kutekeleza ya kufanya mambo na akikosa kufanya hiyo pia mnapitisha. Anakuja, inapelekwa barua kwa district, anapitishwa pengine alichukua, ni vigumu Councillor kukimbia kwa sababu anakaa hapa. Lakini wabunge wanaenda, wananunua nyumba huko, hiyo ndio kitu inafaa mjue, the power is the people's, they only give it to their representative kuwaakilisha, na wakikosa kuwakilisha, wanarudishwa na kuulizwa maswali halafu Speaker ataangalia, pengine tutakuwa na wengine watasema jinsi itaendelea zaidi na akipatikana bila makosa itakuwa tofauti. Lakini ina makosa, itakuwa hiyo ya kutohudumia watu.

Hiyo kitu ya mishahara, watu walisema hao wabunge, wanajiwekea mishahara mikubwa, kwa siku ishirini wamepata nusu milioni. Watu walikasirika na walimu ambao wanafanya kazi nyingi wanalinda watoto, wanaelemisha taifa nzima, hata hawapati. Hiyo kitu irekebishwe, walituambia hivyo, tukasema basi, wametuambia hivyo na tutafanya kazi. Wakisema hivyo tunajadiliana inaweza kuwaje, tutakuja na Commission of Salary and Emolument.

Mishahara ya watu wote wa umma itakuwa kwa hiyo Commission, watajadiliana hawa watu wanafanya kazi inafika wapi, mshahara yao itafika wapi, na ikitoa order, kwa sababu ni Constitutional office, ni Tume ambayo iko kwa Katiba, lazima itekelezwe okay? Sasa walimu wangekuwa hapa, walimu wenzangu wako wapi hapa?

**Audience:** (inaudible)

**Com. Adagala:** Nimefurahi, hiyo mambo ya strike tusilipize, strike is legal, ukitaka kuandamana, ukitaka ku-strike uta strike. Sasa walimu wote wangekuwa hapa kwa sababu tumeshajulisha mambo yenu. New bottles, new wine, mnaelewa? New Constitution new rights.

**Vincent:** Sasa tuko sura ya nane ambayo inaongea juu ya Urais. Kwa muktasari tu..

**Com. Adagala**: Si kupita, si pendekezo.

**Cllr. Nalyanya**: Hakuna saa lakini ulipokuwa nje walisoma habari ya Electoral commission na hiyo ndio shida ya watu hapa.

**Com. Adagala**: Pendekezo?

**Cllr. Nalyanya**: Pendekezo ni kwamba, kama sisi sasa watu wa Matete hatujui na hatuelewi tuko wapi, hata watu wanajaribu kuamua kwanza, huenda wakarudisha kura kusudi tumefinywa, sisi tuko wilaya ya Lugari, kama wilaya yetu lakini kura tuko Malava mahali ambapo hatupendi na tulikatwa tu kwa nguvu kusudi ya Constitution ambayo ilikuweko. Sasa sisi tufanye nini?

**Com. Adagala**: Kuna kitu Councillor kinakuja na si nyinyi peke yenu, ita Councillor, simama huku Councillor, kuna kitu kinakuja watu wa Malava msikie, you have … mna shida ya constituency?

**Audience**: Yeah.

**Com. Adagala**: Mna shida ya district?

**Audience:** Yes.

**Com. Adagala**: Kuna Tume itakuja, na unajua tulikuwa na shida hapa na Prof. Ogendo, na Prof. Ogendo, hakuna lile linamshinda, lakini tulishindwa na mambo ya hapa. Lakini kwao pia wako na hiyo, huko Nyando, wana sehemu moja PC Raburu alisema, siwezi kuenda kwa hiyo district mimi, akabaki Kisumu lakini mnajua hiyo ndio kitu tunakataa, hiyo kasumba, akasema constituency itakuja yes, itapitia huko lakini, mimi nitabaki Kisumu. Lakini anasema mimi, ni wapi sehemu yake? Sasa hii mipaka yote kuna boundary Commission, okay, itasuluhisha hiyo. Kwa sababu hatuwezi kusema yote hapa…

**Cllr. Nalyanya**: Kabla ya kura?

**Com. Adagala:** No, constituency tunajua tulitaka daraja tena, daraja ya kuvuka, tulisema tusitatize na kuzungusha zungusha wananchi. Hata hao Provincial Administration, hawakufutwa kazi, waliambiwa tu, report to your employer, okay? Let me talk about it, hii ya hapa, the 210 constituencies will remain for this lakini baadaye kitu kitakuwa na kazi nyingi ni hii Tume, itakuwa na kazi nyingi sana, na hapa ndio mahali pamoja, kwingine ni Sotik na ingine ya mikoa.

Kama watu watu wa Garissa wanasema, Garissa iko Coast Province, okay? Haya ninataka kumjulisha hiyo itasuhuliswa na

itasuhuliswa, sio kwa wakati huu wa many transition, many difficult things. Tume itakaa, okay? I am happy even if it is raining na hatutaendelea sana, nimefurahi nimeleta hiyo kwa watu wa Malava, itasuhulishwa, sio wakati huu. Hakuna constituency change, hata huko Gachoka wanataka, hata wapi, lakini hiyo itafanyiwa by 2007 itakuwa yote sawa okay.

Najua mumevunjika moyo lakini hiyo nilisema itakaa, okay? Let me tell you, vitu vya constituency si vitu vya haraka. Kuna kitu kingine kina-semekana, *oo munyore avekuno mba,* Munyore ako wapi? Munyore wako hapa watoe hii mvua, kuna kitu kinaita MMG na watu wakasema ni nominated Members of Parliament. Sio hivyo, sehemu zile ambazo haziwakilishwi hata Councillor alikuwa amesema Tachoni ni wengi ni sawa, lakini sehemu kama hizi zitaangaliwa si msonge mbele? No, it is okay, sit, wacha wale waje, haya keti. Mnanisikia?

**Audience**: Yeah.

**Com. Adagala:** Sehemu kama hizi kura itapigwa na tutakuwa na 90 elective seats by political parties, ndio tunazungumzia watu wa kabila ndogo, wanawake, walemavu hata watu wa kabila ndogo wamekuwa walemavu, sivyo?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Adagala**: Hata nimefurahi ni mimi nimekuja hapa kwa sababu ninajua shida zenu, tulikuwa hapa na tukapitia wengine wakawa Lugari huko kwa constituency hiyo na huku, hivyo viti wale ambao wanajisikia hawawakilishwi, hizo 90 seats ni zao, za wanawake ziko huko ndani, za walemavu ziko humo, za kabila ndogo ziko humo.

Kama huko Maseno kuna sehemu ambayo wa Luhya wanaishi, Kisumu Rural, na wamesema since 1905 they have never even had, hawajakuwa na Assistant Chief, hawajakuwa na waakilishi kwa sababu hiyo inachukuliwa na majority, MP anachukua, MP anachagua Chief na Assistant Chief, si mnajua hivyo wanafanya?

**Audience:** Mmh.

**Com. Adagala**: Wakasema kwa wakati huu, wale ambao watakuwa kama wadogo kwa hiyo sehemu watawakilishwa na huyo mbunge ambaye atachaguliwa na chama. Sasa kama hapa Malava ikiwa ni Ford Kenya itachukuwa kama vile, sitaki kubadilisha kwa sababu tutafika kwa mambo mengine, watu wa Matete tunajua mliuliza mnataka constituency yenu.

**Audience:** Eeh.

**Com. Adagala**: Na wa Luhya wamezaa ni wengi, hiyo tunakubali. Tunasema watu wa Matete watasema sisi hatuakilishwi, wengine wale ni Kabras, na hapa ni mchanganyiko. Sasa mtasema sisi hapa ni mchanganyiko tunataka hicho kiti kimoja cha watu tisaini, mtu ende atuwakilishe Bunge, okay. Na party ambayo itakuwa imechukua kiti hapa, itamsikiliza na nyinyi mtasema nani au mtachagua watu wawili au watatu kwa sababu ni election halafu party ita elect na aende kumuwakilisha hapa.

Kwa wakati huu hatukutaka kwenda kwa mambo ya mipaka ya ..hata hatungemaliza, lakini bado mnaweza kufanya pendekezo

na mseme hata hivyo, tungependa kuwa na constituency yetu. Kugawa ma -constituency si kitu kidogo, lazima hiyo Tume ya Electoral pia itembee ifike sivyo? Tukisema tu haitatosha, hilo ni jukumu lao kutembea na hii Tume iko, kazi yao hapa is to conduct the next election na ku-wind up business in 90 days. Miezi mitatu wawe wamemaliza kazi yao, Tume mpya itachaguliwa ambayo haina vitu vyao … itachaguliwa na Bunge okay?

Wao watafanya Bunge lizaliwe na Bunge ikizaliwa, Bunge litabuni Electoral Commission mpya, hiyo ndio sasa itakagua. Tafadhali Councillor wewe ndio unafaa uelewe hii ueleze …

**Councillor:** (inaudible)

**Com. Adagala**: Naona mzee ako hapa angekuwa namba one kwa darasa kwa sababu amekaa vizuri, very active. Msife moyo kila kitu hakiwezi kutendeka kwa siku moja.

**Interjection:**

**Com. Adagala:** Sasa muelewe kuna mtu akisema, unajua wasichana wanachanganya mambo wanasema, 90 nominated MPs ni elected na kuna wale ambao wana … Sasa mkitaka kuchanganya mwanamke na pia mtu wa Matete, hiyo mtakuwa mumejiweka mbele sana. Kwa sababu itakuwa oh ni mwanamke. Hata mlemavu alikuwa hapa na mimi nimeketi na walemavu, hata Prof. Ogendo ana jicho kama hili langu moja na mguu umempa shida, ni kama mlemavu, okay? Hii *yamwada* na hii ina operation, na hata Ombaka. Kuna watu ambao wako capable, msichukue… Mlemavu bado ako hapa? Alienda, anaona mvua. Angepelekwa nyumbani hata, lakini inafaa mfikirie na muone mtawakilishwa Bungeni na hivyo viti. Sasa ikiwa safina ndio ita … hapa, itawalazimisha kwa sababu kuna division nyingi by the way.

Watu wa Gachoka walisema huo Nyagah wametutawala huko wametusahau, sasa chini ametusahau, tunataka Mbunge wetu. Sasa huyo atakuwa huyo wa elected, inaitwa MMG. Mimi sikuweko wakati huo, bado nilikuwa ninazika baba yangu kwa sababu alifariki wakati huo, sasa nina elewa hivyo. Lakini Prof. Ghai angeeleza kwa nini, hiyo sio nominated itakuwa elected by party. Siku ya kupiga kura utakuwa una piga kura na pia, mnapigia party. Sasa parties zitakuwa na … na imewekwa kwa sababu ya watu kama nyinyi au parties, watu wamesema President is a President with minority votes. It is not true, kwa sababu ya sasa sio ukweli kwa sababu hiyo opposition ingekuwa party moja, wangepata nyingi.

Lakini hauwezi kuchukua mtoto ambaye amekuwa namba one with ten marks na wa pili alikuwa na nane, na watatu alikuwa na tatu, halafu tena useme sasa hawa wote, wana nyingi kuliko namba one, sasa huyu hastahili kuwa namba one. Hiyo tunaita simple majority, okay? Sasa hiyo si kweli lakini tumefikiria watu wa kabila ndogo wawe na wakilishi kwa wakati, yule ako elected by party.

Electoral Commission ambayo inasimamia uchaguzi ndio inabadilisha mipaka na inaongeza constituency na hiyo itabuniwa na kukagua na kutembea Kenya nzima na kusema, kama Nairobi Westlands ni kubwa kuliko Vihiga district na ina wapigaji kura

mia moja elfu na zaidi, Nairobi inafaa ikaguliwe itakaa vipi lakini kwa wakati huu itapita kwa hiyo njia ya MMG okay.

**Cllr. Nalyanya:** Ile ambayo nilikuwa nayo ni kwamba ni kuelewa vizuri watu wa Matete hawa shida ya constituency…

**Com. Adagala:** *khali uvoli mmu lluhya*.

**Cllr. Nalyanya:** *(in Luhya dialect) Tape 4 Side B towards the end.*

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Adagala:** Ministry, yes, yeye ndiye anaelewa hiyo na wengine hata tulikuwa hapa, mlitutaka ………..(*luhya dialect*) okay, na hiyo pia itakuwa hiyo boundary Commission, na hiyo itabuniwa. Si nilianza na hiyo, boundary ya districts na provincies, okay? Kuna watu ambao wana shida kuliko nyinyi. Watu wa North Eastern, Kenyatta alifanya mpaka mipaka…. ikapitia kwa sababu alitaka kuenda Somalia, akawaambia nenda lakini mto utabaki akafanya three miles strip, hawa watu hata saa zingine ukisikia unaweza[*avazisa kumukera avaleta* three miles okay? Ili wasiwe na access kwa maji na hawa ni wafugaji. Sasa wa Pokomo, si mnasikia watu wanauwana huko?

**Audience**: Eeh.

**Com. Adagala**: Wa Pokomo wanaishi kwa mto huu na hawa hawawezi kufika na ng'ombe na ngamia kwa mto, ni kitu cha kushangaza. Isitoshe, Garissa town ambayo ni headquarters ya North Eastern iko kwa hiyo Tana River na imewekwa Tana River ambayo iko part of Coast Province. Unaona hiyo si kitu cha kusuluhisha very quickly na district zingine ndio nimewaambia ya Kisumu na Nyando iko huku na huko. Lakini yenu specifically, you want to be in Lugari constituency, also district, let's talk of district and constituency kwa sababu wakikagua hata hizi districts ambazo ziko, constituency itagawanywa, ziko na division already okay.

Tuvumulie tuangalie yale mambo makubwa na tujue maoni yenu yamewekwa kwa boundary Commission, na hakuna watu kukaa, watakuwa wanafanya kazi mumeelewa?

**Audience:** Ndiyo

**Com. Adagala:** Hatukubadilisha constituency wala district yeyote. Hata tulihifadhi, tuliwaambia walitaka wengine ziwe 42 mkasema no, wacha ziwe 70 kwa sababu Suba waliuliza district wakiwa na sababu, Teso waliuliza wakiwa na sababu, Lugari waliuliza wakiwa na sababu, hata Vihiga, Kakamega hata yenyewe ilikuwa kubwa sana, okay?

Sasa hiyo ndio tukasema district tutafanya ziwe 70, constituency na hizo zingine, sasa yenu itakuwa kati ya hiyo mbili.

**Mr. Werengai**: Mimi Commissioner nikiona kwa Constitution hapa, inaonyesha very clearly, hii ikiwa implemented, Constitution hii ikianza kufanya kazi mambo ya Matete pia yatakuwa yamesikilizwa. Kwa sababu ukisoma hapa, I can't read

properly, even my eyes can't read now.

Sisi tunasema hivi, hatutaki constituency mpya kwa sasa kwa sababu tunajua mambo ya constituency haiwezekani kwa sasa, itakuwa baada ya uchaguzi labda. Lakini tunachotaka, ni ku-reverse kwa ile constituency ambaye tulikuwa ndani kwa sababu sisi ndio tulitaka Lugari district na tuka create Lugari district ikiwa na one constituency, kama Mt. Elgon, kama Teso, kama Kuria. So haya makosa ambayo yalishafanyika, sisi tumeandika katika constituency, hii ikiwa a sub district na Lugari as a whole iwe transferred wafikie huko kwetu, simple like that. Asante tena Commission vile mlitengeneza hii.

**Com. Adagala**: Mr. Werengai, I want you to sit down na uandike hiyo, itakuwa hapa lakini unajua itakuwa muda. Na you are a representative to National Constitutional Conference ni nani? Chairman, Councillor ni nani?

**Councillor**: (inaudible) Jane Kauka, hayuko hapa? Halafu na Okia, wako, hao tutawaambia.

**Com. Adagala**: Mnajua hiyo mambo ni ya kupigania, mnajua?

**Audience:** Yeah.

**Com. Adagala:** Yeah, sasa muwe mumepeleka watu ambao watapigania. Wengine watakuwa wanapigania district 42, yaani Kakamega tutarudi, Kakamega, Lugari, Butere- Mumias, Vihiga, itarudi pamoja, 42. Na wanasema wacha niwaachie siri, wanasema hizi district zilibuniwa na mtu binafsi, lakini wananchi, nani alibuni hizo 42? Mkoloni, muwe na hiyo argument Werengai, mkoloni.

**Alphayo Musungu**: Kwa Majina naitwa Alphayo Musungu, mambo yangu ni haya, katika area hii ya Matete, some providers na clerk huandikwa kutoka tu pahali pamoja Malava, hapa Matete division, watoto wetu hawaandikwi, tungelipenda wakati tutaanza kupiga kura ama kwa sasa watoto wetu waandikwe.

**Com. Adagala**: Hiyo ni Electoral Commission, andika barua kwa Electoral Commission uwaambie hiyo. Haya tuendelee, nataka msikie vile Werengai alisema, ikiwa ni, sijui mnanichinjia kondoo au nini, nani anazungumza hapo?

Ikiwa districts 70 zile zilitengenezwa zitakuweko, mtarudi Lugari, sasa suluhisho lote liko hapo sivyo?

**Audience:** Yeah.

**Com. Adagala**: Basi.

**Vincent**: Tutaendelea na sura ya nane, kimya tafadhali.

**Com. Adagala**: (inaudible)

**Vincent:** Tutaendelea na sura ya nane ambayo inaongea juu ya urais. Tutakuwa na utaratibu mpya wa urais ama katika tawi la urais. Kwanza tutakuwa na Rais ambaye atachaguliwa na watu pia akisaidiwa na Vice President ambaye atakuwa running mate. Mamlaka ya Rais pia yako katika sehemu hii. Running mate ama Makamu wa Rais atakuwa cheo moja na Rais,

**Com. Adagala**: Okay, Vice President atajulikana mbeleni kama sasa jana, Uhuru akisimama inafaa jana angetuambia my running mate is so and so kama vile NARC imefanya, wamesema Vice President atakuwa Wamalwa, vile wamepanga, sio ukubali nao lakini mpango. Wakiwa party ambayo itashinda, Charity Ngilu atakuwa. Lakini sio chaguo lao, hilo ni chaguo la Rais, ndiye anasema wewe kwa hii party utabuni … okay. Yeye ndiye atachagua.

**Vincent**: Pia tutakuwa na Prime Minister ama Waziri Mkuu ambaye atachaguliwa na Rais kutoka kwa chama chenye wabunge wengi bungeni, mumesikia?

**Audience**: Mmh.

**Vincent:** Pia kutakuwa na wasaidizi wawili wa Waziri Mkuu ambao pia watachaguliwa na Rais lakini wataidhinishwa na Bunge. Tutakuwa na baraza la mawaziri ambalo litakuwa na watu kumi na tano, watu hawa watachaguliwa, yeah Ministers ama mawaziri, watachaguliwa kutoka kwa watu wenye taaluma tofauti tofauti, ama ujuzi tofauti tofauti. Watu hawa hawatakuwa Wabunge.

**Com. Adagala**: Mlituambia hamtaki Minister of Health kuwa a retired general, Minister wa Health awe daktari eh?

**Audience:** Yeah.

**Com. Adagala**: Yeah, hiyo ndio tunasema, na hawatakua Wabunge, mtu ambaye anang'ang'ania niende Parliament nitafanywa mbunge nikule pesa niwe powerful. Ukienda Bunge, wewe ni mbunge.

**Vincent**: Tutakuwa pia na Waziri wasaidizi kumi na tano ambao pia hawatakuwa Wabunge. Tutakuwa na makatibu wa wizara ambao watakuwa kumi na tano, mmoja katika kila wizara. Waziri Mkuu anaweza kuondolewa na Bunge kupitia kura ya kutokua na imani naye, vote of no confidence, mumeambiwa hiyo, si ndiyo?

**Audience:** ndiyo.

**Vincent**: Pia Rais ataondolewa na Bunge ama anaweza kushtakiwa na Bunge, kitu ambacho knaitwa impeachment. Anaweza pia kutolewa kwa kura ya kutokuwa na maoni. Mamlaka ya watu hawa yote yako katika sehemu hii, mishahara yao itakadiriwa na Tume ya mishahara ambayo iko ndani ya Katiba. Kwa hivyo hawatakuwa na uwezo wa kujipatia mshahara yao, iwapo hakutakuwa na Rais ama labda Rais a-resign ama wakati wa kura, Speaker wa Bunge ndio atakayeshikilia wadhifa wa Rais kwa muda wa miezi mitatu.

Kwa ufupi tu, hayo tu ndio maelezo ya urais. Mtu ambaye atachaguliwa kama Rais lazima

awe chini ya umri wa miaka thelathini na mitano na umri wake usizidi miaka sabini,
awe mtu mwenye amesoma hadi chuo kikuu,
awe na shahada ya decree kutoka kwa chuo kikuu ambacho kinatambulikana, pia ni lazima a -declare mali,
awe mzaliwa wa Kenya na iwapo itapatikana kwamba alipata uraia wa Kenya kwa njia ya udanganyifu, basi atapoteza urais.

**Com. Adagala**: Daraja, njoo tu mbele upange laini hapa. Ukitaka kuzungumza njoo mbele, wengine ambao wanataka kuzungumzia hilo jambo, kujeni nikiwa ninaeleza. Daraja ya kuvuka hiyo, tumesema transitional provision, mtu ambaye amekuwa Rais term mbili au zaidi vile iko kwa Katiba ya sasa, hata-ruhusiwa kusimama.

Mtu ambaye ako na miaka sabini, tumesema ukisimama Rais, term yako ya mwisho, muhula wa mwisho wakati unasimama, uwe na miaka sabini, ukimaliza umefika 75, okay? Mumeelewa? Hapo ni kusema hivi, wale kwa wakati huu wamefika miaka 70 na walitaka kusimama, watasimama kwa wakati huu.

Ikifika mwaka wa elfu mbili na saba, itakuwa lazima uwe sabini mwisho. Mtu wa miaka themanini hatakuweko na themanini na tano, na sabini na tano anasimama, la. Kwa sababu tuliona pia hii itakuwa kutatanisha watu sana au kulete uadui mwingi sana na hatukutaka uadui ujengwe ama tuambiwe mlibuni hii kwa sababu ya mtu fulani. Sasa tunasema wao ambao wanataka na wako na miaka sabini na mbili, nafikiri watu kama Kibaki na Nyachae pengine wamefikia hapo, watasimama wakati huu.

Wakati ujao 70, sio kusema Rais atatoka kwa Urais akiwa na miaka sabini, atatoka akiwa na miaka sabini na tano, lakini akisimama muhula wa mwisho awe na miaka sabini na pia wabunge wa sasa wanaweza kusimama wale walikuwa wabunge. Wale wanaujuzi, nafikiri hata Nassir sasa aweza kusimama tena.

Wanaweza kusimama, sio watachaguliwa, watasimama, kuchaguliwa ni mambo mengine. Sasa wanaweza kujitokeza kwa kura na kusimama lakini 2007 lazima wawe mwisho miaka sabini ndio asimame.

Ikiwa sabini na tatu, hautasimama. Utakuwa umemaliza na kustaafu. Wale ambao wako Councillors, kuna kitu cha elimu na umri, wale wabunge ambao hawana elimu ambayo inahitajika lakini wana ujuzi wakati huu wanaweza kusimama na hiyo miaka. Na Councillors pia kwa sababu tumeweka elimu ya Councillors, wale walikuwa Councillors sasa, Village Council na Locational council, civic council, kwa hivyo ukiwa na umri umepita miaka sabini, bado unaweza kusimama na ni sawa, okay?

Elimu tunayo na ni ile ya kuenda National Council lakini watu walikuwa na mapendekezo, ilikuwa tofauti tofauti. Unajua watu wa Western Province tumesoma, isipokuwa tuna shida siku hizi ya kusoma, lakini watu wa North Eastern walisema, mkiweka

mambo ya Form four sisi hata wengine hatutakuwa na Councillors. Tukaenda Laikipia, huko pokot, tukaambiwa unajua hapa, in our division we have six people who are graduates with degrees. Nikasema ala, hawa ni wale wako kwa familia yangu pekee, wakasema eh, ufikirie, you in your family you have six people with degrees na familia nyingi za Western ziko na watu, watatu, wawili, mmoja lakini huko, division nzima, watu sita.

Wakasema mkiweka hii vitu basi mnasema hawa watu sita ndio watagombea, sasa hiyo ni kwa sababu sehemu ziko tofauti tofauti. Na huko Coast, wale wa Tana River wanakuwa wa mwisho kwa Standard eight na nini, sasa wao walisema standard eight, wa huku wakasema Form four, imewachwa wazi kidogo kwa wakati huu, okay?

Pengine itatokea baadaye lakini lazima tuwe na hiyo elimu kama hiyo ya Primary school halafu tunasema, tulisema Primary na wao waling'ang'ania wakafika Form four basi. Lakini nchi nzima hatuwezi kulinganisha, okay? Hiyo ndio provision za Presidency ya Parliament na National Council, Parliament yote, Assembly na National Council. Mkizungumza Parliament kwa Katiba hii ni milango miwili, imekuwa polygamous kidogo okay. Sasa mnachukua hiyo mlango wa Assembly, hawa ni wabunge wale wako na hiyo ni Lower House, Upper House ni National Council.

Tumeambiwa, Werengai na wengine pengine ambao wanajua mambo haya hapa na Councillors mungeangalia hayo mambo, hata mbunge wenu anafaa kuangalia hayo mambo ya National, lakini hapa hii laini ya National Council, muangalie muone kama ina kazi ya kutosha. Kwanza itakuwa balance of power na checks and balances, hii itakuwa inaangalia hawa Wabunge wasijiwekee mishahara kauli moja, hawa watu wanafanya nini na hawa pia wanaangalia. Unaona? Ili isiwe watu wanafanya tu fwaa wanaenda.

Kama vile President alikuwa ilikuwa kama sasa, si amechagua mawaziri lakini kwa Bunge lijalo, Prime Minister atachagua na majina yataenda kwa Bunge na wajadili, ikiwa mtu ana kasoro fulani atawekwa kando, watatafuta mwingine. Itachukuwa muda na hawa wengine, President akichagua inaenda Bunge, ili iwe checks and balances. Hiyo ndio tunataka ili imla itoke. Tunaweza kuwa na imla, dictatorship of Parliament, imla ya Bunge, inaweza kuweko na sasa hii itakuwa inaangalia huko na hii inaangalia huko. Na Auditor General anaangalia pia na wananchi wanaangalia hii, ya power of recall.

Wanamulika torch kwa Member of Paraliment au kwa Councillor, okay? Sasa hao wote watakuwa Members of Parliament. National Council, National Assembly. Na watu wanatuambia ni gharama kubwa, na tumetoa… Kwanza, Provincial Administration haitakuweko, sasa hiyo gharama yote imetolewa. Na hii ya kuchagua, tumekuwa na hiyo ya Councillors lakini tuliambiwa mtu akitaka kutuwakilisha, achaguliwe. Na watu walikuwa wanasema Councillor na Chief tofauti ya kazi yao ni nini?

Na kwa nini Chief anafanya kazi ya Councillor na kwa nini Councillor hana kitu cha kufanya? Tukasema basi, wacha tuweke hiyo iwe elective na tutakuwa na ma-executive officers kama huyo Town Clerk hapo, okay? Huyu mzee wangu bado

anaendelea kuwa namba one kwa hii darasa, sivyo mzee?

**Major Engwe**: Ndiyo, asante sana. Majina Major Engwe, pendekezo langu ni kwa kazi ya waziri. Ningesema…

**Com. Adagala**: Iwe ya Form two, isiwe ya Form one, fikiria ukifika hapa iwe ya Form two.

**Major Engwe**: Major Engwe, pendekezo, Waziri apewe mamlaka ya kutosha ili kwa ofisi yake tukiangalia tuone anafanya kazi ama iko pingamizi kutoka kwa upande mwingine vile tuko wakati huu.

**Com. Adagala**: Hatutaki mambo ya Form one.

**Major Engwe**: Ubaya hatujui hiyo tofauti.

**Com. Adagala**: Wewe umesema unatoa maoni ya form two Form three itakuwa kwa National Constitutional Conference, Form four itakuwa Bunge. Umekuwa hapa sivyo. Nimesema watu walikuwa wameshatoa maoni na sitaki kusikia kama vile iko wakati huu. Sikilizeni kwa sababu wakati huu na tena nimepeana mfano wa new wine in new bottle, ile tunayo ambayo iko, new wine in old bottle ni hiyo ya kuvuka kwa daraja pekee. Usinirudishe Egypt, unaturudisha Egypt kwa utumwa, hapa minyororo imefunguliwa tafadhali eleweni. Sasa tunataka kusema, tukiwa na minyororo tumeikata sisi wenyewe, sasa tutafanya nini na mikono yetu tukienda mbele.

Usituambie tulikuwa tunafungwa minyororo, rudisha hiyo minyororo, unataka urudishe minyororo?

**Major Engwe**: Hapana.

**Com. Adagala**: Yeah, sasa sema jambo lako kwa kuendelea mbele. Useme jambo lipya. Sema jambo lako kwa Katiba mpya, Kenya mpya. Simama hapa, mambo ya zamani tuliiweka …

**Major Engwe:** Kwa Katiba mpya, tunataka kila mtu akipewa kazi awe na uwezo wa kudumu.

**Com. Adagala**: Very good. Hasa waziri, sitaki mambo ya Form one, mnaturudisha nyuma kwa minyororo, nataka yale mambo ya mbele, hiyo ndio point.

**Opanda Wamalika:** Jina langu ni Opanda Wamalika. Rais ambaye anachaguliwa isiwe lazima awe na degree lakini anaweza kuwa na an equivalent kwa mfano awe a finalist katika professional examination kama CPA, ABII na other professional examinations.

**Com. Adagala**: (inaudible) tulichukua maoni hayo na tukaweka maoni yetu pamoja. Sijui kwa nini mumekuwa kichwa ngumu. Tuliweka pamoja yale yalikuwa ya watu wengi na watu wengi walisema degree, wamechoka na mambo ya kutoelewa na pia dunia imekuwa tendewani, globalization, vitu vingi vinatendeka. Wanataka mtu ambaye anaelewa.

Rais atakosaje kuwa na degree na MP ana degree? Asante sana kwa maoni yako kwa sababu ume…..

**Opanda Wamalika**: Okay asante.

**Cllr. Nalyanya**: Mimi nina maoni mawili. Ya kwanza, Rais hafai kuwa mjumbe ambaye anawakilisha constituency.
**Com. Adagala**: Uko kwa Form one, tuendelee …

**Cllor. Nalyanya**: Hiyo mumemaliza. Ya pili, haya maneno ambayo mumesema mawaziri wasiwe wajumbe, mimi ninaona kwamba ni heri mawaziri wawe wajumbe ndio wafanye kazi yao kwa wananchi vizuri.

**Com. Adagala**: Na wale ambao hawana, eh Councillor, simama hapo useme vile unataka. Na unaruka ruka na wewe ni Councillor. Na wale wabunge wao si waziri, watu walituambia- Councillor soma hii report- watu walisema, mtu akiwa waziri anapeleka vitu vyote kwao, au akiwa waziri anasahau kwao anafanyia tu taifa, wakasema, unajua Sabatia wanasema hivyo. Wanataka mbunge pekee, hawataki mambo ya (inaudible) wanataka tu mjumbe, wamechoka na hayo mambo mengine. Unajua unachoka nayo mwishowe?
**Audience**: eh.

**Com. Adagala**: Si mimi ninasema, enda Sabatia. Wanasema wacha awe tu mbunge, asiwe na loyalty kwa mtu mwingine, wamechoka na hiyo na inachokesha. Ikiwa hata mnapata nini, mwishowe mnachoka kwa sababu mnataka tu mjumbe kuketi naye, mzungumze naye, aende kusema watu wangu wamesema, na hakuna mjumbe atapeleka jambo bungeni bila kuuliza the people of power, mjue hivyo? Unajua watu wanaenda kule tu wanaropoka mtu vile anataka tu, anaenda kule, wengine wanasema, beat a woman to show a lot of love, let's beat the men also so we can show them the love we have for them. Wanaropoka tu kule, hawajauliza wakina mama waliwapigia kura na wakina mama ndio wanapiga kura, halafu wanaenda kule wanasema wacha wapigwe, ndio upendo..

**Cllr. Nalyanya**: Labda kuna criteria ambayo inatumika kuchagua mawaziri, hiyo hamujatuambia.

**Com. Adagala**: …. na pia itatengenezwa na Bunge, okay? Commission haiambii mtu jambo, we are clerks, I wish you would know. Yetu ni kuandika, we are a secretariat in the end, we are not even like the Commissions which we have put here, which are really strong. We are just clerks, fanya hii tunafanya, fanya ile, sheria ndio hii fanya, okay? Ninyi ndio mtatuambia hata mnaweza kuketi na watu wengine wa siasa na museme atachaguliwa vipi.

Lakini ya kwanza itakuwa by profession, land economist, economist awe finance, sio watu wanaenda kule halafu wanaanza kujifunza kazi. Unaweza kuwa hata na roho nzuri, lakini pia health awe Doctor au mtu ako kwa medical administration. Na wata-apply halafu majina yatakaguliwa kwa Bunge, Bunge ndio litafanya hiyo interview. Judges pia, itakuwa application to

Judiciary Service Commission, okay?

**Vincent**: Sawa tutaangalia sura ya tisa ambayo inaongea juu ya mahakama.
**Interjections:**

**Com. Adagala**: Mnakubali?
**Audidence:** Tumekubali.

**Com. Adagala**: Inafaa mkubali kuzungumzia mahakama hapa sura ya tisa, unajua sasa tuko gizani sasa mtasikiliza tu eh, mnakubali?
**Audience:** Yeah.

**Com. Adagala**: Kama haukubali, kwanza utoe hiyo ribbon yellow kwa sababu hauungi mkono okay? Mlikuwa na Chief Justice huko sasa mtatusaidia hapa. Sisi hatujawahi kupata Chief Justice hata Judge.

**Vincent**: Sehemu hii inaanza na maadili muhimu kuhusu uhuru wa mahakama. Mahakama pia imepewa jukumu la kupitisha ama ya kufafanua maswala ya Katiba. Utaratibu wa mahakama mpya sasa umebuniwa, utakuwa na mahakama ya juu zaidi ambayo itaitwa
Supreme Court, hiyo sasa ndio itakuwa mahakama ya juu zaidi. Mahakama hii itasikia kesi za rufani kutoka kwa mahakama za chini, mahakama hii itakuwa chini ya Jaji Mkuu na Majaji wengine sita.

Pia tutakuwa na mahakama ya Court of Appeal, mahakama ya rufani, mahakama hii itasikiza kesi za rufani kutoka kwa mahakama za chini yaani High Court. Mahakama itakuwa chini ya Rais wa Mahakama na Majaji wengine kumi. Pia tutakuwa na mahakama ya High Court ambayo itakuwa chini ya Principle Judge na Majaji wengine hamsini.

Pia sura hii inabuni Tume ya mahakama ambayo itachagua mahakimu. Ma-jaji wa mahakama ya Supreme Court, Court of Appeal na High Court watachaguliwa na Rais lakini wataidhinishwa na Bunge. Na mahakimu watachaguliwa na hii Tume ambayo ni Tume ya mahakama.

Pia kutakuwa na office/ofisi ya Mkuu wa Sheria lakini mamlaka ya Mkuu wa Sheria sasa yamepunguzwa. Kutakuwa na ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye atasimamia mashtaka yote ya serikali ama mashtaka ya hatia za aina mbali mbali.

**Com. Adagala**: Kwa ufupi ni kusema hiyo ofisi ya Amos Wako-pengine wakina mama hawaelewi na wazee wanaelewa kwa sababu wanakaa kwa siasa- hiyo ofisi imegawanywa mara mbili. Kwa sababu kuna kazi na sasa Attorney General, advisor to the government, yule ambaye anashauri serikali atakuwa tofauti na yule ambaye anafanya hii kazi ya ku-prosecute mtu

akifungwa. Ni kazi ndogo na inafaa ifanywe na mtu mwingine, okay?

**Vincent:** Na kwa ndugu wetu Waislamu, kutakuwa na mahakama za Kadhi tofauti. Mahakama ya juu zaidi itakuwa mahakama ya rufani ya Kadhi ambaye itakuwa chini ya Kadhi, na Kadhi wengine ambao watateuliwa na hii Tume ya Mahakama. Pia mawakili wametambuliwa katika Katiba, wako na jukumu la kuilinda Katiba na pia kulinda haki za binaadamu.

Vitendo vya ufisadi vya mawakili vimetupiliwa mbali katika Katiba hii. Kwa muktasari tu, haya ndio maeleze ambayo yako katika sura hii.

**Com. Adagala**: Kitu kimoja, wacha niseme kuhusu hii seat ilikuwa ya Chesoni. Sasa alipoaga, ilikuwa kama tuseme Headmaster wa Secondary school anaaga, halafu wanachukua yule ambaye amesomea kuwa wa primary school wanamwambia basi wewe utakuwa Headmaster wa secondary. Kimasomo haiambatani halafu wale walimu wa secondary watakuwa na masomo zaidi kuliko Headmaster. Hiyo ndio iko sasa, hii mambo ya Chunga na Chesoni, kwanza Chesoni alienda kwa Electoral Commission na Chunga akachukuwa hiyo, sasa hiyo si sawa okay?

Na hawa watu wote wako chini ya Attorney General, sasa wanataka hiyo ofisi iwe tofauti, hiyo ya Kidula, ya kina Chunga, iwe tofauti.

**Vincent**: Mwisho kabisa kuna kitu nimesahau. Wananchi ambao hawawezi kulipia huduma za mawakili, kutakuwa na afisi ya Public defender ambaye inasikia malalamishi yao.

**John Kariuki**: Okay, jina langu ni John Kariuki ningelitaka pia Katiba hii na mahakama ya Ki-Katiba yaani Constitutional Court to handle human rights cases halafu pia tungetaka Katiba hii iwashughulikie wale ambao walifungwa na kupata skills ili waweze kujisaidia kuendeleza mafunzo waliyopata katika jela. Serikali iwape kitu kidogo ili waendelee na wasirudi kuibia watu.

Pia tungelitaka serikali pia iwape conjugal rights, yaani waweze kukutana na spouses wao, hiyo iandikwe na ijitokeze kabisa ili tuweze ku-control ukimwi.

**Com. Adagala:** Ukimwi unakuwa controlled na …Wengine wanasema tusiwe na urithi wa wanawake kwa sababu hiyo ndio inaeneza. Pengine ni njia ingine lakini ni rights, wanasayansi wapate matibabu au wafanye nini, hiyo ni conjugal rights na iko kwa Katiba. Ile ulisema ya Constitutional Court, Supreme Court iko na Constitutional matters ndani na iko na Constitutional Commission, okay? Kuna hiyo mbili, jambo lako la kwanza?

**John Kariuki**: Ilikuwa Constitutional Court.

**Com. Adagala:** Na ya pili?

**John Kariuki**: Ya pili imekuwa conjugal rights.

**Com. Adagala**: Ya tatu?

**John Kariuki**: Ya tatu imekuwa soft grants kwa wale wafungwa ambao wametoka jela.

**Com. Adagala**: Okay, watu wengine walituambia hawa watu wafungwa kwa nini mnawapa skills, hata juzi walisema tu, hawa watu wamefanya hatia, kwa nini munasema wasome. Wana haki ya kupata skills hapa, okay? Na hiyo sasa ni haki, kwa sasa ni kama lazima na kama purnishment lakini mambo ya nini, hata walisema wale wanapata masomo, kuna economic and Social Council ita-handle hiyo, okay? Haya, iko hapa.

Ninajua mko na jela hapa ndio mnasema hiyo mambo.

**Opanda Wamalika**: Mimi ni Opanda Wamalika. Ninapendekeza katika Katiba tuwe na koti za ki-kristo. Christian court ambazo zitakuwa zikisuluhisha mizozo ya Kikristo ikitumia bibilia na Katiba za makanisa ya ki-kristo ambazo ziko Kenya.

**Com. Adagala**: Unajua wakristo wanakitu kinawatatiza, unasema court na bibilia imesema msiende kotini, unajua wamesema hivyo? Msipelekane kotini, inafaa muite kitu kingine, wenyewe mtafikiria. Na ya pili mna hiyo kitu kinaitwa a peace gift, a period of praise after Christ died okay. Sasa mfikirie hapo, pengine sio sheria kabisa, kuna principles, do unto others as you like them to do unto you, love your neighbors as you love yourself, hizo principles, hizo zote ziko. Hata vile inafaa tu-change hicho kifungo cha kumi, hiyo yote. Ninajua wengine wameenda, Pastors wameenda, wa kuu wa kanisa wameenda, mtu wa Salvation Army bado ako hapa?

**Audience**: Alienda.

**Com. Adagala:** Okay watu wengi wanasema, I don't have enough money for tithing, inafaa wafundishwe uki-tithe ndio unapata. Hii vitu ni vya Mungu, halafu tu, ninatoa tu sadaka, lakini tithe lazima utoe ndio hiyo sadaka iongezwe. Hawajui na ni kwa sababu kwa kanisa hawafundishi vizuri kuna hizo vitu, ni principles. Kwa sababu it is said, you are in a time of break, it is very difficult to say these other things. Wa-mama naona wameenda, wamefunga maleso wanaenda.

**Joseph Mabutsi:** Tukirudi kwa mahakama ya mabusi, hata ikiwa umepigana, unaenda kufungwa pamoja na muuaji ama mwenye amebomoa, sasa ukitoka pale, pia wewe utakuwa umejifunza kuua. Ningependa ikiwa umeiba ufungwe kando na muuaji na mwenye kupigana, hapo itakuwa vizuri.

**Com. Adagala:** Na tena tumesema jela lazima iwe na makao mazuri, wamesema asubuhi leo tulikuwa na mtoto huko Machakos sijui Kitui, ambaye aliua mtu wa miaka kumi na tatu na mahakama ilishtuka, huyo mtoto alifungwa na watu wazima na mahakama ilikuwa imesema asifungwe na watu wazima. Lakini unajua polisi hata hawajui mambo ya mahakama, pengine

hawa wazazi wakija kumhonga ndio huyo atawekwa kando. Lakini ile umesema… ameenda wapi huyo mtu? Yes, hard core criminals wanafaa wawekwe tofauti, sasa hiyo ni kitu kizuri lakini Parliament ndio itafanya hiyo na tutaweka hapa kwa sababu ni maoni. Haya hiyo ndio mwisho huyo mtu amesimama.

**Cllr. Nalyanya**: Councillor Nalyanya tena. Mimi ninaonelea Katiba yetu mpya iwe na Subordinate court kwa kuwa sasa tuko na Village, Locational na District Councils, hizi courts zije kwa location kusudi, ni expensive sana kwa wananchi kutoka kama hapa mpaka Eldoret, sasa ndio mahakama yenye iko karibu kabisa. Kwa hivyo walete karibu na wananchi.

Ya pili, tuwe na Customary law court, kusudi tuko na mambo fulani ambayo ni purely custom na inaenda kotini, unakuta watu wanatukanana huko, kwa hivyo tuwe na hiyo koti.

**Com. Adagala:** Wewe ni rafiki yangu kabisa, nilipigania hili jambo na kuna nchi zingine kama Tamil tigers, walisema kwa TV, we have made our district courts and they are according to our traditional indigenous law. Unajua hii mahakama tunaendesha ni kitu cha ukoloni, na ilifaa itoke lakini vile tulikuwa hapo pengine tukipigania hivi inaweza kuvunwa na wewe uandike. Where is this person? Kwa nini mnatoa maoni halafu mnakimbia.

**Cllr. Nalyanya**: Niko hapa.

**Com. Adagala**: Njoo hapa, wewe ni mtu ambaye anajua kuandika vizuri eh Councillor, you draw the chart and you put the reason, what each level of the court will be doing. Unajua watu hawajui, kuna watu wamefanya submission, memorandum na map ya Kenya ndani yake, vile inafaa Kenya igawiwe na vitu ndani. Wanaweka chart, so don't just say, you are a literate person, write it down, it shall be there and it is easier than waiting for her to transcribe halafu tutaona. Fanya hapa, tuweke hapa. Traditional matters should be, but this I think would be up to the district because most districts zinafikaa hapo, district ingine ina mila ingine okay? Isipokuwa Jaluoland na huku Luhya land, lakini unajua saa zingine kama za wa Teso ni wao ndani, sasa inafaa ifike kwa district level.

You should do like that. Even Kikuyus I think they are slightly different, hawa wa Kiambu na wale wa Nyeri na Nyandarua.

**Esther Werengai**: Jina langu ni Esther Werengai. Mimi ni Chair niko kwa laini ya koti ya wa- mama, ningependa wa-mama wawe na koti yao kwa location ya kumaliza hii maneno madogo madogo ya wa-mama kurudi chini kwa sub-location. Halafu tena kwa divisions, tuwe na wa-mama ambao wanaweza kusuluhisha shida za wa-mama pekee yake.

**Com. Adagala**: Okay, mama kuna division, simama hapo tu kidogo. Kuna division na mahali kwingi division ni constituency, sasa hiyo ni laini ya National Assembly lakini kama hapa mna divisions mbili. Kuna zingine pia ni divisions mbili lakini hii ni laini ya hao Wabunge wa National Assembly. Kuna laini ingine na umezungumzia mara mbili bila … Vitu vipya na Kenya mpya okay?

Kuna village, sub location, hiyo ndio village yenyewe halafu kuna location. Mama haujasoma leo, we have two Houses; House moja inatoka kwa constituency inaenda National Assembly, hiyo ndio pia ina division okay? Kuna nyumba ingine inaanza village, hiyo ndio sub-location, location, district, National Council, Baraza la taifa. Sasa hauwezi kuvuka, sema laini ile vile unataka ikae, umesema village ni vitu vidogo vidogo, sawa halafu mpaka location, halafu iende mpaka wapi?

**Esther Werengai:** Division.

**Cllr. Nalyanya**: You are mixing.

**Esther Werengai**: Nimesema tu Location na division.

**Com. Adagala**: Madam, toka kwa civic ya zamani, hii ni civic ya sasa na utasimama hapo mpaka utaelewa. *Inyumba nene vagiranga National Council, inyumba nge vagiranga* National Assembly, division iko upande wa *nyumba nge*. Ukiwa na wa-mama wawili kwa boma, hauwezi kuchanganyisha. *Nyumba nene* inaanza na village inaenda sub-location, location, district, National Council. *Nyumba nge* ni hiyo ya constituency, National Assembly.

Kama huyu mama wa National Assembly ako na watoto, kwanza tuko na Province for co-ordination, sasa huyu ana watoto wanne, na huyu ana mmoja. Unaona, anaenda tu kutoka kwa… Haujaelewa? Ndio hauwezi kukuwa na koti ambayo iko village na sub location na location halafu division, infact division iko upande huu.

Tumeunda nyumba mbili ya Bunge, na kutoka-chini nilisema sio huko juu peke yake- kutoka chini inaenda mpaka juu, niambie vizuri kinaganaga, ulitaka koti?

**Esther Werengai**: Koti ya wa mama.

**Com. Adagala**: Sio family court?

**Masinde:** Mambo ya division ndio hajaelewa, division inapatikana wapi?

**Com. Adagala**: Wacha nikuambie, division, this will probably work in your favour, division is part of Provincial Administration. Unajua hivyo, umeelewa ndani kwa ndani?

**Esther Werengai**: Mmh.

**Com. Adagala:** Pengine itamsaidia hapa ili isiwe hii kitu cha kugawa, mtasema tuko constituency hii, inafaa iwe kule kitu kama hicho au district inapita okay? Mama umeelewa kuna nyumba mbili? Mama mkubwa na mama mdogo, hauwezi kuchukua vitu vya mama mdogo na uweke kwa nyumba ya mama mkubwa.

**Esther Werengai**: Sijaelewa sana.

**Com. Adagala**: Umekataa.

**Esther Werengai:** Kwa sababu mimi …

**Com. Adagala**: Umekataa, civic …

**Esther Werengai**: I am confused.

**Com. Adagala**: You want to be confused, civic mpya, new skin new wine,

**Cllr. Nalyanya**: I think the problem you have is in court see is dealing with judiciary and she wants a public court.

**Com. Adagala**: Yes, but she is saying where it should be and now she is saying, location and division, no inafaa uende sub-location, location, district.

**Esther Werengai:** That is the thing.

**Com. Adagala**: But how far do you want it to go?

**Esther Werengai**: From location .

**Com. Adagala**: Location down?

**Esther Werengai**: Location down is where we have a lot of problem.

**Com. Adagala**: I am asking you is that what you want?

**Esther Werengai**: Yes please.

**Com. Adagala**: Thank you very much , lakini hiyo civic ujifunze, mzee atakufundisha akuambie. Okay nafikiri nyote mumeelewa, sio mama peke ….

**Cllr. Nalyanya**: Lakini mimi Madam mambo ya division imekujia upande wa constitutency.

**Com. Adagala**: Division ni provincial administration. Division, Councillor, ni administrative unit, ni Provincial Administration, she is mentioning it, and I am telling her it is fair but actually she has made me realize that we should say that is part of Provincial Adminsitration. So eventually, division will probably go, I am saying probably, it will go, it is a part of Provincial Administration. Hamuelewi hatuta-kuwa na DO, DC, na PC, haitakuweko, so division wakili ameniambia …

**Vincent:** Labda mtaelewa zaidi baada ya kupitia mapendekezo ambayo yako katika sura ya kumi (2). Mapendekezo juu ya serikali za mashinani.

**Com. Adagala**: Okay, endelea kijana. Hii ndio ilikuwa mfupa mgumu sana, hiyo ya Bill of Rights niliwaambia ilikuwa rahisi lakini hata hiyo ya Presidency ilikuwa, hiki kitu kiliundwa vibaya, lakini kile kitu kilikuwa kimechukuliwa na tumeirudisha ni hiyo devolution. Waliita majimbo, watu wakasema hatutaki majimbo haifanyi kazi na haikufanya kazi kwa sababu mtu alichukua

nguvu yake, *valifogoi sana* ikavunjika miguu, mikono.

Tape ends, words lost……otiende, federalism ilienda wapi? Akasema, it was murdered, iliuawa. Sasa kuna kitu wacha niseme wale wataelewa wataeleza wengine. Kuna kitu kinaitwa capitalism. Capitalism ndio watu wanasema hapa kwa sababu sisi hatujakuwa ujamaa, hiyo mambo kama ya Tanzania au ya China. Na sasa imekuwa ukiwa na capitalism kile inafanya ni kutengeneza federalism, hapo mzee Werengai na wazee wengine wako hapa, hapo ndio Mboya alikosana na wa America.

Ukiwa na capitalism, iwe na federalism kwa sababu ndio human say of capitalism. Vitu vinaletwa chini ili wakina mama pia wafanye biashara, vijana wafanye biashara wapate kazi, wazee wawe na hilo jukumu pia la kufanya na wawe na jukumu la kuamua, ni devolution hiyo.

Ile ilifanyika Lugari na Vihiga ilikuwa decentralization, na wanasema bringing services closer to the people lakini vile mnaona hata hapa hamkua na jukumu la kuamua, hata sasa mkitaka Malava forest mfanye nini, hamuwezi,ikiwa hata shule, hamuwezi. Kwa sababu hamna nguvu, nguvu zenu zilitolewa lakini wakamletea hope ya district, bringing services closer to the people. Hiyo ni decentralization, ikiwa serikali ya imla pia inakuja karibu, ikiwa ile nzuri kidogo kidogo, pia inakuja karibu lakini nyinyi wenyewe hamna njia ya kuamua.

Deconcentration ni kama hiyo ya President, too much power concentrated, sasa tunaifungua. Na ikifungulika pia inaingiana na devolution kwa sababu lazima iende mahali, *ni groupu siongo no ovemu na sienyu, vachinya yaha vachinya wamanya lichuna lichura mmgunia, liremwa?*

**Audience**: eh.

**Com. Adagala:** *ni iyo,* wanaweka wanaweka sasa ukitoa hiyo, hii maji itateremka mpaka itafika pahali pa mwisho, hiyo ndio tumeachia President, tukamuambia hiyo ndio power yako. Hii ingine itarudi kwa wananchi, ingine iende kwa Prime Minister, ingine iende kwa Parliament, ingine iende kwa mahakama independent, okay?

Shida ya mahakama hawa, hawataki kuwa independent, sijui wao ni wakina nani, wanataka wawe dependent kwa yule mtu aliwapa kazi. Sasa tukifika hapa, hiyo ni deconcentration au ni kama ukiwa na quencher, hauwezi kuweka tu kwa mdomo, hata haitakuwa tamu, itakuwa kali, jaribu quencher ukinywa kama iko hivyo hata … lakini unaweka kiasi kidogo halafu unaweka maji. Hiyo ndio tumefanya ili watu wote wapate na sio mtu mmoja anakunywa quencher ya chupa peke yake.

Sasa devolution inamletea deconcentrated power chini lakini sio inaingia ndani yetu, inalete tu chini. Hata tulikuwa na arguments na Councillors wengine kwa sababu walikwua wanasema, they should be given power over land. Tukawauliza, tukawauliza na tukimpa hiyo power, wananchi watafaidika vipi? Wakasema no, no, just give us the land. We told them yeah, but what we know, we will give you the land and then you keep it to yourself na haitaenda kwa wananchi.

Sasa tunataka ifike kwa wananchi, hiyo ndio devolution. Power inakuja, nguvu inafika kwa wale wenye nguvu, si tulisema mumetengeneza Katiba, nguvu ni yenu? Sasa hii pia nguvu inarudishwa kwa devolution, sasa mtakuwa na uwezo wa kuamua, kushiriki, infact this kind of devolution, this kind of federalism ni shirikisho, participation. Lazima mu-participate kwa hiyo serikali ya kuchagua hiyo. Unajua sasa, they bring allocation to you, then they appoint the chief, you see that. Lakini sasa mnasema tunataka tu-elect hiyo ndio power, wananchi wanajua wenyewe hatukutoa hii mambo pahali pengine, walituambia we want to elect. To do that, we have to put a structure that brings power there, the elections, chief akifurafura akifanya au yule mtu ambaye amechaguliwa, power of recall, mnamwita mnamuambia, "wewe, unafanya hivi, umepotelea kwa wasichana. Iko wengine wanafanya hivyo hata wanakuwa kwa magazeti, kitu kama hicho, inakua service, sio power. Hizo positions ambazo ziko sasa ni za power, nataka service, mtu ambaye ako chini ya wananchi sio juu ya wananchi, sasa hiyo ndio devolution. You participate, make decisions, have management like over hii miwa, mnasema sasa tunapanda miwa na ndizi, mta-decide halafu mna-benefit kama hiyo miwa pia ikiwa na bei, itatoka ile ita-benefit hao, hata mahindi ndio inakuwa huku.

Sasa mnasema factory ya mahindi, kunayo Western moja?

**Audience:** Hakuna

**Com. Adagala:** Iko North Rift? Iko Nyanza?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Adagala**: Hakuna, factory iwe hapa, hiyo ndio value added. Mna-produce halafu mnasaga, halafu mnapeleka na kazi iko hapo, ni factory. Sio hii zingine zenye zimejazana, ni factory. Kuna factory ambaye inatengeneza jogoo, mtu anajua kule iko?

**Audience:** hapana.

**Com. Adagala**: Some kwa packet ya jogoo utaona iko wapi, ya jimbi iko wapi, hiyo ni kazi nyingi sana na iko mahali kwingine, iko Nairobi. Hiyo sasa deconcentrated, mahindi inatoka huku, watu wanakuja wanachukua na ma-lorry, watu wa nje, mnapata malipo ambayo hata hayafiki kwa ile ya fertilizer, inaenda Nairobi, inasagwa, inarudi. Bei imekuwa *kongo*, hata wewe mwenyewe hauwezi ku-afford na wewe ndio ulilima hiyo, na mtoto wako hajapata kazi hapo. Unaona, hiyo ndio deconcentration siku hizi. Ni structure ya devolution, ni district, wengine tulitaka province lakini ikaja district halafu tukasema basi, kama ni district, 70 districts, tukakwama hapo.

Na kwa sababu walitaka district halafu iwe constituency, hawa watu hawakutaka province, tukasema ikiwa district peleka, haya. Zungukana hapo tukasema 70, hiyo sasa ni benefits, itakuwa factory hapa, wakina mama watapata kazi ya kufanya, vijana, wazee watapata, hawatakuwa wanazunguka na hii magari unaona inaenda Nairobi. Watakuwa wanapata kazi hapa, factory ya miwa iko hapa lakini headquarters iko wapi?

**Audience:** Nairobi.

**Com. Adagala:** Yeah, tunataka headquarters hapa na pale hata wakiguza ile, hapa na Kisumu ijengwe, okay? Hiyo ninamwambia, sisemi lazima, nyinyi wenyewe mtasema. Na bei ya sukari, kwa nini iwe bei moja na Nairobi na sukari inatengenezwa hapa? Makaratasi haya, miti inatoka Lugari inaenda Webuye, Bungoma district, makaratasi yanatengenezwa yanaenda Nairobi ndio inakatwa halafu ndio wanakuja kukuuzia. Ile bei ya kitabu cha mtoto ni ile ile Nairobi, kwa nini na factory iko hapa? Tuseme hiyo factory iko hapo, lakini tunafaidika kazi peke hata sio, na watu wa Lugari wamelalamika miti inakatwa, Councillors walisema hata walifanya maandamo, sivyo?

**Audience:** yeah.

**Com. Adagala:** Yeah, you are cutting our trees, why are you …lakini wakasema lakini si yenu. We want them? Wakasema hamtapata, wakasema kwa nini? This is private, hawa watu walipewa hii eneo, acre mbili, tano, kumi, wapi? Kule Land office Nairobi na hawajulikani kwa watu wa Lugari, okay? Sasa hiyo itakuwa kama miti iko hapa, tu- benefit. Hata vitu vingine angalau hiyo imetokea in a factory, kuna madini hapa chini, gold. Wengine wakasema paraffin, nyinyi ndio mlituambia? Hiyo yote pia lazima mu-benefit, mu-exploit, mfanye decision, mu-benefit.

Hapa kuna kitu kinaitwa viazi tamu, *nikhulanga mabuoni ka valogori, mulanga kindu ki*

**Audience:** (Inaudible)

**Com. Adagala:** Mnaita nini?

**Audience**: *ka vanyala*

**Com. Adagala**: ka vanya.. okay, haya hiyo iko hapa lakini bei yake watu wanakuja na lorry wanapeleka na hatuna hata ushuru juu yake ambayo itabakia hapa. Tafadhali msikie devolution, mjue ni ya ku-benefit, okay. Wacha kijana apitie tu technically juu juu na tuendelee.

**Vincent:** Kutakuwa na serikali ya kijiji, serikali hii itakuwa na wanachama kati ya wanachama sita na kumi, wasiopungua sita na wasiozidi kumi. Na pia kutakuwa na serikali ya kata ambayo itakuwa na wakilishi wawili kutoka kwa kila kijiji na mmoja wao atakuwa ni mwanamke. Pia kutachaguliwa administrator wa kata ama administrator wa location ambaye atachaguliwa na wananchi directly, pia kutakuwa na serikali ya wilaya ambayo itakuwa na wakilishi kati ya ishirini na thelathini, kutakuwa na district administrator ama mkuu wa wilaya ambaye atachaguliwa na wananchi.

Pia kutakuwa na serikali ya mkoa ambayo itakuwa na wakilishi kutoka kwa kila wilaya na wakilishi hawa ndio watakaochagua mkuu wa mkoa ama Provincial Administrator. Yafaa tuelewe ya kwamba serikali hii itakuwa na uwezo Fulani; uwezo wa kupitisha sheria na uwezo wa kuchukuwa kodi kutoka kwa wakaazi wa sehemu hizo. Pia serikali hii itasimamia mali ya asili ambayo inapatikana katika sehemu hiyo. Serikali hii pia itakuwa na mamlaka ya kuajiri maafisa ambao watahudumu katika serikali hizi lakini pia serikali kuu itapewa, imehimizwa isaidie serikali hizi katika kuajiri maafisa ambao wanahudumu katika

serikali hizi.

Kijiji ni nini katika sura hii? Kijiji itakuwa ni eneo ambalo saa hizi linaitwa sub-location, kwa ufupi tu hayo ndio maelezo.

**Com. Adagala:** Kwa ile approach I had taken, let me tell you marehemu mzee Solomon Adagala aliniambia, alipokuwa at indepedence, Kakamega County Council, hii yote ya Lugari, hii ndio ilikuwa the richest in the country,
**Audience**: North Nyanza.

**Com. Adagala**: North Nyanza, okay akaniambia hiyo ndio ilikuwa the richest. Nikamuuliza, mlipata wapi pesa? Akasema kwa mahindi, kwa vitu, na wakati huo miwa ilikuwa haijakuja. Panpaper ilikuwa hajafika, akasema hata walijenga Bukhungu stadium, nafikiri ndio ilikuwa ya kwanza, kwa sababu wazungu hawakuwa na haja na stadium, walikuwa wa-chache okay. Wakajenga hiyo na wakataka pia kununua mali ng'ambo, fikirieni.

**Audience:** We were buying shares.
**Com. Adagala**: Yes, I want someone to describe that day, kwa sababu mzee alisema anataka pendekezo lake alikuwa mgonjwa wakati huo, alisema anataka hii sehemu yetu yote irudi kwa hiyo hali ya utajiri na mzee Odieda akaniambia, huu umaskini tunao ni kitu wanaita planned poverty, imekuwa planned tuwe maskini. Ni mpango, sasa minyororo hiyo tuvunje na si ngumu. Watu wanasema ati poverty elleviation na hawajafanya kitu, poverty allievation itatokea wapi? Okay. Sasa hiyo ni kitu muhimu, muhimu sana, muelewe tutakuwa na serikali kwa district. Mama Esther, inafaa uelewe hii ufundishe wanawake, new civic, okay? Itakuwa hivyo.

Devolution ni kitu muhimu kwa sababu sio serikali kuwa karibu pekee, huku Vihiga tuna district na watu wengi wako hapo, wacha nimuambie. Mbeleni tulipokuwa division ya Vihiga, ulikuwa unaenda hapo headquarters,(inaudible) sasa ukienda hata haujui hawa watu wako hapo kwa district. Na wengi ni watu wa Nyanza ambao wanataka wawe karibu nyumbani lakini sio mbali sana, sio mbali sana sio karibu sana na ni watu karibu kustaafu. Na kile nimeambiwa na officers hapo wenyeji wanasema, they frustrate the projects okay? Wale watakuwa kwa district watakuwa kwanza kutoka kwa hiyo district, okay?

Kama watu hawajasoma sana ndio mtu atatoka kwingine lakini hii mambo kama hii nilisikia ati watu walihojiwa mambo ya Army au ya police inside State House, na sio Bukhungu stadium, watu kutoka mbali, hiyo haitakuwa tena.

Watu watakuwa wanaajiriwa pale, hata watu wamesema police must come from the area so that you know them. Na wapate recommendations kutoka kwa locaton, na pia kutoka kwa church, wajuliane ni wakina nani.

**John Kariuki**: Jina langu ni John Kariuki, ningelipenda kusema kwamba Western Province ndio ina mito mingi sana ambayo ni source ya Lake Victoria. Lakini unapata kwamba kitu kama stima hasa Western ni chache sana kulinganisha na area ambazo

hazitoi maji ya kutengeneza sitima.

Halafu unaona pia kwamba River Nzoia ni main source lakini watu ambao wako katika Western region hawakubaliwi kutumia ile river Nzoia kwa irrigation purpose ilhali kule Eqypt wanatumia yale maji na wanatengeneza stima. Ukiangalia Uganda …

**Com. Adagala**: Pendekezo?

**John Kariuki**: Okay napendekeza kwamba, tuwe na uhuru wa kutumia rasilmali ambazo tuko nazo hapa, halafu pia tuwe na vitu kama vituo vya watalii ambavyo ni mali katika Western region kwa sababu tuna hizi sites hapa. Halafu tunalima miwa, Sugar board iwe Western Province, halafu Western watu wamesoma, Ministry of Education iwekwe hapa, area nyingine ambaye ina vitu ambavyo ni tofauti tofauti, hizi ministries zitofautishwe kabisa halafu hawa watu waweze kutembea Kenya nzima, pesa ambazo wanalipwa ziweze kupatikana kwa hawa wa-mama ambao wanauza mboga.

**Com. Adagala**: Eh mama mboga, hata mimi ni mama mboga, nikikosa kazi ninafanya ya mama mboga. Sasa hiyo mambo ya maji, hii mvua mnaona inateremka hata saa zingine tunasema *iviki*, lakini mkienda North Eastern mtawahurumia. Councillor mwingine aliniambia, mama kwenu kuna maji machafu, kama iko hapa eh niambie. Kwa sababu alifikiri kwetu ni Nairobi, nikamuambia kwetu ni Kakamega, kule mvua inanyesha usiku na mchana, na hiyo ni kanuni ya Mungu, siwezi kusema kwa nini. Mungu aliweka mvua Western na hivyo sasa itakuwa nikijifanya mimi ni mkubwa wa Mungu najua vile alifanya. Lakini nyinyi mnamchanga hapa, *mueke vulahi vulahi mwaka ni vulavu……………* tukasema hii ni rasilmali kwetu hakuna kwa sababu ni udongo wa kulima pekee, ikiwezekana muwe munalete na sisi tunampa sukari, kwanza huko sukari ni shilingi mia moja.

Na pia wanaweka nyingi kwa chai kwa sababu ya joto. Eh nikasema hawa watu wanafaa tuwapelekee sukari bakshishi. Hii mvua ni natural resource, Kariuki thank you very much. Hii ni natural resource tena mna msitiu hapa, nafikiri watu wa Kakamega walisema Kakamega forest is a rain forest, so is Malava forest na hii ndio inasafisha hewa ya Kenya, inasafisha, usiku inatoa, si mnajua hiyo biology?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Adagala**: eh, inasafisha na inafaa tuwe na kitu .. hii mambo ingine ya mto, 60% of the waters of Lake Victoria are from Kenya, ingine ni Kagera, Ruanda, nafikiri moja iko Tanzania. Hiyo ina sheria ya 1928, hatutaguza mali ya Nile waters, hiyo ni Nile waters treaty, nafikiri unaijua? 1928, wakoloni walitengeneza na Egypt, haitaguzwa kwa sababu Egypt waliona, eh sasa watu wameanza kustawi watatuharibia maji yetu, na wao wamekuwa nayo, inatoka hapa mpaka inaenda wanafanya irrigation Egypt.

Sondu Mirie ndio hydro-electric dam pekee iko upande huu, kwa nini isiwe kwa Nzoia, na wameweka huko? Serikali ya Misri ilikubali ndio wakaweka, hiyo ni ukoloni. Hii maji yetu ambayo hatutumii ni ukoloni unafanya hivyo. Watu wa Rarieda, maji iko hapo lakini hawawezi kuweka mfereji wakilete kwa nyumba au… Ukiangalia hakuna mwisho na maji iko hapa, hauwezi

kuweka mfereji kwa sababu ya treaty, wakasema wanataka Law of the Lake. Pengine nyinyi mnafaa kwa sababu wao pia wanapokea maji yetu sivyo? Inafaa na huko Rarieda ni dry, sasa huko hakuna mvua, hapa ndio mvua.

Inafaa region hii itengeneze na mnaweza kuandika iweko na munaweza kusema tu hivyo, mueke vipengele tatu, nne ile amesema na wengine wamesema, Law of the river, ili hiyo treaty, na mseme hiyo treaty itolewe, usiseme tu vile unasema Kariuki, ufike hapa, unasema kuna treaty na hiyo treaty inafaa ikaguliwe.

Hatuwezi kupiga maji marufuku lakini watuletee tuhifadhi hii yetu, mazingara yetu, garabodi imeenda, kwetu kwa Kikuyu imeenda. Sijui kama mito imepunguka huku au nini, lakini kwetu hii mito midogo midogo, imekauka. Pengine watu wetu vijana wetu wapate kazi Egypt, wafanyi kitu, lakini hatuwezi kukaa tu kama vile tulikuwa 1928. Tuko watu thelathini million na wengi wako sehemu hii ya Lake basin.

**Opanda Wamalika**: Mimi ni Opanda Wamalika, nataka kuchangia mapendekezo kuhusu devolution of power. Saa hizi tunapata ya kwamba, ijapokuwa ilikuwako hapo awali hii majimbo, lakini central government zenye zimekuwa zimeharibu, sasa tuko na imbalanced development.

**Com. Adagala:** I want you to recall, new Kenya new Katiba …
**Opanda Wamalika**: Kwa hivyo nina-propose ya kwamba devolution of power ichukuwe muda kidogo ili central government iweze kujenga economic institutions kama University. Kwa sababu utapata district moja itakuwa na university nne, tano na ingine haina na tumekuwa tukitoa ushuru ambao unaenda kujenga hiyo university. Kwa hivyo central government should provide key academic institutions in different districts, ndipo sasa tunapojitegemea, tuna National school, tuna university na vitu kama hivyo asante.

**Com. Adagala**: Usisahau bado Province iko, usisahau province kama co-ordination, where did they put university? Lakini pia tutaweza kujijengea tukisema tu Panpaper na Mumias, Nzoia, we want a university, we tell them you are building a university, hii pesa yote wanapata na wahindi na wazungu ndio wanapata mshahara ya juu. Unasikia, don't forget a province also, bado iko, haiko na nguvu kama district lakini ina-co-ordinate okay?

And we put province there because of natural resources so that you can have a wide range of resources. So that if it is Rarieda, you don't have just this beach, na Bondo ina hii na Egypt na Busia ina hii, lakini kama huko Nyanza watakuwa na beach kubwa, watengeneze. Watu wa Nyanza, wacha nimgundulie, tumetembelea nchi, hawana hata cooling store, refrigeration kwa beach, hawana. Na factory ya omena iko Thika, factory ya Passion fruit ambayo nyingi inatoka Kisii na huku, iko Thika, okay? Vitu viwe pahali viko, they get value added there. If it is canning of Passion fruit, there, halafu inapelekwa na kazi inapatikana hapo. Watu wanalima, wanatengeneza, kazi inapatikana hapo.

Ikiwa hiyo pineapple iko Thika, factory ya pineapple iwe Thika okay. Endelea, sasa imebaki lakini mkumbuke devolution ndio exercise na wakina mama mkumbuke tunaleta devolution mashinani na msikalie masikio haya. Hizo boundaries tulisema kuna Commission yake.

**Vincent:** Sawa, tuangalie sura ya kumi na moja ambayo inaongea juu ya ardhi na mali. Kwa ufupi tu sura hii inasema kwamba ardhi ya Kenya ni ya watu wa Kenya na ardhi hii itamilikiwa katika daraja tofuati. Daraja ya kwanza itakuwa ni ardhi ya mtu binafsi, ardhi ya familia, ardhi ya jamaa au jamii na ardhi ya umma.

Ardhi ya umma itashikiliwa na Tume ambayo imebuniwa katika kifungu hiki ama sura hii. Ni Tume hii ambayo itashikilia maswala ya ardhi ya umma haswa maswala ya maeneo ya ardhi ya umma na pia hiyo itakayo kadiri kipimo cha ardhi ya umma. Kifungu hiki pia kinawalinda watu ambao wamemiliki ardhi lakini watu ambao kwa njia ya haki ndio wanalindwa.

Watu ambao wamepata ardhi yao kwa njia ya ufisadi watakaguliwa.

**Com. Adagala**: …. Inaitwa challenging the first registration, kama umeguza ardhi ya umma, ujue ujitayarishe, pengine hautapata heart attack, ujue itakaguliwa, ulipata wapi shamba hii, ulipata wapi hii. Na ninasikia watu wengine wanasema oh mimi nilipewa 100 au mimi nilipewa plot, hiyo allocation, ikiwa ulinunua sawa, ikiwa ulipewa kwa sababu una god father, uko taabani, ikiwa ulinyakuwa kwa mtu mwingine na nguvu, ile kiimla, kuna watoto wengine hata wamechukuliwa shamba lao. Hata huyu Commissioner Kangu vile mnamuona hivi, mama yake na baba yake, walifariki na nyumba kubwa ikachukua shamba yote. Sasa alikuwa yatima hivyo, akasomea kwa dada yake, sasa unaweza kufikiria mtu mkubwa kama huyu hawezi kuwa na shida kama hiyo, lakini hamjui alitoka wapi.

Na huko kweli hata wamezika mama yake mkubwa jana, na nikamuuliza, lakini na shamba yenu iko wapi na ndugu wako, akasema, wanalima, na wazee waliangalia ikichukuliwa. Wazee wanafaa, wazee wa kijiji ndio mambo ya land yote iko chini yao, na mlituambia hivyo, mambo ya Nairobi ni mbali okay. Ninasema wazee ndio wanajua, lakini wazee wakae wasidhulumu ma yatima na wajane, hao ndio wanaumia sana. Kutoka Busia mpaka Mandera, wanaumia kutoka Mombasa mpaka Turkana wanaumia sana, muangalie hiyo, watu wawe na haki zao, waendelee kwa usalama.

Family land itakuwa kwa joint ownership kwa sababu wa mama walisema baba anauza, kwanza wa Masaai, usipige pige mkono kabla sijamaliza. Wanawake wa Maasai wanasema mzee anakuja amekununulia rinda mbili, leso tano, halafu unasema lakini hakuuza ng’ombe, alipata wapi hii? Halafu baadaye ndio unagundua, oh ni ardhi aliuza kwa sababu hao hawaangalii ardhi sana. Lakini Mkikuyu amechoma hapo, Mjaluo amechoma hapo, Mluhya amechoma hapo, hawa ndio wananunua huko, anachukua kwa bei rahisi. Wanasema wengine wanauzia tu kwa bar, wakasema yao wanataka iwe communal land, title deed communal.

Halafu ndio itoke, ndio tunasema individual land, private land na communal title. Haiko hiyo ya crown tena, kwa sababu hiyo ni ya ukoloni imetolewa. *Isa imwamasanga kulamala*. Hii ndio hukumu ya mwisho, huko Laikipia, kuna wazungu ishirini na nne na wana lease ya 99 years, kutoka 1904 okay, sasa hiyo lease si …. Haikuwa ya kununua, sasa hawa wazungu ishirini na nne wana acre… Nimwambie au nisimwambie?

**Audience**: Sema.

**Com. Adagala**: Wana acre 800,000. Mmoja amejenga shule ya homeless children kutoka Westminster, hata ilikuwa kwa gazeti lakini unajua watu wa magazeti wanasema kitu wawache wewe mwenyewe ujigundulie, kulikuwa na hiyo. Westminster, watoto, street children wanatoka huko wanakuja shule na wale wa Laikipia wako kwa street.

**Alphayo Musungu**: Britian, wanakuja kusoma hapa?

**Com. Adagala**: Westminster Britain. Kwa sababu huyo mtu alichoka na hii shamba akasema ah, Westminster where I come from you can build a school there, they will be going there. Ukitaka unaweza kwenda iko hapo, 800,000 acres Masaai akisema sina shamba mnamuambia oh, (inaudible)You know ranch, inakuwa kama wa Masaai 6000 wako na 8000 acres, moja na nusu kwa kila mtu lakini kwa ranch.

Sasa Mmasaai hauwezi ku-complain uko landless, uki-complain wanakuambia join the ranch, sasa yao ranch wamekuwa wengi, wamezidi na vitu kama hivyo. Sasa shida yao ilikuwa kama kubabaika, hii lease inakwisha 2004 na itakuwa reviewed, itakuwa vipi? Hata hii ilikuwa shamba la baba yangu lakini ndugu zangu waliwenda na babu yangu, mbuzi zilipoenda hapo kula during drought polisi wakaja wakanishika na kunipeleka kotini, wakaniambia tress-pass.

Nilihurumia hao watu, hao wazungu wameweka electrical fence kupitia kwa barabara. Saa zingine ndovu wanakuja na wanavunja hiyo kwa miguu na wanapitia, sasa unaenda na gari na mnakutana na ndovu, vile utafanya pengine ni ku-reverse, na unajua hauwezi kuenda reverse sana, sababu ukienda huku, electrical, ukienda huku electrical fence, ukienda kule ndovu, watu wa mkogodo walisema hawaamini okay hiyo ni pengine ninawaambia tu. Lakini joint ownership itakuwepo, communal ownership itakuweko, na kitu kingine wakina mama, nilimuambia nyinyi saa zingine ndio mnarudisha mambo nyuma, ukitoka kwenu, ukifunga ndoa, uwe una shamba kutoka kwa wazazi wako.

Wasichana watarithi, sasa hiyo inabadilisha sana, mtu alisema hapa mapema nikasema, eh, wasichana wataridhi, atakuwa na shamba dada yako lakini mke wako pia atakuwa na shamba. Na tunasema shamba, shamba kwa sababu watu wengi waliotoa maoni walikuwa peasants. Hao wasomi walisusia, walisema, hata teachers hawakuja, hii mambo tumeweka hapa wazazi ndio wametuambia kuhusu teachers, walikaa tu mbali, na mambo yao yamesha suluhishwa hapa.

Kama mahakama, judges walikataa na wananchi wakatuambia mambo ya mahakama, wanasema iko hivi iko hivi, wangekuja wangesema lakini waliogopa kwa sababu ya ufisadi. Walijua mbele ya Tume tutawauliza je, na ufisadi, je kwa sababu

wananchi wanalalamika, okay? Wacha tumalize, nafikiri hiyo ni mambo ya land and property, sio iwe shamba pekee. Inaweza kuwa duka, inaweza kuwa shares na mtu tajiri duniani, Bill Gates, for him he owns a piece of the sky, he makes money from computers and a piece of the sky, unajua hiyo ya E-mail, hiyo yote iko huko juu.

Lakini ile ingine, anaishi kwa nyumba na pengine mtu atahitaji tu nyumba. Watu wa Lugari hapa wacha nimalizie na hiyo, walitoka Maragoli na Bunyore hasa, Lugari, na walisema tumetoka huko watu wako wengi, tukaja Lugari nikauza shamba acre mbili, nikaja Lugari nikanunua acre kumi, sasa nimegawanyia watoto wangu imebaki acre mbili mbili. Sasa tuko kwa hiyo tulianza nayo, sasa hiyo ingine itakuwaje na wakasema heri hata tungebaki huko, heri tungekuwa huko Vihiga na tungefanya iwe town na tungeishi tukipata kazi na nini. Kwa sababu hapa tumegawanya gawanya hata mwishowe mali ambayo ilikuwa inatoka kwa mashamba makubwa haiko.

That large scale farming is not there, okay?

**Alphayo Musungu**: Kwa jina naitwa Alphayo Musungu, upande ya land mimi nina deal nayo huko Lugari.
**Com. Adagala:** Juu ya?

**Alphayo Musungu**: Member wa land control board..
**Com. Adagala**: (inaudible)

**Alphayo Musungu**: Mimi ni member wa land control board na ni mzee kutoka Matete division, tunaona upande wa land kuna makosa upande wa survey. Fees ya survey iko juu sana na wananchi wengi wameshindwa ku-process mashamba, ingelikuwa iwe limit.
**Com. Adagala**: Umeturudisha Form one, kuna Commission on land, hiyo itashughulikia hiyo where were you when we were giving maoni?

**Alphayo Musungu**: Nilikuwako tu.
**Com. Adagala:** Na ulitoa hiyo maoni?

**Alphayo Musungu**: Nilitoa.
**Com. Adagala**: Yes, now you should be asking, where is it here, so we go to Form two, I will tell you the land Commission will deal with that na wananchi wengi walilalamika. Cost of title deed na most of it, walisema three thousand shillings au nini, hiyo ndani yake ina ufisadi. Na hiyo imekubaliwa kwa sababu wanakupa hata na risiti yenyewe, hiyo survey na title deed na demarcation, itakuwa Land Commission na tutapeleka (inaudible) na hiyo si ugumu, unafanya tu computer na inatoa mambo ya Land vuchu vuchu, inatoa. Haya, tuendelee. Tutamaliza in 15 minutes.

**Vincent:** Sawa tutaguzia tu mambo muhimu muhimu, tuko na sura ya 12 ambayo inaongea juu ya mazingara, sura hii inatunza mazingara yetu na mwanakenya ama kila mwananchi anapewa haki ya kulinda mazingira yake na pia ako na haki ya kuipeleka serikali mahakamani iwapo kuna uharibifu wa mazingara.

Kunabuniwa Tume katika sehemu hii, Tume ambayo itaangalia ama itakagua maswala ya mazingara na malalamishi yote kuhusu mazingara yatapelekwa mbele ya Tume hii. Sura ya 13 inaongea juu ya fedha za serikali, public finance.

**Com. Adagala**: Mazingara ni kulinda, kutengeneza, kufanya izae zaidi lakini bila kuharibu hewa na ardhi kama hii fertilizer tunaweka inaharibu lakini tumeiunga kwa hiyo mwishowe hata udongo si kitu, halafu pia lazima ufaidike, watu wale wako pale wafaidike. Mambo ya electricity, watu wa Turkwel walituambia hii stima hata jina yenyewe ni ya kiturkana lakini hapa hatuna stima, heri nyinyi mnayo huko kwenu. Watu wa Gachoka kule Jeremiah Nyagah anatoka, Kiambere ina hydro-electric dam tatu, wakasema hii vitu inapita juu ya nyumba inaenda Nairobi, Uganda, North Eastern, wanafikiri hata yetu inaenda Uganda, hawajui sisi ndio tunapata. Na kweli ukiona watu wa Gachoka, walisema heri tungekuwa tu hata ile ya kutengeneza madirisha, it is a very depressed place, hakuna chochote kinaendelea Gachoka.

Na wacha niwaambie kwa sababu ni ya kweli, Mzee Nyagah alinunua shamba na aka-divide kwa watoto wake, akawajengea kila mtu nyumba na maji kila nyumba, na stima halafu hiyo ndio sehemu inayo stima peke yake. Alikuwa Minister Nyagah, Minister mwingine ametoka hapo, MP pia ametoka hapo wa opposition, na Minister alikuja huyu kijana, akaja akatoa maoni na hakusema chochote kuhusu stima, lakini watu wake kila walikuwa wanazungumza ni stima, endelea.

**Jonathan Werengai Masinde**: Nafikiri… Jina ni Jonathan Werengai Masinde, hii mambo ya mazingara ni kitu muhimu zaidi hasa ninaona kama serikali inasema lakini haiwekei mkazo kabisa.

**Com. Adagala:** Njoo simama tu utakuwa na nafasi yako, serikali inasema na kusema tu, sasa iko kwa Katiba, ikiwa kwa Katiba, serikali ipende isipende- mtu Nassir amesema- serikali inasema kwa kura, hata wewe mwenyewe unaweza kusema, wanakuwa wazuri na nini, lakini sasa ni Katiba. Sasa tuzungumze vile Katiba inasema na vile unataka iendeleze, tusirudi old skin and old wine eh?

**Jonathan Werengai Masinde**: Ninapendekeza hivi kwa saa hii, tukihesabu ile mito ambayo tukonayo kwa kila district, ihesabiwe na ijulikane, hiyo mito yote lazima ihifadhiwe ili si mtu mmoja kwa sababu shamba yake ati imefika karibu na mto na aingilie mto. Hii itatusaidia nchi yetu kuhifadhi mazingira yetu kwa vizazi vijavyo. Tusipofanya vile na saa hii karibu mito ingine inaanza kukatika.

**Com. Adagala**: Kwa sababu ya upungufu wa catchment areas, mto kabisa imekauka huku, iko hivyo, *ledikaho ndyo*?
**Audience**: eh.

**Alphayo Musungu**: Mimi ninazungumza kwa ajili ya pollution, tungelipenda sheria… Kwa jina Alphayo Musungu. Ninazungumzia juu ya mazingira, hii factory ya Webuye imeharibu mazingira yetu. Tulikuwa tunapanda machungwa na lemon, ndimu, sasa hakuna imekwisha kwa ajili yote ilikauka. Kwa hivyo tunapendekeza tuwe na sheria ya kuzuia pollution ambayo inatoka Webuye.

**Com. Adagala**: Na kumbuka vizuri tukiwa watoto tulikuwa tunapiga mpira malimau, ndio wanaita hivyo?
**Audience**: eh.

**Com. Adagala:** Na huko ng'ambo hiyo limau ina bei, hata Nairobi ina bei, hata wewe hauwezi kuinunua. Lakini ilikuwa tu mpira halafu unataka kukula chungwa unachukuwa, ilikuwa kidogo kama paradise, unataka ndimu kwa uji unafanya tu hivi, ni citrus fruit zote.

**Cllr. Nalyanya**: Ni Cllr. Nalyanya, mimi pendekezo langu ni kwamba vile mzee Werengai amesema kuzuia mazingira isiharibe kutoka kwa mto, iwe metres saba ndio mtu alime abakishe. Otherwise unakuta mtu anatoa udongo kwa maji halafu anapanda hapo halafu mito inakauka.

**Com. Adagala**: Au tuhifadhi sehemu fulani hata inaweza kuwa zaidi ya hiyo au iwe kama kwetu sasa, wanapanda majani na majani ni kama mti, okay? Lakini hiyo pia udongo wetu unaenda Egypt na wao wanafurahia. Tukiwa na erosion huku, wanafurahia huko kwao. Haya, malizeni.

**Samuel Sifuna**: Kwa majina ni Samuel Sifuna. Kulingana na mazingira, pendekezo langu lingelikuwa hivi, kuna watu au wanakenya wale ambao walipewa makao katika sehemu za milima za chemichemi, ningependekeza waondolewe ili wapatiwe mahali pengine.
**Com. Adagala**: Kama wapi?

**Samuel Sifuna**: Kama hii scheme mpya, watu wamepewa kwa milima, na huyu DC mpya wa Lugari, wamepewa kwa milima, kwachemi chemi.

**Com. Adagala**: Ndio mambo mengine tumemuambia ni ya Parliament lakini hapa ikisema mazingara au mazingira ihifadhiwe, basi hizo laws pengine zinatoka kwa Parliament. Lakini watu walipewa ardhi hasa wale walikatiwa msitu, mchunge. Pengine wewe pia ulikuwa na hatia lakini kukata msitu na ninakumbuka sasa iko 2%, sehemu mbili kwa mia moja, ikiwa uko na acre mia moja Kenya, sehemu mbili ndio msitu pekee. Lakini mlinde hii ya Malava, mnailinda?

**Audience**: Imeisha, ni kwa barabara tu…

**Com. Adagala**: Iko tu barabara?

**Audience**: Eh.

**Com. Adagala:** mimi ninapitia tu barabara, you should demand it goes back to where it was like 19 something, vile ilikuwa full.

**Vincent:** Sura ya kumi na tatu inaongea juu ya mali ya umma ama fedha za umma. Kwa muktasari tu, sehemu hii inasema kwamba, fedha za umma zitalindwa na kuna afisi ya Auditor General na Controller General ambazo zimewekwa katika Katiba hii na Bunge limepewa uwezo wa kupitisha fedha za umma ama kuidhinisha matumizi ya fedha za umma. Serikali pia imepewa uwezo hapa wa kupata mikopo kutoka nchi za nje. Tena sehemu hii imebuni banki kuu na Governor wa banki kuu na afisi fulani fulani.

Ukaguzi wa fedha za umma umepewa kipao mbele katika sehemu hii, pia nitaongea juu utumishi wa umma. Utumishi wa umma uko katika sura ya kumi na nne na yafaa tuelewa kwamba utumishi wa umma sasa utakuwa watu ambao watashikilia nyadhifa mbali mbali katika umma watakuwa ni watu ambao wamehitimu au ni watu wako na ujuzi katika nyanja tofauti tofauti. Na katika sehemu hii, imebuniwa huduma ya polisi, sasa sio kikosi cha polisi ama police force, lakini ni huduma ya polisi ambayo itakuwa chini ya Commissioner ambaye atakuwa amehitimu kutoka chuo kikuu, na polisi ama ma-afisa wa polisi watatoa huduma kwa watu.

Sasa ni wanaotoa huduma, ni police service sio police force, hawatakuwa watu wa nguvu. Pia kuna correctional services ambayo ilikuwa idara ya magereza, sasa itaitwa correctional services. Idara hii itakuwa na wajibu wa kubadilisha watu wenye vitendo vibaya vibaya katika jamii na watu hawa pia wataweza kupewa ujuzi. Watakuwa pia chini ya Commissioner ambaye atakuwa amehitimu kutoka kwa Chuo kikuu.

Sura ya kumi na tano inaongea juu ya ulinzi. Sura hii imebuni baraza la ulinzi, Rais bado atakuwa ni Amiri Jeshi Mkuu lakini atasaidiwa na baraza ambalo litakuwa na wanachama kama Makamau wa Rais, waziri ambaye anahusika na maneno ya ulinzi, na makamanda tofauti tofauti ambao ndio wataufikia uamuzi wa kutangaza hali ya hatari ama kutangaza vita.

Kuna National Security Council ambayo iko katika sehemu ya 272, Bunge pia litawakilishwa ama Bunge litahusishwa katika maswala ya security, haswa katika maswala ya kutangazwa kwa hali ya hatari. Pia kuna sura ya kumi na sita ambayo inaongea juu ya leadership and integrity, uongozi na hali ya kuhakiki au hali ya ufisadi. Kumebuniwa Tume katika sehemu hii ambayo itaangalia mambo ya ufisadi na watu ambao watashikilia nyadhifa kuu katika serikali, hasa Rais, Waziri Mkuu, mawaziri wasaidizi, na watu ambao wanashikilia nyadhifa ambazo ziko katika Katiba hii, itabidi wa-declare ama watambue mali yao kabla ya kuchukua nyadhifa mbali mbali katika serikali.

Mambo ya ufisadi pia yameshugulikiwa katika sehemu hii. Ufisadi sasa umeondolewa na nimesema ni haramu na kwamba kutakuwa na Tume ambayo itachunguza maswala ya ufidsadi. Katika sura ya kumi na saba.

**Com. Adagala:** Nafikiri this morning on the news items there was something on integrity. Kitu kimebuniwa kwa radio, pengine tutasikiliza kwa radio. Kumekuwa na kitu kimebuniwa, something something integrity, nafikiri watu wamejua nchi inabadilika sasa wanajaribu kuweka anti-corruption, anti-this. Lakini corruption itakuwa zero tolerant, hii vitu mumekuwa munasikia barabara fulani, oo imepakwa lami lakini bado ni ya udongo kwa sababu katibu alichukua pesa akaweka kwa mfuko au akapeleka kwao. Hiyo yote yatakaguliwa, where is this, where is that, who was there na pia kutoka sasa Parliament itakuwa ikiangalia hiyo ili vitu vitekelezwe, where the budge has been put, it must sent for that purpose, not tricking people around again, okay?

**Vincent:** Sura ya kumi na saba inaongea juu ya Tume tofauti tofauti ambazo zimebuniwa katika mswada huu. Kuna Tume kumi na Tume hizi tumezitaja hapo awali, lakini kupitia tu, baadhi yao ni kama Tume ya haki za binaadamu, Tume ya leadership and integrity, Tume ya mishahara, Tume ya walimu, Tume ya Katiba, baina ya Tume zingine.
Maswala ya mishahara yote ya watumishi ya umma sasa inakadiriwa na Tume na hizi Tume zingine pia zina kazi zao ambazo ziko katika mswada huu. Sura ya kumi na nane inaongea juu ya amendment ama kubadilisha Katiba. Katiba itabadilishwa kupitia kwa Bunge, idadi ya kura asili mia sitini na tano katika nyumba zote mbili lakini kuna maswala tofauti, maswala kama ya haki za binaadamu, maswala ya mipaka ya Kenya na maswala ya uraia, haitaweza kubadilishwa bila tu kwa kuuliza wananchi kupitia referendum.

Ufafanuzi wa Katiba uko katika sura ya kumi na tisa na mahakama imepewe uwezo wa kufafanua Katiba. Tunaambiwa kwamba Katiba sasa itafafanuliwa na mahakama tofauti. Mahakama ya Supreme Court ndio itakuwa mahakama ya juu zaidi. Halafu mwisho tuko na sura ya ishirini ambayo inaongea juu ya transitional and consequential provision, ama maswala ya daraja. Hayo yako katika nyongeza tofauti, schedule nazo ziko hapa. Na Commissioner wetu ameongea juu ya transition provision vile tulikuwa tukiendelea.

**Com. Adagala**: Twenty Chapters, okay mnaona vile hiyo ya mwisho imeenda haraka kwa sababu tulikuwa tumefafanua sana huko mbele hata wale wameenda wamepata hii. Sasa hii ingine inabaki ni state law, hiyo ni diesel. Mtaichukua na mtaisoma, changu kitabu kiko tofauti kwa sababu ya macho yangu, wali-print yangu kwa bold kwa sababu hiyo vitu vidogo vidogo *zafwana mavas gajendanga*.

Roundup, five minutes ten people, nusu minute kama kuna na watu wanataka kusema. Kama mumechoka pia mumechoka lakini naona wazee walienda, walitaka kusikia hiyo mambo ya boundary lakini ni sawa kwa sababu inawaumiza sana. Simama

hapa watu ten, half a minute.

**Cllr. Nalyanya**: Mimi ni Councillor Nalyanya, ningependekeza kwamba , mambo ya Katiba kugeuza ama kuwa amendment isiwe tu simply 65% ya Parliamentarians lakini wananchi wahusishwe kwa referendum.

**Com. Adagala**: ….. zamani walikuwa wanasema kuna wenye nchi na wananchi, tuko tu na wananchi. Yule anaona ako mkubwa sana kuliko wa Kenya wengine, aende mahali kwingine, tuko wote sawa mbele ya Katiba. Mwingine huko nyuma, nafasi ya five minutes tufunge, public service, public finance, defence, ulinzi yote hiyo.

**Jotham Mwambia**: Mimi kwa majina ni Jotham Mwambia na ningependa kusema ile wasiwasi ninayo, ningependa kuwasihi ninyi ma Commissioners, mtoe pendekezo ili kwamba iwapo huyu rais ambaye tuko naye anaweza kuvunja Bunge ili …

**Com. Adagala**: Unaniona hivi, niko blank hapa, wewe ndio utatoa pendekezo hilo na sisi tutaandika. Tafadhali muelewe Commission haibuni kitu chochote, inaandika, inaorodhesha, inapanga lakini wewe ndio utatoa hilo pendekezo.

**Jotham Mwambia**: Ninapendekeza kwamba hata ikiwa yeyote yule ambaye ana mamlaka wakati huu, atatumia nafasi yake kupuuza kwa kukuja Bunge, ile Bunge ambaye itakuweko, ningependa itilie maaanani haya mapendekezo ya Commission na yapate kutimizwa wakati wa kipindi tunacho elekea asante.

**Com. Adagala**: Niseme ni kama zero sum game, unajua zero sum game, hatujaendelea kwa sababu umempa nafasi. Umempa nafasi aendelee sasa hii vitu vyote mpaka mwaka wa 2007. Hatujui kama Yesu atakuwa amekuja mwaka ujao au ile ingine au 2007, sasa wanasema ni seven years from millennium, sasa hiyo hatutahitaji, tutakuwa Mbinguni. The kingdom of God will have come.

**Jotham Mwambia**: Nilikuwa na wasiwasi.

**Com. Adagala**: Wasiwasi wako umeupa msingi sana kwa sababu umesema iendele mpaka 2007 na hiyo tutakaa tu.
**Jotham Mwambia**: Hapana.

**Com. Adagala**: Tutakataa, tutakuwa kwa hii ya… Wananchi watakuwa wamebadilika na watakuwa wanaishi kwa Katiba ya zamani. Tena wananchi ndio watakuwa new wine, na itakuwa inaishi na old bottle, itapasuka tutakuwa na unrest. Haya, mtu mwingine?

**Cllr. Nalyanya**: Mimi Councillor Nalyanya ninapendekeza kwamba Katiba hii itumike kabla ya uchaguzi yaani uchaguzi ufanywe chini ya Katiba hii na wasipofanya hivyo, twende hata kwa civil disobedience.

**Com. Adagala**: Councillor, hiyo unajua sasa hiyo itakuwa kwa maandishi, tuliuliza watu wa magazeti waje, lakini unajua hata kama tunasema ufisadi uko mahali kwingine, kwa magazetii iko. Councillor?

**Cllr. Nalyanya**: Madam.

**Com. Adagala**: Councillor unajua, there are so many things, mliona hata Ghai alikuwa kwa demonstration? Councillor, don't wait for it not to be used, there is a problem of time, the clock is ticking, October 30th budget is finished, na hiyo ndio haja serikali inayo pekee, hii vitu vingine hawana haja. The clock is ticking, mimi msichana M-Quaker sisemi ili iwe na violence. Ninaelewa civil disobedience. Lakini, vijana wa Kakamega wamefanya history na nyinyi Councillors munaketi. You will not do it then, you can't wait for Bunge to be adjourned or dissolved or whatever then you do it, you have to do it within the time before they do it.

**Interjection**: (inaudible)

**Com. Adagala**: (inaudible) ……… hatakuwa na quorum hata moja na anasema ni jukumu langu, atasema na itakuwa kwa sheria sasa unataka uongoje avunje ndio uanze kuandamana. Time, time, Councillor small problems of time, it is ticking away. Unajua wananchi wanataka, wanapenda, lakini hata Western Province mumenyamaza tu hakuna habari imetokea Western Province.

**Interjection:** We say, but they don't write.

**Com. Adagala**: Go and look at the press there with all your Councillors those who really think have not appeared in the., wewe uko mwerevu umekuja hapa, wengine hawaja kuja, chukua hata wakina mama waende hapo, kuandamana ni haramu lakini mtakuwa mumefika hapo na mseme kwa press, museme tunataka, (inaudible). Lakini Western Province, mumenyamaza, kwa sababu (inaudible) for candidate, hiyo ya candidate(inaudible). Tulipofanya Kakamega, sisemi muende kufanya hivo, even writing and facing to all the newspapers, Councillor so and so, so wamesema hivi, na m-fight, maisha yenu itakaa kwa ….. hapana, Mrs. Werengai being a delegate ……….

**Mrs. Werengai**: Wengine tunaandika lakini hawa…

**Interjections:** (inaudible)

**Com. Adagala:** Muende mufanye fax, mnunue fax nzuri , hiyo ungenunua sweater au kitambaa, weka kwa fax iende kwa magazeti, one of the newspapers. 'Not al etter' a press release from the constituency, okay?

**Interjections:** (inaudible)

**Com. Adagala**: Asante, I am glad I came back to Matete, kwa sababu pengine angekuwa Commissioner mwingine hangeelewa hizi nini zenu, na ilinichukua a couple of one or two hours to get back the awareness I had Councillor, I am glad I got it kwa sababu tu nilichukua tu tena oh, niko Malava hii sehemu ya Kabras na ile ya Lugari ni. Sasa ningeenda Lugari, Lumakanda lakini inafaa niende kwa hospitali hiyo ya Kaimosi wapasue hili jicho lingine ili nione vizuri. Sasa nikaona nikienda kule na kurudi huku itakuwa muda. Sasa Commissioner Kangu atakuwa Lugari na mimi nitaenda County Hall Kakamega.

Na unajua, take advantage of your misfortune, come to Kakamega, it is a misfortune you have. You must always make the most of adversity, ukiwa na shida fulani, itumie ili ufaidike. Si mko huku na kule, kujeni pia Kakamega wale ambao munaweza. Najua two days is… lakini kesho, wale ambao mkitaka zaidi itakuwa kama revision kwenu. Asante sana, nataka kuona kamati tukutane nao kidogo, wameenda wengi, wameenda?

**Kamati**: Tuko.

**Com. Adagala:** Kamati tutakuwa na nyinyi five minutes at the most kwa sababu inafaa mpange kitu fulani na District Co-ordinator na your representatives for the National Constitutional Conference who are not here. They should be at Lugari tomorrow, okay? So that they can know the things you are saying, okay? Hiyo ndio hiyo tu.
Mtu aniambie Burudi Nabwera ako wapi.

**Audience**: He is in Lugari.

**Com. Adagala**: Will he be in Lugari? Okay, mkiweko muambie tu tuliweka Kitabu cha kumbukumbu cha mzee na picha yake na mzee Solomon Adagala iko hapo ya New York. Asanteni Mungu amubariki, pendekezo zenu zote zitimizwe, God bless Kenya.

**Amaswachi Temba**: Sina mengi ya kusema, when you started this session I never introduced myself. I am the Co-ordinator. My name is Amaswache Temba, I was with my Assistant John Kariuki. I am happy we have done our best, Matete was the best, it recorded the best in Lugari district and we started on a high note and finished with a high note.

Let me thank the few who have taken trouble to stay upto now, it needs dedication because this Constitution that we are working for, needs our dedication and hard work and commitment and the way the Councillor said it, even if it means watering our blood, we shall do it because we have committed the cause of serving this country through this Constitution. Before I finish, I will give the Chairman of Malava 3C's Mr. Wanjala a minute to say a word and then Ms. Mukolwe to pray for us.

**Chairman:** Asante sana Bwana Co-ordinator, langu ni kurudisha shukrani kubwa kwa wale wote ambao walikuja, ingawa wengi wameenda lakini ninawashukuru ninyi ambao mlibaki. Ninapenda kumshukuru Commissioner Kavetsa na team yake sana kwa mambo yote, kwa kutusomea Katiba yote chapter ishirini na tena walifanya kazi nzuri sana. Ningependa mumpigie clap, moja …………Asante.

**Ms. Mukolwe**: Asante tuamini na tuombe. Asante Baba Mungu kwa wakati huu, tunakushukuru kwamba siku nzima kabla hatujapanga leo, wewe mwenyewe uliweza kutupatia, tazama Mungu baba tumekaa hapa pamoja na Commissioner wetu na wananchi wote, tukiizungumzia nchi tunavyotaka iendelee.

Na tazama Mungu Baba haya yasiwe matakwa yetu pekee yetu bali, yadhinishwe na wewe. Angalia tunafika ukingoni na watu tunataka kutawanyika kila mtu aende kwake nyumbani. Tunakuomba kwamba katika safari hiyo, tunaomba Ma-Commissioner wetu ambao watatumia gari, Mungu Baba uwe Mlinzi, Dereve na Macho katika ile gari. Na kuna wengine kati yetu ambao pia watatumia magari na bicycle na miguu, Mungu baba uwe kiongozi wao. Na utujalie tena wakati mwingine ambao tutaweza kutana, tugawanyike mwilini bali roho zetu na nia zetu ziwe pamoja.

Tunaomba tukiamini na ni katika pendo la Bwana wetu, aliye Bwana na mkombozi wetu – AMEN.

Meeting ended at 6.40pm.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**